

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 21 Juni, 2005

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2005/2006.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

Viongozi Walioshika Nyadhifa mbalimbali Nchini

SPIKA: Bahati mbaya Mheshimiwa Chubi, swali lako halikumfikia Waziri kwa wakati ili aweze kuandaa jibu. Kwa hiyo, kwa leo halina jibu, lakini litapewa nafasi nyingine. Ahsante.

Daraja la Godegode

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga daraja la Godegode na kwa kuwa, ahadi hiyo hajiatekelezwa hadi sasa:-

- (a) Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kutokutekeleza ahadi hiyo?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, kujengwa kwa daraja hilo kutasaidia sana magari kupita bila matatizo?
- (c) Je, Serikali inafahamu kwamba, barabara kutoka Mpwapwa – Manghangu – Kimagai hadi Godegode ni kiungo kikubwa kati ya Jimo la Mpwapwa na Kibakwe, hivyo kujengwa kwa daraja nililotaja kutasaidia sana mawasiliano ya barabara katika majimbo hayo mawili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali Na. 4411 la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu za kimsingi za kutotekeliza ahadi ya kujenga daraja la Godegode ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Halmashauri ya Mpwapwa inashauriwa kuleta maombi ya kujenga daraja hili wakati watakapouwa wanawasilisha miradi ya barabara itakayotekeliza chini ya mradi wa *National Road Transport Program* itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kujengwa kwa daraja hilo kutasaidia magari kupitia bila matatizo katika eneo hilo, hasa kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo ambayo inaelekea kwenye Bonde la kilimo cha umwagiliaji la Lumuma kwenye uzalishaji mkubwa wa mpunga na vitunguu.

(c) Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali inafahamu kuwa, kujengwa kwa daraja hilo kutasaidia sana mawasiliano ya barabara kati ya majimbo ya Mpwapwa na Kibakwe. Aidha, kwa kutambua umuhimu huo Serikali imekuwa ikiifanyia matengenezo barabara ya Mpwapwa-Lumuma kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka 2003/2004, kilometra 25 kati ya Mpwapwa na Godegode zilifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara pamoja na ujenzi wa makalvati yenye kipenyo cha mm

900 na urefu wa mita 42 kwa ghamara ya shilingi 27,948,000.00 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Mwaka 2004/2005 Halmashauri ilipanga kuyafanya matengenezo maeneo korofi yenye urefu wa kilometa 4.5 kati ya Godegode na Pawaga kwa jumla ya shilingi 26,000,000.00 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara. Mkandarasi kwa ajili ya kazi hii amekwisha patikana na Mkataba kati ya Halmashauri na Mkandarasi umesainiwa tarehe 13/06/2005.

Mheshimiwa 2005/2006 Halmashauri imetenga shilingi milioni 8.2 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mara kwa mara, *routine maintenance* kilometa 20, kilometa 2 matengenezo ya sehemu korofi *Spot Improvement* kwa shilingi milioni 2.6 na kilometa 1.5 matengenezo ya muda maalum *Periodic Maintenance* kwa shilingi milioni 9.9 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyoyatoa hapo juu yanaonyesha ni jinsi gani barabara ya Mpwapwa – Lumuma inavyopewa umuhimu katika kuifanya matengenezo ili iweze kupidika wakati wote. Ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwa ufuatiliaji wake wa karibu katika masuala mbalimbali ya maendeleo katika Jimbo lake. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wakazi wa maeneo haya kuwa wavumilivu mpaka hapo fedha za ujenzi wa daraja la Godegode zitakapopatikana.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Ni kweli fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Swali, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba pamoja na matengenezo ya barabara hiyo kama daraja halitatengenezwa itakuwa ni vigumu sana kwa magari kupita kwa ajili ya kusafirisha mazao pamoja na abiria katika Kata za Godegode, Lumuma na Mbuga?

Swali la pili, kwa kuwa barabara ni maendeleo, barabara ndiyo uchumi wetu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kama alivyosema kwamba tupeleke maombi ya kuomba fedha kwa ajili ya matengenezo ya daraja la Godegode na tayari tumeshapeleka taarifa hiyo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kufuatilia hilo ili daraja hilo la Godegode liweze kujengwa? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwa kiasi fulani kwamba daraja lile kama halikutengenezwa inaonekana kana kwamba juhudhi hizi tunazozifanya sasa hivi ni kama vile hazina maana. Lakini naomba tu nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ile inahitajika kupidika muda wote ikiwa ni pamoja na kiangazi. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, ndiyo maana unaona jitihada za matengenezo ya barabara zipo kurahisisha angalau wakati wa kiangazi wakati ufumbuzi wa kudumu unapatikana.

Lakini pili, hili la kufuatilia kama nilivyosema mradi tumekutamkia kwamba ukiwasilisha jambo hili katika mpango huu tuliuoutaja kazi ya Ofisi yetu kwa kweli itakuwa ni kusaidia kuhakikisha kwamba mpango huo unakubalika. Lakini vile vile naomba nisikukatishe tamaa muendelee vile kutumia utaratibu wa kawaida wa Bajeti kupidisha maombi haya Mkoani kwa sababu nao ni utaratibu ambaa vile vile unawenza ukatusaidia kupata fedha kwa ajili ya daraja hilo.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo moja la nyongeza na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo amekuwa akiyatua Bungeni hapa. Tatizo la madaraja lipo pia Wilayani Kongwa ambako tuna tatizo kubwa sana kati ya Kongwa, Sagara na Iduo na daraja la Mkutani na uwezo wa Halmashauri ya Wilaya kutengeneza au kujenga madaraja haya ni mdogo kabisa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya mfuko wa barabara kuongeza asilimia ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa TAMISEMI ili fedha hizo ziweze kuongezeka na kuziwezesha Halmashauri zetu kuweza kujenga madaraja zenyewe? (*Makofî*)

SPIKA: Mfuko wa barabara uko Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ipo Sheria ambayo Mfuko wa Barabara inatumia na inaelekeza wazi kabisa kwamba asilimia 30 ya mapato hayo yatakwenda TAMISEMI kama Sheria hiyo haijabadilishwa Mfuko wa Barabara hautaweza kufanya chochote.

SPIKA: Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge niwatambulisse wageni mashuhuri walioko kwenye *Gallery* ya Spika. *Honourable Members, I wish to recognise the presents in the Speaker's Gallery of Fellow Parliamentarians from Kenya, Uganda, Rwanda and Burundi. They belong to an Organisation called The Parliamentary Network on World Bank, East African Chapter. You are most welcome. (Applause)*

Na. 102

Cheti cha Kuzaliwa

MHE. ABDULA S. LUTAVI aliuliza:-

Kwa kuwa katika dunia hii ya sasa sote tunafahamu manufaa na faida ya kuwa na cheti cha kuzaliwa na hali halisi inaonyesha kwamba, idadi kubwa ya Watanzania wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawana vyeti vya kuzaliwa ambavyo ni kumbukumbu muhimu sana ya uzawa wetu:-

Je, kuna uvunjaji wa sheria yoyote ya nchi kwa mtoto aliyezaliwa Tanzania kutopatiwa cheti cha kuzaliwa?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Masuala ya uandikishaji wa vizazi na vifo yanasmamiwa na Sheria ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 ya Sheria za Nchi. Sheria hiyo inataka kizazi au kifo kilichotokea, kuandikishwa katika Daftari la Vizazi na Vifo la Wilaya husika.

Sheria inamtaka baba au mama wa mtoto, au kama wote hawapo, mkazi wa nyumba ambapo kizazi kimetokea, kuandikisha kizazi hicho kwa Msajili wa Vizazi na Vifo wa Wilaya kilipotokea. Ni kosa la jinai kutoandikisha kizazi. Wakati Sheria husika ilipoanza kutumika, kizazi au kifo kilichowahusu Waafrika hakikulazimika kuandikishwa na hivyo kosa la jinai la kutoandikisha kizazi halikuwahusu wazalendo.

Hata hivyo, Serikali ilianzisha Mpango wa Usajili wa Lazima wa Vizazi, *Civil Registration Programme*, hapo mwaka 1979 kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la idadi ya watu *UNFPA*. Hadi kufikia mwaka huu wa 2005, Mpango huu umekwishafikishwa kwenye Wilaya zote Tanzania Bara isipokuwa Wilaya ya Sumbawanga, ambayo nayo itafikiwa ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, chini ya Mpango huu na kwa kuzingatia masharti ya Fungu la 27 la Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Serikali ilitoa mwongozo wenye nguvu ya kisheria kadhaa kati ya mwaka 1979 na hivi sasa kufanya usajili kwenye maeneo au Wilaya ambazo programu imefanyika kuwa ni wa lazima. Kwa kuzingatia matengenezo hayo, suala la usajili wa vizazi sasa ni la lazima katika maeneo mengi ya nchi.

Hivyo basi, ni dhahiri kwamba kutokana na utaratibu huu, hivi sasa ni uvunjaji wa sheria wa nchi kwa mtoto aliyezaliwa Tanzania kutosajiliwa na hivyo kutopatiwa cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, napenda niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuandikishwa na hivyo hawana vyeti vya kuzaliwa, kwamba Sheria hii inahu na kulifanya kuwa kosa, kutosajili vizazi vipya. Aidha, kwa mujibu wa Fungu la 19 la Sheria ya Vizazi na Vifo, uandikishaji nje ya muda, *late registration of birth*, unakubalika na hivyo kuwawezesha kupata vyeti vya kuzaliwa. Ingawa siyo kosa la jinai kwa wale waliozaliwa wakati usajili haukuwa wa lazima kutokuwa na vyeti, wanashauriwa Waheshimiwa Wabunge watumie utaratibu huu wa *late registration* kujisajili na kupata vyeti.

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize maswali angalau mawili ya nyongeza. Pamoja na ufasaha wa majibu aliyyoatoa Mheshimiwa Waziri juu ya swali hili. Nilikuwa nataka niulize tu kwamba sasa kwa vile inatajwa kuwamba ni kosa la jinai na inapotajwa kwamba ni kosa la jinai wananchi wengi wanaonekana bado hawajalifahamu hili. Mheshimiwa Waziri anaona

umuhimu wa kuhakikisha kwamba ili kosa hili lisiendelee kutendeka katika maeneo ya vijiji inatakiwa elimu hasa wananchi hawa wapate kulielewa? (*Makofii*)

La pili, Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba niulize watu wanatoka maeneo ya Mangombya kwenda Tandahimba, wanatoka Bulumkuti kwenda Tandahimba, wanatoka Chikongo kwenda Tandahimba, mwendo huu ni mrefu sana. Sasa kama kweli kazi hii inatakiwa ifanyike vizuri katika maeneo yote ambayo wananchi wetu wanaishi haoni umuhimu kwamba sasa kazi hii ya kutoa vyeti na uandikishaji wa vifo na vizazi ingefikishwa mpaka hata kwenye maeneo ya Kata hasa ikitanguliwa na elimu? (*Makofii*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na yeze kwamba ipo haja ya kuweza kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili la kujiandikisha kwa upande wa vizazi na upande wa vifo. Natumaini kwamba baada ya Ofisi ya *Administrator General* kubadilika kuwa *Executive Agency* kutakuwa na ufanisi mkubwa zaidi wa kulisimamia suala hili.

Suala la pili, ni kweli wananchi inabidi waende mbali kuweza kujiandikisha. Lakini mpango ambao tunao sasa hivi au programu iliyopo sasa hivi ni kwamba vizazi vinaweza vikaandikishwa pale panapotokea katika hospitali. Lakini suala la usajili inabidi mtu aende katika Ofisi ya Katibu Tawala. Na sababu zenyewe ni umuhimu kwamba ifanyike katika maeneo hayo. Kwa sababu hawa ndiyo waliioteuliwa kufanya kazi hiyo na hizi *documents* ni hatari kama zitawekwa katika ngazi ya Kata. Kwa hiyo, kwa sababu hizo za usalama inabidi tuendelee na utaratibu wa kuwafanya Makatibu Tawala kufanya kazi hiyo.

SPIKA: Kanuni zinaruhusu maswali yasizidi matatu, kwa hiyo, tutumie nafasi zote tatu.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Ofisi za Kijiji kwa sasa ndiyo zinazotunza rejista za wakazi na kwa kuwa Ofisi hizi ni Ofisi za Serikali na kwa kuwa ziko karibu na wananchi. Je, Wizara sasa iko tayari kuleta mabadiliko ya Sheria ndani ya Bunge ili *registration* hiyo iweze kufanyika kwenye Ofisi za Vijiji? (*Makofii*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, tatizo siyo sheria, sheria tunaweza tukaileta hapa wakati wowote. Lakini Sheria itafanya kazi kweli. Sheria itafanya kazi katika ngazi ya vijiji, hatuna uwezo huo. Hatuna usalama wa kutosha wa kuweza kuvitunza vyeti vile na vyeti hivi ni muhimu katika suala zima la uraia. Kwa hiyo, ni vyeti ambavyo ni nyeti. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba twende hatua kwa hatua. (*Makofii*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ndogo. Kwa kuwa mara nyingi tu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba bei ya cheti ni ndogo na umetolewa mfano na Mheshimiwa Lutavi kwamba mtu anapotoka kijijini kama Bweni, Jojo kufika Kilindoni kufuata cheti kuna gharama za usafiri ambazo zinazidi zaidi ya shilingi 3,000 ukichanganyika na zile zinakuwa zaidi ya elfu sita na.

Kuna mtoto ambaye anataka cheti kwa zaidi ya miaka 16 gharama yake inakuwa kubwa. Je, kwa nini Serikali isiweke kiwango kile kile cha shilingi 3,500 pale Wilayani ili ule mpango wa kuzidisha baada ya miaka 16 gharama zake ziwe kubwa usiondoke na wananchi wote Watanzania waweze kupata vyeti hivyo kwa urahisi? (*Makofsi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kweli tatizo linavyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge na uwezo mdogo kwa baadhi ya wananchi wetu. Lakini kama Serikali ilivyokuwa inaelezea humu Bungeni, kwanza jukumu jamani la kuhakikisha kwamba watoto ambao tunawaleta duniani, ni letu sisi kama wazazi hasa kama kweli shilingi 3,000 zimekuwa ni mzigo kwa mzazi na tukio ni moja tu. Mimi nadhani tutakuwa na tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili limekuwa linaulizwa mara nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge, Serikali iko tayari kuangalia ni jinsi gani tunawenza tukaliangalia suala hili ili tuweze tukakidhi hoja hii. Lakini la msingi wajibu wetu kama wazazi ni vizuri pia tukautambua. Nakushukuru. (*Makofsi*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tendo la kujifungua ni la furaha na jamii yote inakuwepo pale baba na ndugu na kwa kuwa Serikali na hospitali zake za Serikali au za Misheni au za Mashirika mengine ya binafsi zinathaminiwa na zinakubalika na jamii hasa Daktari wa Wilaya au Daktari wa hospitali inayohusika pale ya Kanisa au vipi.

Je, Serikali inaonaje kuandikisha watoto pale pale wanapozaliwa kwa sababu baba yuko, mjomba yuko, anaondoka wakati anapotengeneza utaratibu wa kumtoa mtoto pale kliniki na wengine wanafanya mambo ya cheti za kuzaliwa? (*Makofsi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, suala ambalo linagomba hapa ni kule kusajili. Kusajili ndiyo kuna matatizo, kwa ajili ya usalama wa vyeti vyenyewe. Lakini suala la kuijandikisha utaratibu upo. Kwa hiyo, pale pale mtoto anapozaliwa ikiwa ni hospitali, ni mahali popote anaweza akajiandikisha.

Na. 103

Hakimu wa Mahakama za Mwanzo – Kondoaa

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wilayani Kondoaa:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri na kuwapanga Mahakamu husika kwenye Mahakama hizo Wilayani Kondoaa?
- (b) Je, Serikali imejiwekea lengo kwamba ni lini italimaliza tatizo la upungufu wa watumishi hao nchini?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo nchini. Wakati tuna Mahakama za Mwanzo 1,105 kuna Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 666 tu. Hivyo, upo upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 439.

Serikali imepanga mikakati ifuatayo ili kusaidia kupunguza upungufu huu:-

1. Kuajiri Watanzania wenyе sifa za Uhakimu wa Mahakama za Mwanzo waliohitimu kwenye vyuo vinavyotambulika na Serikali. Kwa mwaka huu wa Fedha 2004/2005, Serikali imetoa nafasi za ajira mpya 55 kwa ajili ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na taratibu za ajira zinaendelea kufanyika.
2. Kwa kuitia mpango maalum, kufanya upanuzi wa Chuo cha Uongozi cha Mahakama Lushoto, ili kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 badala ya 150 wa sasa.
3. Kutoa ajira ya Mkataba kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wastaifu wenyе sifa nzuri za maadili na utendaji.

Mheshimiwa Spika, napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa kwa kuzingatia hali halisi ya upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo uliopo, Wilaya ya Kondoa kwa ujumla ina unafuu kiasi ikilinganishwa na Wilaya nyingine hapa nchini kwa kuwa ina Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 7 kwa Mahakama za Mwanzo 15 zilizopo Wilayani humo. Hata hivyo, Wilaya hii ya Kondoa nayo itafikiriwa mara taratibu za ajira mpya zitakapokamilika.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri nina maswali mawili tu ya nyongeza. Kwa kuwa hao Mahakimu walioko sasa hivi katika Mahakama za Mwanzo wanazimika kusafiri pia kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo ambazo hazina Mahakimu kuhukumu kesi na kwa kuwa hawana usafiri wa uhakika mpaka kwenye Mahakama hizo nyingine. Je, Wizara ina mpango gani kwa kuwasaidia usafiri wa kufika kwenye Mahakama ambazo hazina Mahakimu? (*Makofit*)

Swali la pili, kwa kuwa Mahakimu hawa wanapokwenda wanakaa siku kadhaa katika Mahakama hizo na wanastahili kulipwa posho ya kujikimu na kwa kuwa kwa muda mrefu hawajalipwa. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwalipa posho ya uhakika ili waweze kufanya kazi hizo?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la usafiri wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hili limekuwa ni tatizo sugu tumekuwa nalo kwa muda mrefu. Lakini mategemeo yangu kwamba katika Awamu ya Nne Serikali husika itaweza kulififikiria hili kwa makini zaidi na hasa ikizingatia kwamba sasa hivi tuna *Legal Reform Programme* ambayo hivi majuzi nilii-lounge hiyo programu yenye na katika programu hiyo ni pamoja na kutatua haya matatizo ya usafiri. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba katika kipindi cha 2006/2007 tatizo hili litakuwa limetafutiwa suluhi.

Kuhusu masuala ya posho taratibu ni kwamba Mahakimu hawa wana usafiri kwenda kwenye Mahakama nyingine na wanakaa huko, basi wanalipwa hizo posho. Sasa kama kuna tatizo katika Jimbo la Mheshimiwa Degera, basi anipatie hiyo taarifa ili niweze kulishughulikia suala hilo.

MHE. WILLIAM J. KUSILA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hilo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni kwa nchi nzima siyo kwa Mheshimiwa Degera tu na kwa Kusila pia. Kwa kuwa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilikuwa kitivo cha kwanza kuanzishwa hapa nchini mwaka 65 pale Lumumba na mpaka leo bado kipo kinaendelea kutoa wahitimu wa Stashahada na Shahada katika Sheria. Hivi wahitimu hao wote wanakwenda wapi? Kwa nini mpaka leo bado tuna tatizo hili kubwa katika nchi?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Kusila kama ifuatavyo:-

Ni kweli kitivo hiki tumekuwa nacho kwa muda mrefu na sasa hivi tuna vyuo vingi ambavyo vinatoa wahitimu hawa wa upande wa Sheria. Tumaini moja wapo ni Mzumbe na mahali pengine, hawa wanasheria wapo lakini mpaka sasa hivi tatizo limekuwa katika kuwapa mafunzo ya kimaadili, maadili ya uhakimu. Sasa Chuo chetu cha Lushoto ni kidogo hakiwezi kuwachukua wote hawa na kuwapa mafunzo hayo. Kwa hiyo nasema kwamba kwa jinsi tunavyopanua vyuo vyetu na tutakavyokuwa na utaratibu wa kukifanya chuo hiki cha Lushoto kuwa kikubwa zaidi, basi tunaweza tukawachukua hawa mawakili. Kufuzu tu Sheria hakumainishi kwamba utaajiriwa kuwa hakimu. Ni lazima pia ujifundishe *Judicial Ethics* ambazo zinaambatana na uhakimu.

Na. 104

**Kiwango cha Utozaji wa Kodi ya Ongezeko
la Thamani (VAT)**

MHE. AGGREY D. J. MWANRI (K.n.y MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) aliuliza:-

Kwa kuwa maelezo ya ziada yaliyotolewa toka Hazina kwa swali langu Na. 52 lililojibiwa Bungeni tarehe 16.6.2004 kuhusu sababu za kutopunguza kiwango cha kutoza kodi ya *VAT* hayakuwa hasa ya utafiti wa kina kulingana na wenyewe vielelezo vya waliohojiwa na majibu ya wahojiwa na wadau wengine bali ni maelezo na mapendekezo binafsi tu na kwa kuwa hata kwenye maelezo hayo Serikali ilikiri kwamba, kiwango cha kutoza *VAT* kikipunguzwa kutoka asilimia 18, na *compliance* ya walipa kodi ikapanda toka asimia 65 ya sasa hadi asilimia 75, Serikali itakusanya shilingi bilioni 610 kwa mwaka ikilinganishwa na shilingi bilioni 589 zinazokusanywa sasa:-

Je, kwa nini Serikali inadhani kuwa *compliance* ya asilimia 75 au zaidi haiwezi kufikiwa na walipa kodi kama kiwango cha *VAT* kitapunguzwa na usimamizi wa *TRA* katika ukusanyaji wa kodi hiyo kuimarishwa zaidi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwanza kabisa naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba maelezo ya ziada niliyotoa Bungeni tarehe 16/6/2001 kwa swali Na. 52 kuhusu sababu za kutopunguza kiwango cha kutoza kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) cha asilimia 20 yalikuwa yamefanyiwa utafiti wa kina na kwamba hayakuwa maelezo ya mapendekezo ya mtu binafsi. Napenda pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba utafiti uliofanywa ulizingatia pia njia ya kupunguza kiwango cha *VAT* kwa kutumia *sensitivity analysis* yaani uchambuzi ambao huainisha viwango mbalimbali vya kodi ya *VAT Tax rates* pia makusanyo ya kodi pamoja na ridhaa ya kulipa kodi yaani *VAT compliance* ambavyo kwa pamoja huainisha kiwango cha mapato ya kodi kitakachokusanywa na kitakachopotea ikiwa kiwango cha kodi kitapunguzwa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi yaani *VAT compliance katika* mfumo wa utoaji wa kodi wa namna hii kilitegemewa kuwa cha juu sana hata kufikia asilimia 100. Lakini kwa sababu mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata kiutendaji hakuna nchi yoyote duniani iliyofikia kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi cha asilimia 100 zikiwemo nchi zinazotoza *VAT* chini ya kiwango cha asilimia 20. Kwa mfano, wakati kiwango cha *VAT* Kenya kilipokuwa asilimia 18 mwaka 2002, kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi kilikuwa ni asilimia 56. Pia Madagascar inayotoza *VAT* kiwango cha asilimia 15, kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi ni asilimia 67, ikilinganishwa na sisi ambapo tumefikia kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi cha asimia 65 pamoja na kuwa tunatoza *VAT* kiwango cha asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ridhaa ya kulipa kodi haitegemei kiwango cha kodi peke yake, bali hutegemea pia mambo mengine kama vile kuwepo misingi madhubuti ya usimamiaji kodi, kuwepo kwa sheria inayowezesha ukusanyaji kuwa rahisi na taratibu zinazompunguzia mlipa kodi gharama za ridhaa ya kulipa kodi (*compliance costs*).

Mheshimiwa Spika, mfumo wa *VAT* hapa Tanzania una misamaha mingi inayotolewa kwa manufaa ya jamii yote ya Watanzania. Mlaji anayelengwa

kupunguziwa kiwango cha kodi kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge, tayari ananufaika kwa njia moja au nyingine na misamaha inayotolewa chini ya sheria ya kodi hii. Bidhaa muhimu kama vile nafaka au unga, mchele, mboga na nyama isiyosindikwa na huduma za elimu na matibabu havitozwi *VAT*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi zinapanda zaidi ya kiwango cha sasa cha asilimia 65 kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 Serikali imebuni mikakati mbalimbali ikiwemo ya upandishaji wa kiwango cha usajili wa *VAT* (*VAT threshold*) kutoka shilingi 20 milioni hadi shilingi 40 milioni kwa mwaka na kuboresha mfumo wa utendaji ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haidhani kuwa kiwango cha ridhaa ya kulipa kodi cha asilimia 75 hakiwezi kufikiwa kama kiwango cha *VAT* kitapunguzwa na usimamizi wa *TRA* katika ukusanyaji wa kodi hiyo kuimarishwa zaidi. Kwa maneno mengine ni kwamba hili linawezekana. Hata hivyo, kinachosisitizwa ni kwamba mafanikio haya yanahitaji muda mzuri wa kutekeleza mikakati ya ukusanyaji na ari ya hali ya juu ya walipa kodi.

Ili kuweza kuwa na mafanikio mazuri zaidi, ushushaji wa kiwango cha *VAT* inabidi uende sambamba na uondoaji wa misamaha mingi iliyopo ili kuweza kupanua wigo wa kodi hiyo. Kwa sababu hizi, Serikali bado inafanya tathmini ya kina ili kuangalia uwezekano wa kupunguza kiwango cha *VAT* bila ya kuathiri mapato ya Serikali ambayo yanahitajika sana ili kutoa huduma muhimu kwa wananchi wake.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swalii la nyongeza. Namshukuru sana kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoo.

Kwa kuwa kupanda kwa *VAT* ni sehemu ya zile *overhead expenditure* na kwa kuwa sasa hivi tumeingia katika jumuiya ya Afrika Mashariki, ambapo kama alivyogusia hapa, Kenya wenzetu wapo kwenye asilimia 18 na Uganda ni hivyo hivyo najua imepanda kidogo, na tunaingia katika hali ya ushindani na bidhaa zetu zitakuwa juu kwa sababu *VAT* iko juu.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya ku-*harmonize* katika suala hili la *VAT* walau tuwe na kiwango kimoja?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, kweli *VAT* ni *overhead costs* lakini wakati sisi *VAT* iko juu wenzetu Afrika Mashariki *rate* zao nyingine za ushuru ni kubwa zaidi kuliko za kwetu, na hata wao vilevile wako katika fikra ya kuweza kuziongeza sio ku-*harmonize* kwetu sisi

kwamba tulete chini lakini na wao vilevile wako katika *harmonize* kuleta juu ili wapate *compliance* kubwa vilevile. Kwa hivyo si lazima kwamba tukipunguza sisi kwenda chini na wakati tunaona mapato yetu maduhuli yetu yatakuwa kidogo sana, yataathirika sana hata kwa *two percent* unaweza kupoteza kiasi cha bilioni 65. Ambacho hatuwezi kwa sasa hivi kupoteza kiasi kama hicho, kama nilivyosema kuna misamaha mingi zaidi na kuna mambo mengi zaidi lazima tuliangalie na tumefanya *sensitive analysis* kwa kina kuona namna gani *VAT* ikipunguzwa hata kwa *percentage* moja inaweza kutuaathiri mapato yetu.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, swali langu hasa lilikuwa ambalo liloulizwa na Mheshimiwa Mwanri. Lakini bora niongeze tu kwa kuwa Waziri amesema Serikali ilikuwa inajaribu kutafakari namna ya kupungua, hivi inachukua muda gani na hiyo *harmonization* ya Kenya na Uganda wamemnong'onezea lini?

SPIKA: Hakusikia vizuri swali lako, hakulipata vizuri, hebu rudia Mheshimiwa Janguo.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Waziri alisema kwamba hata hivyo Serikali inafikiria uwezekano wa kuweza kuupunguza, nasema inachukua muda gani kufikiria ili waweze kupunguza. Lakini alipojibu hili swali amesema kwamba Kenya na Uganda wanataka *ku-harmonize* kwa maana ya kupandisha, wamemnong'onezea siku gani kwamba watafanya hivyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kuna mikutano mbalimbali wanakutana Mawaziri wa Fedha wa Afrika Mashariki na jana vilevile walikuwa na kikao kuangalia mambo mbalimbali yanayohusu maslahi yetu ya *customs Union* ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo siwezi kukwambia tarehe fulani, lakini takwambia kwamba wanakutana Mawaziri wa Fedha na jana Mawaziri Fedha wako huko Arusha wanakutana.

Na. 105

Mifuko ya Udhagini wa Mikopo

MHE. JOB YUSTINO NDUGAI (K.n.y. MHE. MARGARETH AGNESS MKANGA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha mifuko ya udhamini wa mikopo kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuhimili ushindani wa kibashara;

Je, ni wafanyabiashara wangapi na vyama vyaya ushirika vingapi vimenufaika na dhamana hizo tangu zilipoanzishwa mpaka leo ambapo swali hili linapojibiwa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalí la Mheshimiwa Magreth Mkanga Mbunge Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo ya utangulizi:-

Mheshimiwa Spika, mfuko wa udhamini wa mikopo kwa ajili ya mauzo nje ya nchi ulianza kutumika Julai, 2002 kwa kutoa udhamini kwa mikopo inayotolewa na mabenki kwa wauzaji wa bidhaa za nje yaani *Exporters*. Katika kuanzisha mfuko huo Serikali ilichangia shilingi bilioni 5.0 na Benki Kuu ya Tanzania ilichangia shilingi bilioni 1.5 na kufanya mfuko huu kwa kipindi cha mwaka 2002/2003 kuwa na mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 6.5.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali ilitenga shilingi bilioni 13.0 kwa ajili ya kuboresha mfuko huo. Hadi mwaka huu wa 2004/2005 mtaji umekua na kufikia shilingi bilioni 21.144 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 1.644 zilizotokana na riba na ada ya udhamini. Hadi sasa gharama za uendeshaji wa mfuko zinalipwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swalí la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2002/2003 hadi mwaka 2004/2005 mfuko ultoa dhamana kama ifuatavyo:-

(i) Katika mwaka 2002/2003, Dhamana ya jumla ya shilingi bilioni 6.73 kwa Vyama 17 vya Ushirika vinavyoshughulika na ununuzi wa kahawa, pamba na korosho na kiwanda cha nguo cha *Star Apparel*.

(ii) Katika mwaka 2003/2004, Dhamana ya jumla ya shilingi bilioni 7.5 kwa Bodi ya Pareto, mashamba mawili (2) ya Maua na Vyama 19 vya Ushirika vinavyoshughulika na ununuzi wa kahawa, pamba na korosho.

(iii) Mwaka 2004/2005, Dhamana ya jumla ya shilingi 18.85 bilioni kwa kiwanda cha Maturubai – Morogoro *Canvas Mill*, Shamba la Mifugo Sumbawanga – *Agricultural Animal Foods Industries Limited*, Vyama 9 vidogo vya Ushirika vinavyoshughulika na uuzaji wa tumbaku, kampuni moja ya kununua korosho –*Bucco Investment Holdings Limited* na Shamba la Maua – *Tengeru Flowers Company*.

MHE. JOB YUSTINO NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swalí la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Mkanga na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Slpika, kwa kuwa katika majibu haya inaonyesha wazi kwamba ni *exporters* wachache sana ambao wamefaidika na kuwepo kwa mfuko huu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa *speed* hii ndogo ya kutoa

udhamini wa mikopo ni kwamba haiendani na mategemeo na matarajio ya mkakati wetu wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, labda pengine wafanyabiashara au wakulima au wanaushirika wengi hawana habari ya fursa hii, fedha zipo na nawaomba wananchi pamoja na nyie Waheshimiwa Wabunge ambaao ni wafanyabishara, mtumie fursa hii fedha zipo ni kuzitumia tuondoshe umaskini.

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na mimi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri hao ambaao walifaidika na huo mfuko wa udhamini walikuwa wanabadilika kila mara Wizara ya fedha na kwa Serikali kwa ujumla haioni kwamba utaratibu kama huo hauridhishi kwa wajasilia mali wetu wa Tanzania na kwamba kuna haja ya kufikiria mkakati mzuri zaidi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, bidhaa tunapoendelea na mara nyingine zinakuja, hivi sasa Serikali imeliona hilo na imekusudia kuleta dhamana za aina mbili pia.

Dhamana ya mikopo ya miradi midogo na ya kati SME sasa hii inaitwa *SMG*, *CGS* na dhamana ya mikopo ya miradi mikubwa ya maendeleo na mauzo nchi za nje, ambayo tunategemea baada ya si muda mrefu itakuwa inafanya kazi na itasaidia zaidi wale wote ambaao watahitaji dhamana wakulima wadogo wadogo wakitangulia pamoja na wafanyakazi wadogo wadogo na wa kati na wale wakubwa pia ambaao watasafirisha nje. (*Makofi*)

Yote hii miwili inapata msaada *World Bank* pamoja na Benki Kuu kwa ushirikiano Vyuo Vikuu na vilevile *IMF* pia itajiunga katika kudhamini mfuko huu.

Kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba baada ya muda si mrefu mifuko hii itakapoanza kufanya kazi, wananchi wataitumia vivilyo kwa maendeleo yao.

Na. 106

**Ajali za Magari ya *Trailer* Katika Mzunguko wa Barabara ya
Dodoma Eneo la Shabiby**

MHE. WILLIAM J. KUSILLA (K.n.y. MHE. MARIAM S. MFAKI aliliuza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ajali nyingi za magari makubwa yenye *trailer* kuanguka katika mzunguko wa barabara ulioko karibu na Kituo cha mafuta Shabiby, Dodoma:-

(a) Je, ni magari mangapi yaliyoanguka katika mitaro iliyopita katika eneo hilo hadi sasa?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha magari hayo kuanguka na Serikali inachukua hatua gani kurekebisha kasoro hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumewahi kutokea ajali za magari makubwa yenye *trailer* kuanguka katika mzunguko wa barabara ulioko eneo la Shabiby Mjini Dodoma. Kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba zimetokea ajali tatu za magari hayo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu mbili za msingi zinazosababisha ajali hizo ya kwanza ni uzembe wa madereva wanaoendesha magari kwa mwendo wa kasi wanapoingia katika mzunguko huo bila ya kuzingatia alama inayoonyesha kuwapo kwa mzunguko wa barabara eneo hilo na kuwataka wapunguze mwendo. Pili eneo la mzunguko upande wa kushoto kama unatokea Dodoma barabara ni nyembamba, ukilinganisha na ule wa upande wa kulia. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inashughulikia kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili ikiwa pamoja na uwezekano wa kuweka matuta yaani *bumps* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa mara nyingine kwa madereva kwamba wawe makini katika kuzingatia alama za barabarani ili kuepuka ajali zinazotokana na uzembe.

MHE. WILLIAM J. KUSILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba alama zilizowekwa kuonyesha mzunguko huu hazionekani vizuri na kwa hiyo kuna haja kuweka alama ambazo zinaonekana wazi wazi hasa wakati wa usiku.

Pili Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa sababu za kitaalam za kuwa na mzunguko hasa ikizingatiwa kwamba hakuna barabara nyingi. Mzunguko ule pale ni wanini hasa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nakubaliana naye kwamba alama ambazo zimezekwa barabarani zimezibwa na mabango mengi na hilo tumelitambua tunatafuta alama ambazo zitakuwa zina meremeta usiku na mchana kuonekana vema. Mzungukoko ulioko pale kwa sababu gani, na mzunguko ule hauna barabara nyingi, ungeweza kabisa kubomolewa, lakini

katika mpango mkubwa wa Jiji la Dodoma pale ndipo mwisho wa barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam, ukishapita pale unaingia katika mamlakanyingine mbili za Dodoma ambazo ni *CDA* na Manispaa ya Dodoma.

Lakini vile vile tunategemea kutengeneza barabara ya kuambaa uwanja wa ndege ili malori makubwa yasipite mjini, ndio maana umeona mzungukuo ule uko pale.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo sana. Kwa kuwa sasa hivi Dodoma ina magari mengi ya mizigo, na magari mengi hayo upakia mizigo mikubwa sana wakati mwengine mipana sana kuzidi hata ile kile kiwango cha bodi ya gari lenyewe.

Je, Serikali ina utaratibu wa kudhibiti upakiaji huo mbaya wa mizigo ambaa unawaweza kusababisha ajali mbaya barabarani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupakia mizigo barabarani unafahamika na haya malori mnayoyaona makubwa yamepakia mizigo unasema ni mikubwa sana kwa kawaida ipo kwenye kiwango kinachotakiwa upana huo wa mizigo, lakini sasa hivi Dodoma ni Bandari ya nchi kavu. Kwa sababu ni Bandari ya nchi kavu hapa, utaona malori makubwa mengi sana yanakuja wanatumia barabara hii badala ya kutumia reli, na ni uzoefu tu kwamba hatukuzoea kuyaona malori makubwa mengi yanapita kwenye barabara hiyo. Lakini mara *train* itakapokamilika mizunguko hiyo ya malori ya mizigo hapa Dodoma utakwisha na jinsi tunavyopanua barabara hii tunavyoongeza upana wa barabara hii ya Morogoro Dodoma utaona kwamba ule upana na ukubwa wa mizigo utakuwa ni sahihi tu kwa matumizi ya barabara hii. Vile vile ningeomba tu watu wa Dodoma wazoe sasa kwamba malori makubwa yatakuwa mengi na yanapita mpaka Manyoni na Singida. Kwa hiyo, ni suala la kuzoea malori hayo. (*Makofii*)

SPIKA: Ninao ujumbe toka kwa Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kwamba anaomba swali lake namba 107 lilonolewe. Kwa hiyo, + limeondolewa tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Mawasiliano

Na. 107

Amani ya Nchi

Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na muulizaji.

Na. 108

Mhimili wa Mtandao wa Mawasiliano Nchini

MHE. WILFRED M LWAKATARE (k.n.y MHE. HAMAD RASHID MOHAMED) aliuliza:-

Kwa kuwa kuna umuhimu wa kuanza na muhimili katika mtandoa wa mawasiliano nchini:-

- (a) Je, ni njia gani zimeshatandikwa za *Fibre optic* kukidhi haja hiyo;
- (b) Je, ni mashirika mangapi na ni yapi yanayotekeleza mradi huo, na ni fedha kiasi gani zimetumika kwa mradi huo na ni ngapi kati ya hizo ni msaada, mkopo au zimetolewa na shirika lenyewe;
- (c) Je, ni mradi huo unategemewa kukamilika baada ya muda gani.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, jumla ya njia zenyet urefu wa kilomita 476 zimetandikwa ardhini na Shirika la Reli Tanzania na *TTCL*, reli zikiwa kilomita 457 na *TTCL* kilomita 19. *TANESCO* wanaendelea kutandika kilomita 2000, *SONGAS* kilomita 300, *TAZARA* njia 12 na tunategemea *TRC* inaendelea kutandika njia nyingine zenyet urefu wa kilomita 380

(b) Mashirika yaliyojitekeza mradi huo ni sita nayo ni *TTCL*, *TRC*, *TAZARA*, *TANESCO*, *SONGAS* na *ITN*. Fedha zilizotumika ni kama ifuatavyo;

TTCL ni Dola za Kimarekani 170,558, *TRC* jumla ya shilingi bilioni 41.14, msaada ikiwa ni shilingi 26.8 bilioni na mchango wa *TRC* bilioni 14.26. *TAZARA*, *TANESCO* na *SONGAS* miradi yao iliunganishwa na miradi yao iliunganishwa na miradi mama na mradi wa *optic fibre* na baadhi ya miradi hiyo bado inaendelea.

ITN ni mtandoa wa jeshi ambaa unatarajiwa kuwaunganisha na ile mingine ili isaidiane kufanikisha juhudii za kujenga na kuimarisha Serikali *Electronic that* maana ya hii *Government*.

(c)Mheshimiwa Spika, maendeleo ya teknolojia yameleta mabadiliko makubwa katika sekta ya mawasiliano na hivyo kuendelea kurahisisha utoaji wa huduma zinazohusika. Pamoja na jitihada na juhudii za mashirika na Taasisi nilizozitaja hapo awali katika kuboresha miundo mbinu na mwasiliano katika Taasisi zao Wizara iliona

umuhimu wa kuunganisha juhudhi hizo ili Mashirika hayo mbalimbali na nia ya kuanzisha mradi wa Taifa wa ujenzi wa uti wa mgongo wa miundo mbinu wa mawasiliano nchini.

Hivyo Serikali iliwaomba washauri toka China na kampuni ya *Wordtel* yenyewe ushirikiano na *ITU* kutupatia msaada wa wataalam wahandisi kwa lengo la kufanya utafiti wa awali kwa ajili ya kutoa mapendekezo kwa Serikali ya Tanzania, juu ya kujenga mtandao huo.

Wataalam hao tayari wamemaliza kazi hiyo na hivi karibuni wamewasilisha ripoti yao Serikalini. Tunategemea uchambuzi wa ripoti hii na nyingine ya wataalam wetu wa nchi waliopewa jukumu la kuandaa muundo wa Taasisi ya kuratibu mtandao huo zitakapojadiliwa na kutolewa mapendekezo ndivyo tutakavyopata Mwaga na kujua mradi tunaotegemea utaanza lini na kukamilika lini.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa *TTCL* walipata upendeleo na fursa ya kufanya biashara peke yake kwa muda wa miaka mitano na mkatuba ulikuwa unazungumza kwamba wangeweza kuweka njia za simu zaidi ya 800,000 kwa nchi zima.

(a) Je, Serikali inatamka nini kuhusu suala hilo na je watailipa Serikali na Taifa fidia ya kutofanya hivyo?

(b) Na kama hawatalipa fidia hiyo nani analibeba suala hilo ili Watanzania waweze kumjua waje wamhukumu wakati wa kupiga kura. (*Makofit*)

NAIBU WA WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kama atakumbuka Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ni kwamba *TTCL* ni kweli ilipewa *school civity* ya miaka minne uiondolee huduma ya *basic* na mambo mengine.

Lakini siyo *line* 800. Kulikuwa kutolewe huduma za *Mobile* na huduma za teknolojia ya sasa ambayo ipo, nataka nikiri kwamba kwa upande huduma za mawasiliano ya *Mobile* zimepita kiwango kile ambacho kimewekwa na nitakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba zimefikia katika maeneo mengi tu.

Lakini tulipoweka mikataba hii na kuingiliana na Mikataba mingine ni kwamba panafanywa huduma hizi kufuatana na taratibu zilizokubaliana. Napenda nikiri kwamba hatukufikia kiwango tulichofikia, lakini tumefikia muafaka katika mambo mengi tu ya huduma za mawasiliano nchini.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, sasa matangazo ya vikao. Kuna Kamati moja ya Bunge imepangiwa kufanya kikao leo nayo ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo

kuwa leo tarehe 21 Juni kutafanyika vikao saa 9 mchana, chumba Na. 428 jengo la utawala.

Halafu kuna vikao vya vikundi vya Wabunge, vikundi vya hiari vya Wabunge vifuatavyo, Umoja wa Wabunge Wanawake (*TWPG*) Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Makinda anawatangazia Wajumbe wa Umoja huo kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 21 saa 7 mchana, chumba Na. 231.

Umoja wa Wabunge wa Kupambana na *UKIMWI (TAPAC)*, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anawatangazia Wajumbe wa kikao cha Kamati ya Utendaji sio wote, Kamati ya Utendaji ya Umoja huo kwamba mchana leo kutakuwa na kikao mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana katika Ofisi ya *TAPAC*.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho ni kikundi cha Amani *Forum* Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Ibrahim Marwa anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Amani *Forum* kwamba leo saa 7 mchana kutakuwa na kikao ukumbi Na. 227. Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*. (*Makofit*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua Makadirio ya matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2005/2006. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudini kubwa za kufufua uchumi wa nchi, kujenga demokrasia na kudumisha amani na Umoja wa Kitaifa. Juhudi hizo zimevezesha Taifa letu kuongeza uwezo wa kutoa huduma kama vile ujenzi wa barabara, madarasa, zahanati na nyumba za watumishi. Aidha, amerejesha imani kwa Wahisani, hivyo kuwavutia kuendelea kutoa misaada na kufuta baadhi ya madeni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, chini ya uongozi wake bora, Vyama vya Siasa katika kipindi chake vimepewa uhuru zaidi wa kushiriki masuala ya siasa. Ninampongeza kwa kuweka mazingira mazuri ya ushindani katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2005, jambo ambalo litaifanya nchi yetu iendelee kuwa ya amani na utulivu. Kutokana na hali ya utulivu iliyopo, Tanzania imekuwa daima mstari wa mbele na

kiongozi wa kusuluhisha migogoro ya nchi za Maziwa Makuu na katika kuanzisha ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2005. Naomba vilevile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuwa mgombea mwenza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwake kuwa mgombea wa nafasi ya Urais katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa salam za rambirambi kwa ndugu wa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine waliofariki dunia wakati na baada ya Bunge la Bajeti la mwaka 2004/2005. Waheshimiwa Wabunge na Viongozi hao ni Hayati Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Kapteni Theodosus James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Waziri katika Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Hayati Abu Towagale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Hayati Paulo Bomani aliyekuwa Muasisi wa CCM na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mtumishi wa siku nydingi wa Serikali. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa Hotuba yake iliyotoa mwelekeo na majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itatekeleza maagizo yaliyomo katika Hotuba yake inayozingatia malengo na mikakati tuliyojiwekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000 - 2025. Aidha, naomba niwashukuru na kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Pesambilii Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa Hotuba zao nzuri zinazofanua hali ya uchumi wa nchi na kufanya mapitio ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu (1995-2005). Pia kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 na kuelezea matarajio ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchambua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Maoni na ushauri wa Kamati utazingatiwa wakati wa kutekeleza majukumu na malengo yaliyowekwa katika maeneo yote kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tat, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeshuhudia mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake ya msingi na ya kisera kwa maeneo mbalimbali inayoyasimamia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Tat, Serikali imefanikiwa kuanzisha maeneo mapya ya utawala katika ngazi mbalimbali. Idadi ya Mikoa imeongezeka kutoka 20 mwaka 1995 hadi Mikoa 21 mwaka 2005 ambapo Mkoa wa Manyara ulianzishwa; Wilaya zimeongezeka kutoka 99 mwaka 1995 hadi 106 mwaka 2005 ikiwa ni ongezeko la Wilaya 7. Wilaya hizo ni Mvomero, Namtumbo, Ilemela, Kishapu, Kilolo, Kilindi na Uyui. Aidha, Tarafa mpya nane zimeanzishwa na kuongeza idadi ya Tarafa kutoka 508 hadi 516, Kata mpya 17 zimeanzishwa na kuongeza idadi ya Kata kutoka 2,536 hadi 2,553 na Vijiji vilivyosajiliwa hadi sasa ni 9,822. Idadi hii ya vijiji inazingatia kufutwa kwa baadhi ya vijiji kufuatia uanzishwaji wa Mamlaka za Miji Midogo na baadhi ya Halmashauri za Miji.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa mamlaka za Halmashauri, ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wananchi, mwezi Juni 1996 Serikali ilivunja iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kuunda Tume ya Jiji na hatimaye kuundwa kwa Manispaa za Ilala, Kinondoni, Temeke na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mwaka 1999. Vilevile, mwaka 2000 Serikali ilianzisha rasmi Halmashauri za Wilaya za Ruangwa, Tandahimba, Kongwa, Mkuranga, Karatu, Sikunge, Missungwi, Bukombe, Mbarali, Manispaa ya Shinyanga na Jiji la Mwanza. Mwaka 2004, Miji midogo 90 ilianzishwa pamoja na Halmashauri za Miji ya Kibaha, Korogwe na Babati. Aidha, mwezi Julai 2005 Serikali itaanzisha Halmashauri tano katika Wilaya za Namtumbo, Kilolo, Mvomero, Kilindi na Kishapu. Vilevile, Halmashauri ya Mji mmoja wa Mpanda, Manispaa nane za Mtwar/Mikindani, Songea, Sumbawanga, Kigoma/Ujiji, Bukoba, Musoma, Singida na Arumeru na Halmashauri za Jiji hapa naomba nifanye sahihisho Halmashauri za Jiji la Arusha, Mbeya na katika hotuba yangu inayogawanywa pale ibara ya kumi ongeza Jiji la Tanga zitaanzishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Viongozi na Watendaji wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kutekeleza jukumu la kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa, Ofisi yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa Viongozi na Watendaji mbalimbali kwa lengo la kujenga mazingira bora ya kitaalam katika Sekta ya Umma kama ifuatavyo:-

- (i) Kuhusu muundo mpya wa utendaji kazi katika Tawala za Mikoa, yametolewa mafunzo kwa Viongozi na Watendaji Wakuu katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri katika Mikoa yote wapatao 3,076;
- (ii) Kuhusu teknolojia ya mawasiliano na Uongozi katika Sekta ya Umma, yametolewa mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa wote 21 ambao pia walipata mafunzo ya ziada ya Utawala nchini Ireland, wengine waliopata mafunzo hayo ni Wakuu wa Wilaya 15, Viongozi na Maafisa Wandamizi 114;

- (iii) Mafunzo ya teknolojia na mawasiliano katika ukusanyaji na utunzaji wa takwimu yametolewa kwa Maafisa Mipango wote wa Mikoa 21 na Maafisa Elimu 2 kila Mkoa;
- (iv) Mafunzo ya kutumia mfumo wa mawasiliano yametolewa kwa watumishi 155;
- (v) Mafunzo ya upangaji wa mipango shirikishi jamii katika muundo mpya wa utendaji kazi katika Tawala za Mikoa yameendeshwa katika Halmashauri 60 na kuhudhuriwa na washiriki 1,610 wa ngazi ya Wilaya na Kata;
- (vi) Mafunzo ya Utawala Bora yametolewa kwa Makatibu Tarafa katika Mikoa 19 na Makatibu Tawala wa Wilaya 105;
- (vii) Mafunzo kuhusu uboreshaji wa ujuzi na stadi za kazi yametolewa kwa Wakuu wa Wilaya wote 106;
- (viii) Mafunzo ya kuboresha ujuzi na stadi za kazi yametolewa kwa Madiwani 3,447;
- (ix) Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa, Vitongoji, Kamati tano za Kila Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya kila Mtaa wapatao 76,000 walipata mafunzo kuhusu ujuzi na stadi za kazi;
- (x) Ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi kwa kuhusisha Viongozi na Watendaji Wakuu zimefanyika kwa ajili ya kubadilishana uzoefu. Katika programu ya ziara ya mafunzo nchini Japan, mafunzo yalitolewa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa 12 ya Dodoma, Morogoro, Mbeya, Tanga, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Arusha, Singida, Shinyanga, Kagera na Iringa. Vilevile mafunzo yalitolewa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri 24 kutoka Mikoa hiyo, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 4 na Afisa Mtendaji wa Kata 1; na
- (xi) Elimu iliyopatikana kutokana na ziara nchini Japan imetolewa kwa watendaji wapatao 1,300 kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri katika Mikoa hiyo 12.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Vyombo vya Usafiri, mwaka 1999 Serikali ilifanikiwa kununua magari 99 kwa ajili ya usafiri wa Wakuu wa Wilaya wote nchini. Vilevile, mwaka 2000/2001 Serikali ilinunua pikipiki 512 kwa ajili ya kutatua tatizo la usafiri kwa Makatibu Tarafa wote nchini. Aidha, malori 96 ya Halmashauri yalinunuliwa kwa awamu kati ya mwaka 1996 na mwaka 2001 kwa ajili ya kazi za barabara. Kupatikana kwa vyombo hivyo vya usafiri vyenye uhakika kumeweza kuhusu juhudini za Serikali kuwafikia wananchi na kufanikisha shughuli za maendeleo kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika kipindi cha Awamu ya Tat, Serikali imewezesha kufanyika chaguzi mbili kwa Viongozi wa Serikali za Mitaa ngazi za Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Chaguzi hizi zilifanyika mwaka 1999 ambapo Vyama vya Siasa 13 vilishiriki na mwaka 2004 Vyama vya Siasa 16 vilishiriki kati ya 18 vilivyoandikishwa. Kanuni za Uchaguzi ziliandaliwa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali vikiwemo Vyama vya Siasa vilivyopata usajili wa kudumu. Aidha, kwa jumla chaguzi zilifanyika katika mazingira ya uhuru na amani. Katika chaguzi zote CCM ilishinda.

Mheshimiwa Spika, Ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa, katika kuimarisha Utawala Bora, Serikali imekubali kuwaajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa kote nchini. Maafisa Watendaji wa Vijiji 7,770 tayari wameajiriwa hadi kufikia mwezi Mei 2005 na mishahara ya Maafisa Watendaji hawa imeanza kulipwa na Serikali Kuu kwa awamu mbili kutegemea tarehe ya ajira tangu mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Migogoro ya Mipaka, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaendelea kushughulikia migogoro ya mipaka Kimkoo na Kiwilaya. Migogoro iliyoshughulikiwa ni kati ya Wilaya za Kiteto na Kondo na Mbarali na Iringa. Migogoro ya maeneo yaliyobaki itaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya Rushwa, elimu imeendelea kutolewa kwa watumishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu maeneo mbalimbali ya rushwa. Maeneo haya ni pamoja na utoaji wa zabuni, viwanja, ajira za watumishi na huduma mbalimbali na vilevile katika kuingia mikataba ya kisheria. Kutokana na elimu hiyo, vitendo vya rushwa katika sehemu za kazi vimeitungua. Aidha, Mwongozo wa kuandaa mkakati wa kupambana na vitendo vya rushwa umeandaliwa na kupelekwa katika Halmashauri zote na Halmashauri hizo zimewasilisha Bajeti zao na utekelezaji utaanza mwezi Julai 2005.

Mheshimiwa Spika, Uboreshaji wa miundo mbinu mijini, kupitia Mradi wa Uimarishaji Huduma Mijini, miundombinu imeboreshwa kwa kufanyiwa ukarabati na upanuzi ikiwa ni pamoja na Barabara, Vituo vya mabasi, mifereji ya maji ya mvua na maeneo ya kutupa takataka katika Manispaa za Arusha, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Tabora, Tanga na Jiji la Dar es Salaam na Mwanza. Jumla ya kilometra 134.95 kati ya lengo la kujenga kilomita 82 za barabara sawa na asilimia 164.6 zimeimarishwa kwa kiwango cha lami na vituo 12 vya mabasi vimejengwa kati ya vituo 6 vilivyopangwa sawa na asilimia 200.

Uboreshaji huu umewezesha kuinua mapato katika Miji husika, kuboresha hali ya usafi wa mazingira ya miji, kuinua kipato cha wananchi na hivyo kupunguza hali ya umaskini. Hata hivyo mradi huu umemalizika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Barabara Vijijini, kutokana na ruzuku ya Mfuko wa Barabara, Halmashauri zimeweza kufanya matengenezo makubwa ya barabara za vijijini kwa viwango mbalimbali vya matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*), sehemu korofii (*Spot Improvements*), matengenezo ya kawaida (*Routine Maintenance*) na

kujenga makalvati na madaraja. Aidha, barabara zilizofanyiwa matengenezo zimeongezeka kutoka kilomita zaidi ya 7,000 mwaka 1998/1999 na kufikia kilomita 13,868 mwaka 2004/2005. Hii ni sawa na ongezeko la kilomita 6,868 ya malengo. Hata hivyo Mfuko huu bado ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya matengenezo ya barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Usafiri na Usafirishaji Vijiji unaoteklezwa katika Halmashauri za Wilaya za Masasi, Iringa, Mbozi, Rufiji, Muheza, Morogoro na Iramba kuanzia mwaka 1995 umeonyesha mafanikio hasa kutokana na Wananchi wenye kuweza kuainisha matatizo ya usafiri yanayowakabili na kuamua kuyaondoa kwa kuchangia nguvu zao ambapo Serikali na Wahisani huchangia kiasi kidogo tu katika gharama za mradi. Katika awamu ya majaribio ya Halmashauri zilizohusika na Mpango huu, vijiji 100 vimefaidika katika mpango ikiwa ni pamoja na kuunganishwa kwenye barabara kuu pamoja na kuweza kuanzisha huduma nyinginezo. Aidha, mafanikio makubwa ya programu hii ni kama ifuatavyo:-

- (i) Barabara zenyе urefu wa Km.473 zimejengwa kwa kujitolea;
- (ii) Madaraja 96 yamejengwa;
- (iii) Magati (*landing points*) 9 yamejengwa katika maeneo ya ufukweni katika mto Rufiji (*delta areas*);
- (iv) Vyanzo vya maji 20 vimejengwa;
- (v) Huduma za SACCOS 18 zimeanzishwa;
- (vi) Uenezaji wa matumizi ya Punda na Mikokoteni 180; na
- (vii) Mafunzo yametolewa kwa Mafundi 80 wa barabara za vijiji. Kutokana na mafanikio haya Mpango huu utaendelezwa katika Halmashauri nyingine nchini kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Huduma za afya ya Msingi, chini ya mpango wa maboresho ya sekta ya afya ulioanza kutekelezwa mwaka 2000/2001 kuitia Mpango wa Mfuko wa Pamoja wa Afya, jumla ya Halmashauri 113 zimepatiwa fedha kiasi cha shilingi 26,865,447,121.00 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Mfuko.

Baadhi ya mafanikio ya Mpango huu ni kusambazwa kwa Mwongozo wa Mpango wa Mfuko wa Afya kwenye Halmashauri 113, Sekretarieti za Mikoa 21 na kwa Wadau wote wa Sekta ya Afya. Ukarabati na matengenezo madogo madogo kwa mujibu wa Mwongozo yameteklezwa katika Hospitali 53, Vituo vya afya 134 na Zahanati 77.

Aidha, huduma za Mfuko wa Mkoba (*Mobile Clinic*) na elimu ya afya na chanjo pia zimetolewa. Huduma ya chanjo ya surua imetolewa kwa kiwango cha asilimia 90. Vilevile, Kitengo cha kutolea na kukusanya takwimu za Afya kimeimarishwa katika

Halmashauri zote na jumla ya magari 549 yamenunuliwa kwa ajili ya kusambaza madawa, kufuatilia utekelezaji na shughuli za utawala katika Halmashauri na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Afya na Lishe, Mradi huu ulianza mwaka 1990/1991. Madhumuni ya mradi huu ilikuwa ni kuimarisha huduma za afya ya msingi katika Halmashauri za Wilaya za Urambo, Igunga, Iramba, Kasulu, Kibondo, Lindi, Liwale, Nachingwea, Nzega na Singida. Katika mradi huu, hospitali za Wilaya 9 zilikarabatiwa na hospitali mpya ya Wilaya ya Igunga ilijengwa; Vituo vya Afya 22 na Zahanati 39 zilikarabatiwa; vifaa na nyenzo za kufanya kazi vilinunuliwa na kusambazwa. Visima vifupi vya maji 34; vihenge 60 pamoja na vituo 3 vya kulelea watoto wadogo vilijengwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa mmoja pamoja na Waganga Wakuu wa Wilaya watatu walipata mafunzo na kupandishwa vyeo. Aidha Halmashauri zote za mradi zilipewa gari kwa ajili ya ukaguzi na usimamizi wa utekelezaji. Matokeo ya utekelezaji wa Mradi huu ni pamoja na kuongezeka kwa vifaa vya kutolea huduma za Afya katika maeneo ya Mradi na Wananchi kupatiwa huduma za kuridhisha na hivyo kuinua afya zao. Mradi huu ulimalizika mwaka 1999.

Hata hivyo kutokana na mafanikio ya mradi huu Serikali ilianzisha mradi wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini ulioanza mwaka 2000/2001.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ukarabati wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya unatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali ya Tanzania, mkopo wa Benki ya Dunia na misaada kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya unaogharamiwa na Serikali za Norway, Denmark, Uholanzi, Ireland na Shirika la Misaada la Ujerumani (*GTZ*) kwa utaratibu wa Mfuko wa Pamoja wa Afya. Tangu uanze kutekelezwa mwaka 2000/2001, Serikali imefanikiwa kuendesha mafunzo kwa Watendaji wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Wakurugenzi, Wahazini, Wahandisi, Maafisa Mipango, Waganga Wakuu wa Wilaya na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri 32 za awamu ya kwanza. Mafunzo haya yalihusu tathmini ya mahitaji ya ukarabati, taratibu na mipango endelevu ya ukarabati na vifaa vya huduma za afya. Aidha, miongozo kuhusu manunuvi na taratibu za matumizi ya fedha za ukarabati imeandaliwa na kupelekwa katika Halmashauri 32 zinazoanza kazi ya ukarabati. Halmashauri 16 kati ya 32 za awamu hii zimekwishapelekewa jumla ya shilingi bilioni 1.8 na shilingi bilioni 2.8 zitakuwa zimepelekwa kwenye Halmashauri 16 zilizobakia ifikapo tarehe 30, Juni 2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitekeleza mradi wa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya elimu katika Halmashauri zote kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu ya msingi. Katika kutekeleza jukumu hili, jumla ya shilingi 13,623,707,071 zilitolewa katika kipindi cha mwaka 1995 hadi mwaka 2001 ambazo zilifanikisha kununua vitabu vya kiada 1,534,056, makasha ya chaki 557,372, vibao vya kuandikia (*slates*) 329,531, daftari za mahudhurio 3,551,607 na kuchapisha vyeti 2,528,007 vya kumaliza elimu ya msingi nchini. Vifaa hivi vilisafirishwa na kusambazwa hadi shulenii kwa kufuata utaratibu uliozingatia idadi ya shule na wanafunzi katika Halmashauri.

Aidha, umejenga uwezo wa Watendaji wa Elimu ngazi ya Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo na pikipiki 243 kwa ajili ya usafiri. Mradi huu hivi sasa umekwishafungwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulianza kutekelezwa mwaka 2001/2002 na umekuwa wa mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoa na ongezeko la madarasa 30,457 hadi Desemba 2004; Walimu 31,421 wameajiriwa; watoto darasa la kwanza 4,397,721 wameandikishwa; nyumba za Walimu 1,213 zimejengwa; matundu ya vyoo 14,031 yamejengwa; madawati 149,743 yametengenezwa; vivunge vya sayansi 2,763 zimenunuliwa; na kutoa mafunzo kwa Kamati za Shule 13,746. Aidha, mafunzo ya kompyuta yametolewa kwa Maafisa Elimu 42 katika Sekretarieti za Mikoa na Maafisa Elimu 228 wa Halmashauri walipatiwa mafunzo yaliyohusu Muundo Mpya wa Utawala Mikoani. Mafanikio zaidi yametokana na kuzipatia shule za msingi fedha za uendeshaji na kushirikisha jamii katika kutoa maamuzi ya utekelezaji Mpango. Jumla ya shilingi 245,274,357,714.00 zimetumika katika kutekeleza Mpango kati ya mwaka ya 2001/2002 na 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari matokeo ya kutekeleza Mpango huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Uwiano wa kitabu kwa wanafunzi umeimarika kutoka kitabu kimoja kwa wanafunzi wanane (1:8) hadi wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3) kwa madarasa ya I-IV na wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watano (1:5) kwa madarasa ya V-VII;
- (ii) Baadhi ya majengo, vifaa na mazingira ya shule yameimarishwa;
- (iii) Samani zimenunuliwa, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vimeongezeka;
- (iv) Utoro umepungua kwa kiwango kikubwa shulenii kutokana na kuwepo mazingira mazuri ya kujifunzia ikilinganishwa na miaka ya nyuma;
- (v) Ajira ya walimu wapya imeongezeka hivyo kupunguza upungufu wa Walimu kwa kiwango kikubwa;
- (vi) Wananchi wameweza kuchangia nguvu zao hivyo kujenga vyumba vingi vya madarasa, kuweka madawati na kujenga vyoo kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa;
- (vii) Kamati za Shule kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji/Kamati za Mitaa zimeweza kusimamia matumizi ya fedha kikamilifu;
- (viii) Watoto wengi hasa wa kike wameandikishwa darasa la kwanza; na

(ix) Watoto walioshindwa kujiunga na shule katika mkondo rasmi wamepatiwa mafunzo kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA).

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji, kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kupunguza hali ya umaskini kwa wananchi wake, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitekeleza Mradi wa usambazaji maji na huduma za afya katika maeneo yenye ukame ya Halmashauri za Wilaya za Kondoa na Dodoma kuanzia mwaka 1995 kutokana na msaada wa Serikali ya Ubelgiji. Hadi kukamilika kwa mradi mwaka 2002 mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa visima virefu 68; visima vifupi 92; vijiji 11 vilipatiwa maji ya bomba; matanki 11 ya kuvuna maji ya mvua yalijengwa katika shule za msingi na zahanati.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mapato ya Halmashauri, hali ya ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri imeongezeka kutoka mapato ya shilingi 21,884,241,317.00 mwaka 1996 hadi kufikia shilingi 55,187,451,655.00 mwaka 2002, sawa na asilimia 152.0 ya ongezeko.

Aidha, mwaka 2003 Serikali iliamua kufuta kodi zenye kero na zisizo na tija zilizokuwa zikitozwa na Halmashauri ikiwemo Kodi ya Maendeleo, hivyo kupunguza mapato ya Halmashauri yanayotokana na vyanzo vyake kufikia makusanyo ya shilingi 20,834,429,543.00 mwezi Juni 2004.

Hatua hii iliyochukuliwa na Serikali imewezesha Wananchi wengi kushiriki kikamilifu kwa kuchangia katika shughuli za maendeleo na hivyo kuongeza kipato chao na pia kuvutia wawekezaji.

Pengo lililotokana na kufutwa kwa kodi zenye kero liliifidiwa na Serikali kwa kutoa shilingi bilioni 22.9 mwaka 2003/2004 na shilingi bilioni 25 mwaka 2004/2005 ili kuziwezesha Halmashauri kuendelea kutoa huduma zilizokuwa zikitolewa kutokana na mapato yaliyotokana na kodi zenye kero. Aidha, mfumo wa utoaji leseni za biashara ulirekebishwa ili kuondoa kero iliyokuwa inasababishwa na urasimu mkubwa wakati wa kutafuta leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu za Shirika la Elimu Kibaha, kumeiletea Serikali mafanikio makubwa katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Ujenzi wa shule ya Sekondari ya kutwa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 640, hivyo kupunguza tatizo kubwa la wanafunzi wengi wanaofaulu na kukosa nafasi ya kujiunga na masomo ya Sekondari;
- (ii) Kupanuliwa na kuboresha huduma za hospitali ya Tumbi hivyo kuongeza uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi kwa mwaka kutoka wagonjwa wa nje 120,000 mwaka 1996 hadi wagonjwa 300,000 mwaka 2005;
- (iii) Kununua na kuweka mtambo wa kutengeneza maji kwa ajili ya matumizi ya hospitali; na

(iv) Barabara ya Tumbi yenyе urefu wa kilomita 4.5 imefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami hivyo kusaidia wagonjwa hususan akina mama waja wazito na majeruhi wa ajali za barabarani kufikishwa hospitalini kwa wakati na usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa mwaka 1974 kwa madhumuni ya kusimamia na kuendesha soko kuu la Kariakoo pamoja na kujenga masoko mengine mapya na kuyasimamia. Katika kipindi cha Awamu ya Tatu, Shirika limefanikiwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato uliowezesha kiwango cha makusanyo kuongezeka kutoka shilingi milioni 334 mwaka 1995 hadi shilingi milioni 944 mwaka 2005.

Fedha hizo zilitumika katika kuboresha huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika, ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa miundo mbinu katika jengo la soko, uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara kwa kujenga vibanda vyta kuuzia na kutengeneza maumbo ya kuwekeaa bidhaa na pia kuweka viyoyozi kwenye Soko la Shimoni.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo kilianzishwa mwaka 1994 kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya Uboreshaji wa ujuzi na Stadi za kazi kwa washiriki mbalimbali kutoka katika Serikali za Mitaa. Waliopatiwa Mafunzo hayo ni pamoja na Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa 2,633, Maafisa Watendaji wa Vijiji 240, Maafisa Watendaji wa Kata 300 na Madiwani 184 kutoka Mikoa na Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Aidha, Chuo kimekamilisha uandaaji wa Mitaala inayohusu mafunzo mbalimbali katika fani ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, umefanikiwa kuwekeza vitega uchumi mbalimbali tangu uanzishwe. Vitega uchumi hivyo ni pamoja na Dhamana za Serikali, Amana za Mabenki, Hisa za Makampuni na Raslimali za Majengo kama *LAPF Millennium Tower*, Dar es Salaam na nyumba tisa za kuishi watumishi zilizopo Dodoma. Thamani ya vitega uchumi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 19.74 mwezi Juni, 2000 na kufikia shilingi bilioni 66.7 mwezi Juni, 2004. Aidha, Mfuko umefanikiwa kulipa mafao yenyе jumla ya shilingi bilioni 5.09 kwa Wanachama 26,261 waliostaafu, kufariki au kuachishwa kazi kati ya mwaka 1995 na mwezi Juni 2004. Vilevile Shirika limeanzisha utaratibu wa kutoa taarifa kwa wanachama wake mara kwa mara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero kwa wanachama wa Mfuko, hatua zimechukuliwa za kuboresha shughuli za Mfuko ikiwa ni pamoja na kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa malimbikizo ya michango inayodaiwa yanayofikia shilingi bilioni 9 yanalipwa. Hadi mwezi Mei 2005, madeni yenyе thamani ya shilingi bilioni 2.4 yamelipwa. Aidha, Serikali imeandaa mapendekezo yenyе lengo la kuufanya Mfuko kuwa wa pensheni kwa lengo la kuboresha zaidi mafao yanayotolewa kwa wanachama wake wanapostaaafu kazi kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yametokana na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ambapo fedha na mali za Bodi ziliongezeka kutoka shilingi

1,209,847,293.68 zilizokuwepo mwezi Desemba, 1995 na kufikia fedha na mali yenye thamani ya shilingi 2,594,130,387.13 mwezi Novemba, 2004. Utoaji wa mikopo na uwekezaji wa Amana za *NBC* na *CRDB Bank* na kodi inayotokana na pango, umeleta faida ya shilingi 600,635,386.00. Kutokana na mikopo iliyotolewa na Bodi kwa Halmashauri 55, Halmashauri hizo zimeweza kujenga Masoko, Kumbi za Mikutano na vituo vya mabasi.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa msukumo maalum kwa maendeleo vijijini, Sera na Mkakati wa Maendeleo vijijini vimekamilika. Nakala 9,000 za Sera zimesambazwa kwa Wadau mbalimbali. Aidha, tafsiri ya Kiswahili ya Sera imekamilika bado kuchapishwa. Vilevile, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi ibara ya 146 na Sheria Na.7 na 8 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa maendeleo umeandaliwa na kuanza kutumika kuanzia mwaka 2002. Hadi sasa Mfumo huu umeshaenezwa katika Halmashauri 60. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Mifuko ya Mikopo ya kuwezesha Wananchi kiuchumi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, imeendelea kuhakikisha kwamba Halmashauri zinachangia Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa kiwango cha asilimia 10 ya mapato yake. Halmashauri pia zimetakiwa kubuni njia bora zaidi za uendeshaji wa Mfuko wa Mikopo ya Wanawake na Vijana ikiwa ni pamoja na kuwatumia Mawakala. Aidha, Halmashauri zimetakiwa kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inarejeshwa na wanachama wanapatiwa mafunzo ya uendeshaji wa shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Udhhibit wa Uchafuzi wa Mazingira, Halmashauri zote zimetunga Sheria Ndogo zinazozuia uharibifu wa mazingira na kuzitumia kikamilifu. Aidha, Waraka wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa mwaka 2003 uliosambazwa kwa Wakuu wa Mikoa wote ulisisitiza kuhusu utunzaji wa mazingira hususan katika vyanzo vya maji. Kuanzia mwaka 2000 hadi 2004 jumla ya miti 342,283,766 ilipandwa katika maeneo mbalimbali nchini na uoto wenye ukubwa wa hekta 1,504,700 ulihifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, Kupima na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zinakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi, wataalam wa ardhi wametoa ushauri katika Halmashauri 16 kuhusu umuhimu wa kuwa na mipango bora ya ardhi. Manispaa 6 za Arusha, Morogoro Mbeya, Dodoma Tanga, Shinyanga na Jiji la Mwanza zimehimizwa kuhifadhi mazingira na kutunga Sheria Ndogo. Aidha, Sheria Ndogo 207 zimetungwa na Halmashauri mbalimbali na kati ya hizo 67 zimepitishwa na hivyo kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Vilevile, zoezi la kuainisha maeneo ya uwekezaji limefanyiwa kazi na kukamilika kwa ushirikiano kati ya wataalam kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Kituo cha Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, nakala za Sera ya Ardhi, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 zimesambazwa katika Halmashauri zote. Semina kuhusu Sera na Sheria hizo zimefanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata. Aidha, Halmashauri zote isipokuwa za Jiji la Dar es Salaam zinapata asilimia 20 ya makusanyo yanayotokana na kodi za ardhi ili kuendeleza huduma katika sekta ya ardhi. Mwongozo umetolewa ukielezea namna Halmashauri zinavyoweza kuthamini mali zake kwa kuwatumia wathamini wa ardhi waliopo na hata kwa kutumia mashirika na makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kukienzi na kukiendeleza Kilimo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Halmashauri, Asasi mbalimbali na sekta binafsi imeendelea kuhakikisha kuwa masuala ya kilimo bora yanatiliwa mkazo. Aidha maafisa ugani 1,729 wenyе sifa zinazostahili wamepangiwa kazi kwenye vijiji na kata. Usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo umefanyika.

Mheshimiwa Spika, Kuhifadhi na Kusimamia Matumizi endelevu ya Maliasili, Halmashauri zimeendelea kutekeleza Sera na Sheria Ndogo zinazohusu mazingira pale ambapo hazipo. Aidha, upo Mwongozo wa kuandaa mipango inayowiana kisekta ili kuweza kupanga matumizi endelevu ya sekta za Maliasili, Mazingira, Mifugo na Maji kwa kutumia wadau ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Utawala Bora, Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ilipitishwa na Serikali Oktoba 1998. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ilianza na Halmashauri 38 mwaka 2000. Kupitia mpango huu masuala ya Fedha, Utumishi na Utawala Bora sasa yanatekelezwa katika Halmashauri zote kwa ufanisi zaidi. Uwazi na uwajibikaji wa Halmashauri umezidi kuimarika. Idadi ya Halmashauri zenye Hati safi, zimeongezeka toka 3 mwaka 2000 hadi 39 mwaka 2003.

Aidha, idadi ya Halmashauri zilizopata hati yenye masharti imepungua kutoka 70 mwaka 2000 hadi 50 mwaka 2003. Mfumo huu unatoa fursa zaidi na kuamsha ari ya Wananchi ya kushiriki kikamilifu katika maamuzi na kutekeleza mambo yanayohusu ustawi na maendeleo yao kutokana na uelewa mpana wa programu na dhana ya utawala bora. Aidha, unaongeza uwajibikaji wa Serikali za Mitaa kwa wananchi. Serikali pia imeongeza kwa kiasi kikubwa kiwango cha ruzuku inayotolewa kwa Serikali za Mitaa kutoka shilingi bilioni 296.2 mwaka 2003/2004 hadi shilingi bilioni 498.8 mwaka 2005/2006 ili kupanua na kuboresha huduma muhimu kwa Wananchi. Ruzuku hiyo sasa imeanza kutolewa kwa kutumia vigezo maalum katika Sekta ya Elimu na Afya hivyo kuwa na ugawaji wa fedha ulio na uwazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia historia ya Serikali za Mitaa nchini na mafanikio makubwa yaliyopatikana, Serikali imeamua kutenga siku maalum ya Serikali za Mitaa itakayo adhimishwa nchi nzima kwa shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa ikiwa ni pamoa na hotuba za Viongozi, kupokea taarifa mbalimbali zinazohusu shughuli za

Serikali za Mitaa na kufanya tathmini ya mafanikio na kuweka malengo. Siku hiyo ni tarehe 1 Julai ya kila mwaka na itazinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais mwaka huu. Kauli mbiu itakuwa ni Serikali za Mitaa ni kielelezo cha Utaifa na kiini cha maendeleo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya VVU/UKIMWI, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Maambukizi ya VVU/UKIMWI kutokana na fedha inayotolewa na Serikali na Tume Taifa ya kudhibiti VVU/UKIMWI. Kati ya mwaka 2002 na 2005, watumishi 258 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya namna ya kujiepusha na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi pamoja na kutumia zana za kujikinga kwa gharama ya shilingi 92,200,000.00. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilianda Mwongozo kwa ajili ya Halmashauri zote kwa lengo la kusaidia kuunda Kamati za Kudhibiti VVU/UKIMWI katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, tathmini iliyofanyika baada ya mafunzo imeonyesha kuwa watumishi wamepata uelewa wa namna ya kujikinga na UKIMWI kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2004/2005 pamoja na maelezo ya malengo ya Mpango wa Maendeleo na Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/2005 nililiezea Bunge lako Tukufu kuwa Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini tayari vimekamilika. Nafurahi kutamka kwamba, jumla ya nakala 9,000 za Sera ya Maendeleo Vijijini zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wizara za kisekta, Mikoa na Halmashauri. Sera hiyo imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka kwa wananchi na wadau wote. Aidha, Mkakati wa Maendeleo Vijijini sasa uko kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali unaendelea kuchapishwa. Kuwepo kwa Sera na Mkakati wake kutawezesha kazi ya kuratibu na kuhuisha utekelezaji wa Sera na Mikakati ya kisekta katika ngazi ya Kijiji kuwa rahisi. Aidha, Ofisi yangu itahakikisha kuwa elimu kwa umma inatolewa ili wananchi waielewe na kuitekeleza ipasavyo kwa kushiriki kikamilifu katika maamuzi yanayohusu ustawi na maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Maendeleo Vijijini, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo umeendelea kuenezwa kwa kutumia ruzuku ya Serikali na misaada kutoka Serikali ya Austria na Mashirika ya *UNICEF, DANIDA, SIDA* na *FARM AFRICA*, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Hadi sasa Mfumo huu umeenezwu katika Halmashauri 60. Baada ya wananchi kupanga mipango yao kwa kuzingatia vipaumbele, ni jukumu lao kuhakikisha kuwa mipango ambayo imo ndani ya uwezo wao inatekelezwa ipasavyo. Aidha, Halmashauri zinaagizwa kuhakikisha kuwa mipango inayotayarishwa na wananchi inazingatiwa wakati wa kuandaa mipango yao ili kutowakatisha tamaa wananchi na kuwafanya washindwe kujitokeza katika kupanga na kutekeleza mipango yao.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii, Serikali imeanzisha Timu ya Uwezeshaji ambayo itawezesha Jamii katika ngazi ya Kijiji na Mtaa kuwa na uelewa endelevu katika shughuli zao za maendeleo. Katika kufanya hivyo vimeandaliwa Vitabu viwili nya Rejea ya Uwezeshaji katika ngazi ya Kijiji na Mtaa na Kiongozi cha Timu ya Uwezeshaji katika ngazi ya Kijiji na Mtaa. Halmashauri za Wilaya za Mfano 14 zimekwishaendesa warsha za kuunda Timu za Uwezeshaji katika ngazi za Wilaya, Kata, Kijiji na Mtaa. Halmashauri hizo ni pamoja na Masasi, Kisarawe, Kibaha, Bagamoyo, Makete, Mufindi, Hai, Ngara, Mtwara, Magu, Musoma, Kilosa na Mbarali. Ni matumaini ya Serikali kwamba utaratibu huu utasaidia katika kusukuma shughuli za maendeleo ya jamii na utoaji wa huduma bora katika Kijiji na Mtaa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa karibu Halmashauri zote hazijaweza kufikia lengo la kuchangia asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya mfuko wa wanawake na vijana. Ofisi yangu imeupokea ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wa kutumia mawakala kuendesha mfuko huu. Halmashauri zimeelekezwa kutumia utaratibu wa mawakala hususan Mabenki na *SACCOS* na baadhi ya Halmashauri zimeanza maandalizi na nyingine tayari zimeanza kuwatumia mawakala. Mfano wa Halmashauri hizi ni Manispaa zote za Mkoa Dar-es-Salaam na Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga ambazo zinatumia Benki ya Wananchi kuendesha mfuko huu. Ofisi itaendelea kufuatilia utaratibu huu wa Mawakala ili uweze kuanzisha mfuko wake wa mikopo badala ya kuendelea kutegemea fedha za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha majukumu yake, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilianda na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pendekemo la Muundo mpya ambao ulipitishwa na Kamati ya Utekelezaji ya Rais na hatimaye kuridhiwa na Mheshimiwa Rais mwezi Januari, 2005. Katika mabadiliko hayo Ofisi yangu itakuwa na Idara nane na Vitengo vinne na jumla ya watumishi wapya 178 wataajiriwa ili kukidhi mahitaji na matarajio ya muundo huo. Maandalizi ya kuutekeleza muundo mpya, yameanza kwa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2005/2006. Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha kwa kukubali kuipatia Ofisi yangu jengo mjini Dodoma lililokuwa mali ya Benki ya Nyumba ili kukidhi ongezeko la watumishi. Jengo hilo litakamilishwa kujengwa kutokana na msaada wa shilingi bilioni moja kutoka Serikali ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti za Mikoa zinaendelea kuboreshwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliendesha mafunzo ya uwekaji mfumo wa utendaji kazi Serikalini (*Performance Management System*) na uandaaji wa mipango ya utekelezaji wa majukumu ya mikoa (*Strategic Plans*). Zoezi hili la kuboresha Mipango Mikakati ya Mikoa litaendelea kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, vibali vimeendelea kutolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

Umma kulingana na uwezo wa fedha wa Serikali ili kujaza nafasi wazi katika Sekretarieti za Mikoa. Hadi sasa tayari Mikoa imeweza kujaza nafasi 89 kati ya nafasi 105 za Makatibu Tawala Wasaidizi kwenye klasta tano zilizo katika Muundo. Naikumbusha Mikoa ambayo hajajaza nafasi hizo ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Ofisi yangu inaonyesha kuwa nyumba nyingi na Ofisi za Wakuu wa Wilaya zilikuwa chakavu na nyingine kutokuwa na samani za kutosha. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali iliendelea kuzifanyia ukarabati nyumba za Wakuu wa Wilaya, kununua samani na kujenga majengo mapya katika Wilaya ambazo zilikuwa hazina ofisi au ofisi zake zilikuwa zimechakaa sana. Vilevile, katika mwaka 2005/2006, Serikali kupitia Bajeti za Mikoa imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.02 kwa ajili ya Ofisi na nyumba za Wakuu wa Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo sugu linalovikabili vituo vya Afya hapa nchi. Aidha, magari ya Wakuu wa Wilaya wengi yamechoka kwani ni ya mwaka 1999. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali imetenga kiasi cha shilingi billioni 1.89 kwa ajili ya kununua magari 25 ya Wakuu wa Wilaya ambao magari yao yamekuwa mabovu na hayafai tena kutumika katika majukumu walijonayo. Vilevile, jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa katika Vituo vya Afya ambavyo vipo katika mazingira magumu. Ununuzi wa magari haya ni ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya viongozi na watendaji, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Ofisi imeweza kuendesha mafunzo ya kuboresha taaluma, ujuzi na stadi za kazi kwa Viongozi Wakuu na watumishi katika Makao Makuu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri, ngazi ya Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji. Watumishi 56 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi yenye lengo la kuongeza tija na ufanisi wa kazi. Aidha, kwa mwaka 2005/2006, Ofisi yangu itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi kwa kuzingatia mpango wa mafunzo wa 2005 – 2008.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Wilaya 106 walipatiwa mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo wa utendaji kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, Mkuu wa Mkoa mmoja, Wakuu wa Wilaya 10 na Maafisa 11 wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, walipatiwa mafunzo ya *Information Technology and Public Sector Management* katika Chuo cha Uongozi cha Mashariki na Kusini mwa Afrika (*ESAMI*). Kutohata na msaada wa Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*), Serikali imeweza kuwapeleka Osaka Japan Wakurugenzi 2 kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Makatibu Tawala wa Mikoa 4, Wakurugenzi wa Halmashauri 8 na Afisa Mtendaji wa Kata 1. Ziara hiyo ilihusu kujifunza uboreshaji wa Serikali za Mitaa unaofanywa na Serikali ya Japan.

Mafunzo kuhusu elimu iliyopatikana katika ziara ya Makatibu Tawala, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nchini Japan, yametolewa kwa Viongozi na Watendaji Wakuu wote

Katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri katika Mikoa ya Lindi, Arusha, Iringa, Kagera, Mtwara, Kilimanjaro, Singida na Shinyanga. Aidha, Ofisi yangu imeendelea na mafunzo ya Utawala bora kwa Makatibu Tawala wa Wilaya 105 na Makatibu Tarafa wa Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Mwanza, Kagera na Mara, hivyo kufanya idadi ya Mikoa iliyopata mafunzo ya Makatibu Tarafa kufikia 19 hadi sasa. Mikoa miwili iliyobaki ya Arusha na Manyara itapatiwa mafunzo hayo katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na watumishi 98 wa Ofisi yangu, wakiwemo 20 kutoka Mikoa mbalimbali, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Halmashauri za Mkoa wa Dodoma, wamepatiwa mafunzo ya kutumia mtandao wa mawasiliano. Maafisa Serikali za Mitaa 21 walipewa mafunzo yanayohusu kazi na wajibu wao na mfumo wa Serikali za Mitaa kwa ujumla. Pia, watakwimu 45 walipatiwa mafunzo ili wazisaidie Halmashauri kuwa na takwimu sahihi. Mafunzo mengine ya Kompyuta na Mfumo wa Mawasiliano yalifanyika kwa watumishi 133 wakiwemo watumishi 20 wa Mkoa wa Dodoma na Maafisa Elimu 42 ngazi ya Mkoa wamepatiwa mafunzo ya kompyuta kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa takwimu za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Kwa kutambua umuhimu wa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa, Ofisi yangu iliendelea kuwapatia mafunzo ya kuboresha ujuzi na stadi za kazi kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa 5,580.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa mamlaka za miji midogo, miji, Manispaa na jiji, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Mamlaka ya Miji midogo 90 imetangazwa na Serikali kuititia Tangazo Na. 353 la tarehe 17 Septemba, 2004. Vilevile, kwa Tangazo la Serikali Na.352 Mamlaka za Miji midogo ya Korogwe, Kibaha na Babati zilipandishwa hadhi kuwa Halmashauri za Miji. Maandalizi ambayo yamefanywa ni pamoja na kuwapata Watendaji Wakuu na watumishi wengine na kugawana mali kati ya Halmashauri za zamani na mpya. Aidha, Serikali imeanza utaratibu wa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Mpanda na Manispaa nane za Songea, Mtwara/Mikindani, Sumbawanga, Singida, Kigoma/Ujiji, Bukoba, Musoma na Arumeru na Halmashauri za Jiji la Arusha na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, demokrasia na utawala bora ngazi ya Kijiji, Ofisi yangu ilitekeleza ahadi yake ilioitoa kwenye Bunge la Bajeti mwaka jana kwa kuwagawia Waheshimiwa Wabunge Taarifa ya Demokrasia na Utawala Bora Ngazi ya Kijiji (*Village Democracy Initiative*). Aidha, Ofisi itaifanyia kazi maoni na mapendekezo yatakayotolewa.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji ulifanyika mwezi Novemba 2004 kama ulivyopangwa. Serikali za Mitaa ziliendesha na kusimamia uchaguzi huo kama nilivyoelezea katika hotuba yangu ya mwaka jana. Kwa mujibu wa Sheria Na. 7 na Na.8 za mwaka 1982, Ofisi yangu iliandaa Kanuni na kuziwezesha Halmashauri kuendesha uchaguzi huo. Kanuni hizo zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.314, 315, 316, 317, 318 na 319 la tarehe 3 Septemba 2004. Kanuni zilielezea utaratibu wa kuwatambua wapiga kura wenye sifa kwa

kutumia Rejesta ya Wakazi wa kila eneo na ziliweka utaratibu wa kupokea na kushughulikia pingamizi na malalamiko ambayo yangetolewa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Oktoba 2004, Viongozi 12 wa Vyama mbalimbali vya Siasa walifungua Shauri la Kikatiba Na.97 la mwaka 2004 katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Viongozi hao waliomba kuwa orodha ya wapiga kura isitokane na Rejesta ya Wakazi na uchaguzi wa Serikali za Mitaa usimamishwe mpaka kesi ya Kikatiba itakapoamuliwa na Mahakama. Mahakama Kuu ilitoa uamuzi wake tarehe 9 Novemba, 2004, kuwa uchaguzi ulioitishwa tarehe 21/11/2004 na 28/11/2004 uendelee kufanyika isipokuwa Rejesta ya Wakazi isitumike katika kutambua wapiga kura kwenye uchaguzi huo. Uchaguzi ulifanyika tarehe 21/11/2004 kuchagua Viongozi wa Vitongoji na tarehe 28/11/2004 kuchagua Viongozi wa Vijiji na Mitaa kama ulivyopangwa. Aidha, Vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi huo ni Chama cha Mapinduzi (CCM), *The Civic United Front (CUF)*, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), *Tanzania Labour Party (TLP)*, *National Convention for Construction and Reform (NCCR-MAGEUZI)*, *United Democratic Party (UDP)*, Chama cha Haki na Ustawi (CHAUSTA), *Tanzania Peoples Progressive Party (TPPP)*, *Tanzania Democratic Alliance Party (TADEA)*, *United for Multiparty Democracy (UMD)*, *Democratic Party (DP)*, Demokrasia Makini (MAKINI), *National League for Democracy (NLD)*, *The Forum for Restoration of Democracy (FORD)*, *National Reconstruction Alliance (NRA)* na *United Peoples Democratic Party (UPDP)*. Kufuatia uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika, Chama cha Mapinduzi kilifanikiwa kushinda kwa kishindo katika ngazi zote asilimia 94 katika ngazi zote na Vyama vingine viligawana asilimia 6 iliyobaki. Nachukua nafasi hii, kuvipongeza Vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizi na wale wote waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa uliendeshwa vizuri isipokuwa katika maeneo machache kutohana na kukiukwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi. Tarehe 12 Novemba 2004, nilitoa kauli ya Serikali kuhusu uchaguzi huo ambayo ilifanua masuala ya kisheria yaliyotokana na hukumu ya Mahakama Kuu kwa madai yaliyofunguliwa na Vyama 12 vya upinzani dhidi ya uchaguzi huo. Katika kauli hiyo nilieleza kuwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Kijiji, Mtaa na Kitongoji umetupa uzoefu ufuatao:-

- i. Umuhimu kwa Serikali kuendelea kutoa elimu ya uraia na elimu kwa wapiga kura kwa kushirikiana na wadau wengine;
- ii. Umuhimu wa Vyama vya Siasa na wananchi kwa ujumla kujenga utamaduni wa uvumilivu wa kisiasa, ikiwa ni pamoja na kuwa na mila na desturi ya kukubali matokeo; na
- iii. Umuhimu wa wananchi na wahusika wote kutambua kuwa, uchaguzi ni nyenzo ya kuimarisha utawala wa kidemokrasia na kamwe si chombo cha kuvuruga uhuru, utilivu na umoja mionganoni mwa wananchi bali ni hatua ya kutia chachu katika juhudi za kuleta maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2004/2005, ilikuwa shwari kwa Mikoa yote licha ya kuwepo na matukio machache ya

uvunjaji wa amani kama vile kubaka, wizi wa kutumia nguvu na kukamatwa kwa baadhi ya silaha. Matukio hayo yote yalishughulikiwa kwa ushirikiano wa raia wema na Jeshi la Polisi. Aidha, kumekuwepo na tatizo la Wakimbizi hasa katika Mikoa ya Kigoma na Kagera ambao wamekuwa wakijishughulisha na vitendo viovu kama vile wizi, unyang'anyi, ubakaji, uporaji na mauaji. Wakimbizi hawa wamekuwa wakitoroka makambini na kujihusisha na vitendo hivyo. Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na tatizo hili kwa kufanya vikao vya ujirani mwema na nchi watokazo wakimbizi ili kuwarejesha katika nchi zao. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imehakiki na kusajili jumla ya Vijiji 9,822 kufikia mwaka 2004, baada ya kupokea rasmi maombi ya kusajiliwa. Aidha, yapo maombi ambayo hayakushughulikiwa kwa sababu usajili wa vijiji ulisitishwa kutokana na masuala ambayo Halmashauri hazikuzingatia. Ili Msajili wa Vijiji aweze kukisajili kijiji kumbukumbu zifuatazo zinahitajika:-

- i. Muhtasari wa wanakijiji husika wakiomba kijiji chao kugawanywa;
- ii. Muhtasari wa Kamati ya Maendeleo ya Kata;
- iii. Muhtasari wa Baraza la Madiwani;
- iv. Fomu Na. 1 inayoelezea takwimu mbalimbali za kijiji husika;
- v. Kijiji kuwa na kaya zisizopungua 250 zenyе makazi ya kudumu; na
- vi. Kuwepo na maeleo ya mipaka yanayofahamika na wananchi.

Napenda kutoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, ambao ni Wasajili wasaidizi, kuambatanisha kumbukumbu hizo wanapowasilisha maombi ya vijiji vya kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala, Ofisi yangu imepokea maombi mbalimbali ya kuanzishwa kwa vijiji, mitaa, kata, wilaya na mikoa. Ofisi yangu imekwishafanya uchambuzi wa maombi hayo ili kuondokana na utaratibu wa sasa wa kusubiri maombi. Utekelezaji wake utategemea hali yetu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ajira za maafisa watendaji wa vijiji na mitaa, mwezi Machi, 2003 Serikali ilitoa kibali cha kuajiri Watendaji wa Vijiji 9,803. Hadi Mei 2005, jumla ya Watendaji 7,770 wameajiriwa na Halmashauri na mishahara yao kulipwa na Serikali. Taratibu zinaendelea ili nafasi zilizobaki zijazwe. Ajira ya Maafisa Watendaji wa Mitaa itaanza rasmi mwezi Julai 2005, ambapo wataajiriwa Maafisa Watendaji wa Vijiji 2,481 na Maafisa Watendaji wa Mitaa 1,755. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali italipa mishahara ya Maafisa Watendaji wote watakaoajiriwa. Jumla ya shilingi bilioni 11.6 zinaombwa katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 kwa ajili ya mishahara ya Maafisa hao. Napenda kuwakumbusha Maafisa Watendaji wale waliokuwa katika ajira za kudumu kujiendeza kielimu ili watimize masharti yanayoambatana na ajira zao.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Serikali za Mitaa, kama nilivyotoa taarifa mwaka 2004/2005, Serikali ilitenga shilingi bilioni 25 kama ruzuku isiyo na masharti kwa ajili ya fidia kwa Halmashauri kwa vyanzo vya mapato vilivyofutwa. Kwa mwaka 2005/2006, kiasi cha shilingi bilioni 40.1 kimetengwa na Serikali kwa madhumuni hayo. Aidha, Halmashauri zimeweza kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 20.8 kutokana na vyanzo vyake ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 25.0 sawa na asilimia 83.2. Halmashauri zinahimizwa kusimamia vizuri mapato yanayotokana na vyanzo vya mapato vilivyobaki na kutumia vizuri fidia inayotolewa kwa kuzingatia Sheria na Miongozo mbalimbali ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri sasa inatoa leseni katika kituo kimoja kama nilivyoiliarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana. Utaratibu huu umewaondolea kero na kuleta tija kwa wafanyabiashara na kuwawutia wananchi wengi kufanya biashara kwa kupata leseni bila vikwazo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mfanyakibashara wa zamani anapata leseni yake kwa siku moja na mpya anapata leseni baada ya siku saba.

Aidha, Halmashauri hazitozi ada za leseni kwa biashara zenyе mauzo yasiyozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka. Napenda kutoa wito kwa wafanyabiashara kuendelea kulipa kodi na ada kwa mujibu wa Sheria na kuendesha biashara katika maeneo yanayoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimeendelea kufunga vitabu na kuwasilisha hesabu kwa Wakaguzi kwa wakati. Kwa mujibu wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinazoishia Desemba 2003, kati ya Halmashauri 117, Halmashauri 39 zilipata hati safi sawa na asilimia 33 ikilinganishwa na Halmashauri 20 mwaka 2002. Halmashauri 50 zimepata Hati yenye masharti ikilinganishwa na Halmashauri 70 mwaka 2002. Kulingana na takwimu hizi hali ya usimamizi na nidhamu ya fedha imeongezeka. Hata hivyo, bado zipo Halmashauri chache ambazo hazifanyi vizuri. Ili kuboresha zaidi usimamizi na ufungaji wa mahesabu ya Halmashauri, Serikali inaendelea kuzichukulia hatua Halmashauri zenyе mapungufu, kutoa mafunzo kwa Wahasibu na kuwapatia vitendea kazi. Nachukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zilizopata Hati Safi na kuzihimiza Halmashauri nyingine kuchukua hatua za haraka kurekebisha utunzaji na uandikaji wa vitabu vya hesabu kwa mujibu wa kanuni za fedha zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea kushughulikia madeni ya Watumishi na Wazabuni ambayo ni ya hadi kufikia tarehe 30 Juni 2001 katika Halmashauri zote nchini. Katika kipindi cha 2004/2005 madai ya watumishi mbalimbali wakiwemo walimu yameendelea kulipwa. Aidha, kwa mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kulipa madeni ya Watumishi wa Halmashauri pamoja na madeni ya Wazabuni waliotha huduma kabla ya tarehe 30 Juni 2001 katika Halmashauri

yenye thamani ya shilingi 12,286,966,082.84 Halmashauri zote zinaagizwa kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha kwa kuzingatia Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ili kuepukana na madeni yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imeendelea kupambana na Rushwa kwa kuzingatia Mkakati wa Kitaifa wa Vita dhidi ya Rushwa. Mwaka wa fedha 2004/2005 Warsha ya Maadili na Utawala Bora kwa Viongozi na Watendaji imefanyika katika Manispaa za Temeke, Kinondoni na Ilala. Aidha, Warsha mbalimbali za Wadau zimeendeshwa na Kamati za Kupambana na Rushwa zimeundwa katika ngazi za Wilaya.

Katika mwaka 2005/2006 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri zote nchini, itatekeleza Mpango Maalum wa Kupambana na Rushwa kuanzia mwezi Julai, 2005. Mpango huo umezingatia sekta zote zinazolalamikiwa kuhusika na Rushwa katika ngazi za Halmashauri zikiwemo Elimu, Afya, Maliasili, Biashara, Utawala, Fedha na Ardhi. Mpango huu umeandaliwa na Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi yangu pamoja na Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Lengo katika mwaka 2005/2006 ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Vita dhidi ya Rushwa kama ulivyoidhinishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Vita dhidi ya VVU/UKIMWI, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi wake ili kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Mikakati na mipango ya kupambana na ugonjwa huu wa hatari katika ngazi zote iliendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Asasi mbalimbali.

Aidha, Serikali iliingia mkataba na Mfuko wa Dunia wa kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI (*Global Fund Round One*) ili kugharimia baadhi ya shughuli za vita dhidi ya UKIMWI. Katika mkataba huo, Halmashauri kumi na mbili zilipata fedha kutoka Mfuko huo kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Halmashauri hizo ni Makete, Tunduru, Bukoba, Sumbawanga, Hai, Masasi, Magu, Kyela, Kisarawe, Kilombero, Kibondo na Kinondoni. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Mradi huu kwa kipindi cha miezi kumi na nane ni Dola za Kimarekani milioni 4.8. Hadi sasa zimepokelewa Dola za Kimarekani milioni 1.48 katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yafuatayo yamefanyika: -

- (i) Kutoa mafunzo kwa kamati za kudhibiti maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI za Halmashauri kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania;
- (ii) Kuzipatia fedha Halmashauri kumi na mbili zinazotekeleza Programu ya UKIMWI inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na VVU/UKIMWI. Jumla ya shilingi 1,485,000,000.00 zilitolewa kwa Halmashauri hizo. Sehemu kubwa ya fedha hizi zimetumika katika kuwasaidia waathirika, yatima na wajane;

- (iii) Kutoa mafunzo ya uelimishaji rika juu ya VVU/UKIMWI kwa shule za msingi katika Halmashauri 12;
- (iv) Kushirikiana na Mashirika yanayojishughulisha na masuala ya UKIMWI katika Halmashauri;
- (v) Kuzisaidia Halmashauri kufungua akaunti maalum kwa ajili ya masuala ya UKIMWI;
- (vi) Kutayarisha Mkakati wa Ofisi wa kupambana na UKIMWI. Mkakati huu ni kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri; na
- (vii) Kutayarisha Mwongozo wa uelimishaji rika kwa shule za msingi kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mwongozo huu utasambazwa kwa Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Ofisi yangu itaendelea na mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI. Kitengo cha kuratibu shughuli za UKIMWI katika Halmashauri kitaimarishwa kwa nia ya kusimamia shughuli zinazofanywa na Mashirika pamoja na wadau wengine. Katika Halmashauri, mkazo mkubwa utawekwa katika maeneo yafuatayo: -

- (i) Mafunzo (kwa maana ya kujenga uwezo);
- (ii) Kuratibu shughuli za wadau mbalimbali katika Halmashauri;
- (iii) Usimamizi wa karibu wa fedha za Serikali pamoja na za Wahisani; na
- (iv) Ufutiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Ukusanyaji wa Takwimu za Kiutawala, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inaratibu shughuli za Kikundi kazi inachosimamia Mfumo wa ukusanyaji na utumiaji wa takwimu za kiutawala za kila siku (*Routine Data System*). Kikundi hicho kinajumuisha wajumbe kutoka Wizara tano (Afya, Ujenzi, Kilimo na Chakula, Maji na Mifugo na Elimu na Utamaduni), wahisani na Idara za Serikali zikiwemo, Wakala wa Taifa wa Takwimu na Chuo cha Takwimu. Usimamizi wa Mfumo huo, kama nyenzo mojawapo ya kuondoa umaskini umeainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 ni pamoja na kuendesha warsha zilizohusisha Wizara hizo 5 na Watendaji wa Halmashauri zote nchini, Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na vyama visivyo vya Kiserikali kwa nia ya kuelezea umuhimu wa kuwa na takwimu za kiutawala zilizo na kiwango bora kama njia mojawapo ya kuondoa umaskini nchini. Mkakati wa kitaifa umeandaliwa wenye lengo la kuhakikisha takwimu za kiutawala zinakusanywa na kutumika kwenye Wizara, Taasisi na kila mdau hapa nchini.

Aidha, Wajumbe wa kikundi kazi walitembelea Wilaya sita kuona jinsi Halmashauri zinavyokusanya na kutumia takwimu za kiutawala kwa ajili ya kuleta maendeleo. Vilevile, Mkakati wa Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti na utoaji wa taarifa kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa uliandaliwa na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa ulianza kutekeleza Mpango Mkakati wa Mfuko wa miaka mitano (2004/2005 hadi 2008/2009) kwa kuzingatia majukumu yake makuu yaliyofafanuliwa katika Sheria Na. 6 ya mwaka 2000 kama yafuatavyo:-

- (i) Kuhakikisha kuwa unakuwepo mpango wa malipo ya mafao kwa wanachama wanapostaafu;
- (ii) Kusimamia mpango uliopo wa hifadhi ya jamii kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na wengine waliojiunga; na
- (iii) Kubuni na kutekeleza mikakati endelevu ya kuboresha mafao ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, Mfuko ulifanyiwa uthamini wa kitaalam (*actuarial valuation*) ilioonyesha kuwa Mfuko wa sasa wa Akiba una uwezo wa kubadilishwa na kuwa Mfuko wa malipo ya pensheni. Taarifa ya uthamini huu imekwishawasilishwa Serikalini na mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuubadilisha Mfuko huu kuwa wa malipo ya Pensheni unaandaliwa. Ili kusogea huduma karibu zaidi na wanachama, Mfuko umeanzisha Ofisi 3 za Kanda katika miji ya Dar es Salaam (Kanda ya Mashariki), Mwanza (Kanda ya Ziwa) na Arusha (Kanda ya Kaskazini). Pia, katika mwaka 2004/2005 semina mbalimbali za wanachama, waajiri na Wadau wengine ziliendeshwa kikanda ili kupata maoni yao kuhusu Mpango wa pensheni na namna ya uendeshaji wake. Aidha, Mfuko uliandikisha wanachama 61,596 ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanachama 60,274.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Machi 2005, Mfuko ulikusanya shilingi bilioni 25.96 ikiwa ni michango ya wanachama na marejesho ya fedha zilizowekezwa katika Dhamana za Serikali na Amana za Mabenki, Riba na kodi ya pango inayotokana na vtegauchumi mbalimbali vya Shirika. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 8.3 ni michango ya wanachama ambayo ni sawa na asilimia 113.7 ya lengo la mwaka 2004/2005 la kukusanya shilingi bilioni 7.3.

Ili kuongeza mapato, Mfuko uliwekeza shilingi bilioni 30.0 sawa na asilimia 98.5 ya lengo la kipindi hicho la kuwekeza shilingi bilioni 30.45 na hivyo kufanya jumla ya fedha zilizoko katika vtegauchumi mbalimbali kufikia shilingi bilioni 68.4. Katika kipindi hiki pia, Mfuko umekua kutoka shilingi bilioni 65.6 hadi kufikia shilingi bilioni 76.4 mwaka 2004/2005 ilipofika mwezi Machi 2005. Aidha, Mfuko ulilipa jumla ya shilingi bilioni 1.48 ikiwa ni mafao kwa wanachama 3,048 kati ya wanachama 3,536 waliofungua madai wakiwemo 557 waliopunguzwa kazi katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Mfuko unatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha taratibu za kuufanya Mfuko kuwa wa malipo ya pensheni;
- (ii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kompyuta na kuendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na tija;
- (iii) Kutoa elimu kwa Wadau na umma kwa jumla juu ya shughuli zake;
- (iv) Kusimamia uendeshaji wa mfuko mpya wa pensheni; na
- (v) Kuanzisha Ofisi za Kanda ya Kati na ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Serikali pamoja na Halmashauri ziliendelea kutoa michango ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya 1982 iliyounda Bodi. Hadi sasa Bodi imetekeliza kazi zifuatazo:-

- (i) Kukusanya jumla ya shilingi 206,725,766.25 toka Halmashauri kati ya lengo la shilingi 618,124,200.00 na mchango wa Serikali wa shilingi 200,000,000.00;
- (ii) Kutoa mikopo ya jumla shilingi 417,985,080.00 katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya na Ilala na Halmashauri ya Wilaya ya Geita; na
- (iii) Kufuatalia marejesho ya mikopo ya shilingi 101,882,456.00 na riba ya shilingi 39,643,191.05 toka kwenye Halmashauri zilizokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya upembuzi yakinifu wa Muundo wa Bodi utakaoleta tija imekamilika na mapendelekezo yamekwishatolewa na sasa Serikali inayafanyia kazi. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri ambazo zimechangia katika Bodi na kurejesha mikopo kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri ambazo bado hazijachangia kikamilifu na ambazo zimeshindwa kurejesha mikopo kama inavyotakiwa zinakumbushwa kutekeleza wajibu huo wa kisheria haraka ili kuiwezesha Bodi kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, programu ya kuboresha Mazingira Mijini ilianzishwa mwaka 1992 katika Jiji la Dar es Salaam kwa madhumuni ya kuimarisha uwezo wa Jiji wa kupanga, kuratibu na kusimamia ukuaji na maendeleo yake kwa kushirikiana na sekta za umma, binafsi na vikundi visivyo vya kiserikali. Mwaka 1997 Mfumo huo ulianza kutumika katika Halmashauri za Manispaa za Mwanza, Tabora, Arusha, Moshi, Tanga,

Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya. Programu hii ilipata msaada kutoka *UNDP* na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi hadi mwezi Desemba, 2001 mradi ulipokwisha. Aidha, toka mwaka 1998 Serikali ya Denmark kuititia Shirika lake la misaada la *DANIDA* imeendelea kuendesha Programu hii kwenye Miji ya Moshi Tanga, Morogoro na Iringa.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2004/2005 ni pamoja na:-

- (i) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika Halmashauri za Jiji na Manispaa hapa nchini katika kupanga na kusimamia ukuuaji na maendeleo ya Miji kwa kuwashirikisha wananchi;
- (ii) Kuendesha warsha iliyowashirikisha maafisa kutoka *ALAT, UN Habitat, DANIDA* na Wakurugenzi wa Manispaa zinazotekeleza Mfumo wa Usimamizi na Upangaji Kimazingira; na
- (iii) Kuendesha kikao cha Kamati ya Taifa kwa lengo la kusimamia na kutoa miongozo ya utekelezaji wa Programu Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Programu inalenga kutekeleza yafuatayo: -

- (i) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu katika Miji inayofadhiliwa na *DANIDA*;
- (ii) Kuimarisha usimamizi wa taarifa za Kimazingira;
- (iii) Kuendesha warsha juu ya ushiriki na ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na usimamiaji wa Miji kwa kutumia mfumo unaojali mazingira;
- (iv) Kuimarisha Kitengo kinachosimamia programu (*Urban Authority Support Unit*); na
- (v) Kuandaa rasimu ya Programu ya Kitaifa ya usimamizi wa Mazingira katika Halmashauri zote nchini itakayoanza kutekelezwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Shirika la Elimu Kibaha limetoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 109 wa shule ya awali, wanafunzi 954 wa shule ya msingi, na wanafunzi 1,075 wa sekondari. Aidha, Hospitali ya Tumbi pamoja na kazi zingine, imehudumia wagonjwa 353,960 wakiwemo majeruhi wa ajali za barabarani 1,331 na Akina mama 108 walipatiwa mafunzo ya elimu ya lishe bora sambamba na watoto wao kupata huduma ya tiba ya maradhi ya Utapiamlo. Vilevile, elimu kuhusu UKIMWI na utunzaji wa mazingira ilitolewa kwa wafanyakazi na wanafunzi wote.

Mheshimiwa Spika, Shirika liliendelea pia na utoaji wa mafunzo ya stadi mbalimbali. Wanachuo 143 wa Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kibaha walipatiwa mafunzo mbalimbali katika fani za uashi, useremala, ufundi magari, ufundi bomba, umeme, kilimo, sayansi kimu na udereva. Chuo cha Maafisa Tabibu kilihudumia Wanachuo 116 wa mwaka wa kwanza na wa tatu. Aidha, vifaranga 699,364 na lita 120,000 za maziwa viliuzwa kwa wananchi. Kazi zingine zilizotekelawa ni pamoja na: -

- (i) Ukarabati wa maabara na mabweni ya Shule ya Sekondari Kibaha;
- (ii) Ujenzi wa uzio katika mabwawa ya majitaka;
- (iii) Ukarabati wa nyumba za wafanyakazi;
- (iv) Ukarabati wa mabweni ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha;
- (v) Ujenzi wa maabara tatu na madarasa manne ya Shule ya Sekondari Tumbi;
- (vi) Upanuzi wa Hospitali ya Tumbi;
- (vii) Uvnunaji wa maji ya mvua katika Hospitali ya Tumbi; na
- (viii) Ukarabati wa km. 0.5 za barabara ya ndani.

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Shirika litaendelea na jitihada za kupambana na ujinga, maradhi, na umaskini, kutoa huduma mbalimbali kwa jamii pamoja na ukarabati wa miundombinu ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ni pamoja na:-

- (i) Kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa viongozi na watumishi walio katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa;
- (ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya taaluma ya Serikali za Mitaa;
- (iii) Kutoa mafunzo juu ya mabadiliko yanayohusu Serikali za Mitaa kulingana na Programu ya Ubreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa na;
- (iv) Kutoa ushauri kwa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na watu binafsi juu ya masuala yote yanayohusu Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Chuo kimeendelea kutumika katika uendeshaji wa mafunzo ya muda mfupi yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuboresha ujuzi na stadi za kazi kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji kutoka Mikoa ya Manyara, Singida na Tanga. Vilevile, Chuo

kimekamilisha uandaaji wa rasimu za mitaala ya mafunzo ya muda mrefu katika fani za Utawala na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa pamoja na Usimamizi wa Fedha za Serikali za Mitaa. Aidha, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mkuu wa Chuo hicho ameajiriwa na hatua za kuajiri watumishi wengine 30 wa kada mbalimbali zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

- (i) Kuendelea kuboresha mazingira ya Chuo;
- (ii) Kujenga mfumo wa maji safi na salama kutoka kwenye chanzo chenye uhakika;
- (iii) Kuajiri wakufunzi na watumishi wengine wa kusimamia masuala ya utawala na fedha;
- (iv) Kununua vyombo vyaa usafiri;
- (v) Kuandaa na kuendesha mafunzo ya uboreshaji ujuzi na stadi za kazi kwa ajili ya Maafisa Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa; na
- (vi) Kukarabati baadhi ya majengo ya Chuo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko Kariakoo katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Shirika liliendelea kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato na hivyo kuliwezesha Shirika kukusanya wastani wa shilingi 78,739,920.90 kwa mwezi;
- (ii) Kutengeneza maumbo 104 ya kufanya biashara ndogo ndogo kwa gharama ya shilingi 7,394,000/. Idadi hiyo imefanya maumbo yalijotengenezwa hadi sasa kufikia 1,333;
- (iii) Kujenga maturubai katika eneo la mita za mraba 1,161. Kazi hii imegharimu kiasi cha shilingi 79,000,000/= imefanya eneo lililojengwa kufikia mita za mraba 1,779.87. Eneo lililobaki (mita za mraba 2,100) litajengwa katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na mwaka 2006/2007;
- (iv) Kuboresha soko la jumla kwa kufunga sehemu mbili za kupitishia hewa na kufunga vipooza hewa vipyta 26;
- (v) Kulipa madeni jumla ya shilingi milioni 67.2 kati ya shilingi 101,015,574.00 zilizokuwa zinadaiwa. Madeni haya yalitokana na huduma za miaka ya nyuma; na
- (vi) Kununua vitendea kazi mbalimbali vyaa wafanyakazi ambavyo vimegharimu shilingi milioni 3.27.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006, Shirika limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- (i) Kuendelea na awamu ya pili ya kukarabati paa la jengo la soko Kuu;
- (ii) Kuendelea na ujenzi wa maturubai katika soko la wazi lenye eneo la mita za mraba 674.8 kwa lengo la kuwakinga wafanyabiashara ndogo ndogo dhidi ya juu na mvua;
- (iii) Kukamilisha kazi ya kufunga vipooza hewa vipyta soko la jumla (Shimoni);
- (iv) Kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za Soko la Kariakoo; na
- (v) Kuliedeleza eneo la kiwanja cha Tabata na soko dogo kwa kuwashirikisha wataalamu washauri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ambayo lengo lake ni kupunguza umaskini kwa kuwawezesha wananchi kupata huduma bora kuitia Serikali za Mitaa. Kazi zifuatazo zilitekelezwa hadi kufikia Mwezi Mei 2005:-

- (i) Kuwaelimisha wananchi kuhusu maana ya mabadiliko, nafasi na wajibu wao katika kufanikisha lengo kuu la programu;
- (ii) Kuandaa kanuni za utawala bora katika ngazi ya jamii (vijiji, vitongoji na mitaa); uendeshaji wa shughuli za Halmashauri; miongozo ya uandaaji wa mipango shirikishi ya maendeleo na mapambano dhidi ya rushwa;
- (iii) Kuendelea na uboreshaji wa miundo na mifumo mbalimbali ya utumishi kwa madhumuni ya kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi;
- (iv) Mchakato wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa umekamilika katika Halmashauri 38 na unaendelea katika Halmashauri 76 zilizosalia; na
- (v) Mwongozo wa kushirikisha Sekta binafsi umeandalila na umeanza kutumika katika Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, kazi zifuatazo pia zimetekelozwa:-

- (i) Maandalizi ya mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya mipango (*Plan-Rep*) na mbinu ya uchambuzi wa umaskini (*Poverty Audit*) yamekamilika na mafunzo yanetolewa kwa Maafisa katika Sekreterieti za Mikoa na Halmashauri;
- (ii) Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utoaji wa Huduma katika ngazi ya Serikali za Mitaa ultiandalila na mafunzo juu ya utekelezaji wake katika ngazi ya Sekretarieti na katika ngazi ya Halmashauri yalikamilika;

- (iii) Rejesta za Wakazi wa Vijiji na Mitaa zilichapishwa na kusambazwa katika Halmashauri zote;
- (iv) Mafunzo kazini kuhusu Usimamizi wa Fedha, yalitolewa kwa watumishi wa Halmashauri zilizodhihirika kuwa na udhaifu katika usimamizi wa fedha;
- (v) Vigezo vya kugawa ruzuku ya matumizi ya kawaida kwa sekta za Kilimo na Maji vilikamilishwa na vilitumiwa katika kuweka viwango vya ruzuku kwa mwaka 2005/2006;
- (vi) Mfumo mpya wa kuzipatia Halmashauri za Miji na Wilaya Ruzuku ya Maendeleo ulikamilishwa na umeanza kutumika;
- (vii) Mwongozo wa jinsi ya kuendesha ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa uliandaliwa na kukamilishwa na mafunzo yametolewa kwa viongozi na watumishi wahusika katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Mafunzo hayo yamehusisha pia wawakilishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ngazi ya Mko. Aidha, mafunzo na maelekezo kuhusu Kanuni na Taratibu za manunuzi katika Halmashauri yaliendelea kutolewa na ufuatiliaji kuhusu matumizi ya Kanuni hizo umeendelea kufanyika; na
- (viii) Kuzijengea mazingira ambayo yatazipatia Halmashauri fursa na uwezo wa kuajiri, kuendeleza na kusimamia nidhamu ya watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, kazi zitakazotekeliza ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuandaa miongozo kuhusu uwianishaji wa masuala ya jinsia katika mipango na shughuli za Serikali za Mitaa na kupeleka madaraka, majukumu na rasilimali kutoka ngazi ya Halmashauri hadi ngazi ya jamii;
- (ii) Kuweka taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi kwa wananchi;
- (iii) Kuwezesha utekelezaji wa muundo mpya pamoja na mpango wa kujengea uwezo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa;
- (iv) Kuendelea kuboresha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji Mipango (*Plan Rep*) pamoja na ule wa ufuatiliaji wa viwango vya utoaji huduma katika Halmashauri;
- (v) Kuzisaidia na kuziimarisha Halmashauri 38 za awamu ya kwanza katika kutekeleza Mipango Mkakati na Miundo yao iliyoboreshwa na inayojumuisha mifumo mipy ya utumishi;
- (vi) Kuziwezesha na kuzisaidia Halmashauri 76 kukamilisha uandaaji wa Mipango Mkakati, Miundo na Mifumo ya utumishi;
- (vii) Kuimarisha usimamizi wa fedha na ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa;

(viii) Kuendelea kueneza Mfumo wa utunzaji wa hesabu kwa kutumia Mfumo wa "Epicor" katika Halmashauri zilizosalia;

(ix) Kuendelea kutumia Mfumo wa kuzipatia Halmashauri ruzuku ya maendeleo; na

(x) Kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, malengo yafuatayo pia yatakelezwa katika mwaka 2005/2006:-

(i) Kuendelea kuwianisha sheria, kanuni na taratibu zinazotawala ajira na usimamizi wa watumishi wa Serikali za Mitaa ili kuondoa migongano ya kisera na kisheria inayojitokeza katika utekelezaji wa sheria husika;

(ii) Kuendelea kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa ili ziweze kuwa na uwezo wa kuajiri, kuendeleza na kusimamia watumishi wao;

(iii) Kubuni na kutekeleza programu za mafunzo kwa ajili ya viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wa Halmashauri;

(iv) Kuendelea kusimamia na kuratibu zoezi la tathmini ya kazi (*Job Evaluation and Re-grading*) za watumishi wa Halmashauri kwa lengo la kuongeza mishahara inayolingana na majukumu yao;

(v) Kuendelea kuzisaidia Halmashauri katika kuboresha uwekaji na utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za watumishi;

(vi) Kufanya mapitio na kupendekeza marekebisho yanayohitaji kufanywa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kusimika dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi; na

(vii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakusanyaji wa takwimu katika ngazi za Vijiji na Mitaa kwa lengo la kuboresha usahihi wa takwimu zinazokusanywa na kutumika katika ngazi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulianza kutekelezwa mwezi Julai 2001, ukiwa na lengo la kuboresha elimu ya msingi nchini kwa kuinua kiwango cha uandikishaji wa watoto na ubora wa elimu, kujenga uwezo na mifumo ya taasisi. Mpango huu unagharimiwa na fedha kutoka Serikalini, wahisani, michango ya wananchi na mkopo kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 150 zilizokuwa zinatolewa kwa kiwango cha Dola milioni 50 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango kwa mwaka 2004/2005 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Jumla ya watoto 1,235,917 kati ya lengo la wanafunzi 1,041,880 ikiwa ni sawa na asilimia 119, waliandikishwa kuingia darasa la kwanza hadi Machi 2005. Kati ya hao wasichana ni 609,861 na wavulana ni 626,056;
- (ii) Nyumba za walimu 1,024 zimekamilika na nyumba 6,249 ujenzi unaendelea;
- (iii) Jumla ya walimu 10,478 wamepangwa na kuripoti katika Halmashauri kwenda kufundisha shule za msingi;
- (iv) Vyumba vya madarasa 1,342 vimejengwa na kukamilika na vyumba vya madarasa 5,611 ujenzi unaendelea;
- (v) Mafunzo ya uendeshaji shule na usimamizi wa fedha kwa Kamati za shule yaliendelea kutolewa ili kuimarisha usimamizi na uwajibikaji;
- (vi) Shule zote zimepelekewa fedha za uendeshaji kupitia Halmashauri zao;
- (vii) Kuendesha mafunzo ya kuboresha stadi za usimamizi wa uendeshaji wa elimu ya msingi kwa Viongozi na Watendaji Wakuu ngazi ya Mikoa na Halmashauri, Chama cha Walimu Tanzania na Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania.

Jumla ya shilingi 93,322,863,350.00 zilitolewa na kupelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu; Ujenzi wa matundu ya vyoo; Uendeshaji wa shule; Kamati za shule; ufuatiliaji ngazi ya Halmashauri na Kata na kwa ajili kutengeneza madawati.

Hadi Desemba, 2004 shilingi 55,630,512,493.00 zilitumika sawa na asilimia 69 ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, matatizo ambayo kwa kiwango fulani yaliathiri Malengo ya Mpango ni pamoja na:-

- (i) Kuongezeka kwa msongamano madarasani kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi walioandikishwa ikilinganishwa na idadi ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa;
- (ii) Baadhi ya walimu kutotaka kwenda kufundisha katika sehemu nyingine za nchi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya ukosefu wa nyumba za walimu hasa maeneo ya vijijini; na
- (iii) Baadhi ya wananchi kukataa kushiriki kazi za ujenzi kwa kisingizio kuwa Serikali imetoea fedha za kutosha na kuwa michango imefutwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, Mpango umelenga kutekeleza yafuatayo: -

- (i) Kujenga nyumba za walimu 920;
- (ii) Kujenga vyumba vya madarasa 1,792;
- (iii) Kuendelea kutoa fedha za uendeshaji;
- (iv) Kuajiri walimu 7,249;
- (v) Kuandikisha watoto 1,065,843 wenyewe umri wa kwenda shule;
- (vi) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Kamati za Shule, Halmashauri na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- (vii) Kufanya ukaguzi wa mwaka wa mpango na ukaguzi wa mara kwa mara wa matumizi ya fedha ngazi ya shule, Halmashauri na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
- (viii) Kufanya mapitio ya Mpango kulingana na makubaliano na wahisani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Mfuko wa Pamoja wa Afya ulianza mwaka 2000/2001. Mpango unalenga kuboresha na kuinua viwango vya ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuleta hali bora ya afya kwa wananchi.

Mpaka sasa Halmashauri zote zinatekeleza Mpango huu ukiondoa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Maeneo muhimu ya Mpango ni pamoja na:-

- (i) Uboreshaji wa huduma ya uzazi na afya ya mtoto;
- (ii) Uboreshaji wa huduma zinazotolewa katika kudhibiti magonjwa ya kuambukiza;
- (iii) Uboreshaji wa huduma za kinga na tiba dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza;
- (iv) Uboreshaji wa huduma za afya ya jamii na kinga dhidi ya magonjwa; na
- (v) Uimarishaji wa miundo ya kiutawala na uratibu katika ngazi za Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Mpango kwa mwaka 2004/2005 ni pamoja na upatikanaji wa madawa na vifaa katika vituo vya kutolea huduma za Afya kama ilivyopangwa. Aidha, ukarabati mdogo umefanyika katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya zikiwemo Hospitali za Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Maeneo yaliyozingatiwa katika ukarabati hasa ni vyumba vya wazazi, upasuaji, wodi, vyoo, na huduma za maji. Kazi zingine zilizotekelwa ni pamoja na:-

- (i) Ununuzi wa samani na vifaa vya Ofisi za Waganga Wakuu wa Wilaya;

- (ii) Bodi za Afya na Kamati za Vituo vya Afya na Zahanati zimeundwa katika Halmashauri 70;
- (iii) Wananchi wamehamasishwa na kuelimishwa juu ya vita dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, kuzuia malaria na tiba yake, utunzaji wa mazingira, uchimbaji na utumiaji wa vyoo na kudhibiti magonjwa ya milipuko; na
- (iv) Mafunzo mbalimbali yametolewa kwa watumishi wa afya ili kuboresha viwango na stadi katika utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2005/2006, ni kuboresha na kuimarisha ubora wa viwango vya huduma za afya zinazotolewa na Hospitali za Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Halmashauri zinashauriwa zishirikiane na Bodi za Afya zinazoundwa ili kuhakikisha zinasimamia na kufutilia utekelezaji wa Mpango wa uboreshaji wa huduma za afya na kuwashirikisha kikamilifu watoa huduma binafsi na madhehebu ya dini katika kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Ukarabati wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya unatekeleza kutokana na fedha za Serikali, mkopo wa Benki ya Dunia na msaada wa wahisani ambao ni Serikali za Norway, Denmark, Uhlanzi, Ireland Aid na Shirika la Misaada la Ujeruman (GTZ), kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Lengo la mradi ni kuboresha huduma za afya ya Msingi kwa kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya, kununua madawa, samani na vifaa vya hospitali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Wataalam wa kutathmini mahitaji ya ukarabati wa hospitali za Wilaya na kuandaa michoro na miongozo itakayowezesha majengo ya vituo kuwa katika viwango vinavyokubalika katika kutoa huduma za Afya wamepatikana na juhudzi za kumpata Mtaalam wa kufanya tathmini ya vifaa vya hospitali za Wilaya inaendelea;
- (ii) Kazi ya kutafsiri Mwongozo wa usimamizi wa matumizi ya fedha katika lugha ya Kiswahili ambao utatumika kwenye mafunzo ya Kamati imefanyika; na
- (iii) Mwongozo wa upokeaji, utunzaji, utumiaji na utoaji taarifa ya utekelezaji, umeandaliwa. Mafunzo juu ya Mwongozo huo yameendeshwa kwa wasimamizi katika Mikoa 11 na Watendaji Wakuu katika Halmashauri 32 zitakazoanza ukarabati; na
- (iv) Halmashauri 16 zimepelekewa jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, lengo kwa mwaka 2005/2006, ni kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo kwa Watendaji Wakuu wa Halmashauri 40 kuhusu ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Mafunzo haya yatawezesha Watendaji hao kusimamia shughuli za ukarabati na matumizi ya fedha za ukarabati kwa ufasaha zaidi;
- (ii) Kupeleka fedha kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na fedha za kuhamasisha Kamati za Afya;
- (iii) Kuandaa michoro na miongozo ya vituo vya kutolea huduma za afya;
- (iv) Kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri arobaini; na
- (v) Kutathmini mahitaji ya ukarabati wa vifaa vya hospitali.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa, mnamo mwezi Desemba 2004, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Mradi mpya utakaoziwezesha Serikali za Mitaa kupata fedha zaidi kwa matumizi ya shughuli za maendeleo. Mradi huu ambao umezinduliwa rasmi mwezi Aprili 2005, utatekelezwa kutokana na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, mchango wa Serikali Kuu pamoja na Halmashauri husika. Jumla ya Dola za Marekani milioni 60.8 zinatarajiwu kutumika katika kutekeleza shughuli za Mradi hadi utakapomalizika mwaka 2007/2008. Kati ya fedha hizo Dola milioni 52.0 zitatoka Benki ya Dunia, na dola milioni 8.8 ni mchango wa Serikali Kuu pamoja na Halmashauri husika. Mradi huu utahusu maeneo yafuatayo: -

- (i) Utoaji wa ruzuku kwa ajili ya kutekeleza miradi ya miundombinu itakayobuniwa kwa kuwashirikisha wananchi na kuzijengea Halmashauri uwezo wa kutekeleza mradi kwa ufanisi;
- (ii) Kuboresha miundombinu katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa programu ya afya na usafi ngazi ya kaya itakayohusisha mitaa 16 yenye wakazi 180,000 na kuboresha ukusanyaji wa mapato ili kuifanya miundombinu kuwa endelevu. Ili kuonyesha uhitaji, kaya zitatakiwa kuchangia asilimia 5 ya gharama ya mradi unaokusudiwa; na
- (iii) Kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili iweze kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi na kuziwezesha Halmashauri kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia mradi utatoa ruzuku kwa Halmashauri 41 zilizokidhi vigezo vya kupatiwa fedha kama nilivyoolezea katika Hotuba yangu ya mwaka 2004/2005. Halmashauri 25 kati ya hizo zitapata ruzuku kwa ajili ya kutekeleza miradi ya miundombinu pamoja na ruzuku ya kujijengea uwezo wakati Halmashauri 16 zilizobaki zitatengewa ruzuku ili ziweze kujijengea uwezo na kufanikiwa kupata ruzuku ya kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, kazi zilizotekelawa ni pamoja na:-

- (i) Kukamilisha maandalizi ya mradi;
- (ii) Kufanya uzinduzi rasmi wa mradi tarehe 18 Aprili, 2005; na
- (iii) Kupeleka fedha kwenye Halmashauri husika ambapo kiasi cha shilingi bilioni 4.8 zimetolewa kwa Halmashauri 25.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaratibu shughuli zitakazotekelawa na mradi katika Halmashauri 41 ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kuzijengea uwezo Halmashauri 16 ambazo zimeshindwa kufikia vigezo vya mradi na kuzisaidia ili kupata ruzuku ya kujenga miundombinu; ziweze
- (ii) Kuanza ujenzi wa miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam na kuboresha ukusanyaji wa mapato; na
- (iii) Kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili iweze kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi na kuziwezesha Halmashauri kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa majoribio wa Usafiri na Usafirishaji Vijijini uliendelea kutekelezwa katika Halmashauri za Iramba, Muheza, Mbozi, Iringa na Rufiji. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, kazi iliyofanyika ni kutathmini utekelezaji wa mradi na kubaini maeneo yaliyofanya vizuri ili uzoefu huo utumike kuanzisha shughuli za Mradi katika maeneo mapya. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba taarifa ya tathmini hiyo imekamilika na itatumika kama mwongozo wa kupanua mpango huu ili uweze kuzifikia Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya tathmini imeonyesha kuwa, wananchi wameonyesha kupendelea zaidi ujenzi wa miundombinu. Hivyo kwa mwaka 2005/2006 nguvu zaidi zitaelekezwu katika ujenzi wa madaraja, barabara na vivuko vya waendao kwa miguu katika maeneo mapya yenyе uhitaji nchini. Katika kufanikisha azma hiyo mafunzo kwa wataalam wa ujenzi vijijini yatapewa kipaumbele ili kujenga uwezo wa vijiji vyenyewe kuunda miundombinu yao. Utumiaji wa teknolojia ya nguvu kazi katika ujenzi, utahimizwa ili kuendeleza miundombinu na pia kuleta ajira kwa wananchi vijijini. Aidha, wananchi watahamasishwa zaidi katika kuunganisha nguvu na kuanzisha jumuia zao ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Matengenezo ya Barabara uliendelea kupokea mgao wake wa asilimia 30 ya fedha kutoka kwenye Bodi ya Mfuko kwa ajili ya

matengenezo ya barabara za Halmashauri zote. Hadi kufikia mwezi Mei 2005, jumla ya shilingi bilioni 19.02 zimepokelewa na kupelekwa kwenye Halmashauri. Fedha hizi zimetumika na zinaendelea kutumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya kipindi maalum (*periodic maintenance*), matengenezo ya dharura katika sehemu korofî (*spot improvement and emergency repair*), matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*) na shughuli za ufuatiliaji na usimamizi. Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu, jumla ya kilometra 4,736 zilifanyiwa matengenezo mbalimbali kati ya kilometra 11,023 zilizopangwa. Aidha, ukaguzi wa shughuli za barabara kwa mwaka 2004/2005, umeonyesha kwamba Halmashauri nyingi kwa sasa zina nidhamu ya matumizi ya fedha hizo kuliko miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali imeendelea kueneza Mfumo wa *District Road Management System (DROMAS)*, kwenye Halmashauri nyingine 12. Halmashauri hizo ni Morogoro, Rufiji, Kisarawe, Iringa, Mufindi, Mbozi, Muheza, Hai, Moshi, Babati, Sumbawanga na Dodoma. Utekelezaji wa Mfumo huo umeziwezesha Halmashauri 12 za mwanzo kutekeleza Bajeti zao na kutoa taarifa zenye ubora na kuziwasilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Mfuko wa Barabara utaendelea kuzifanya matengenezo barabara za Halmashauri ili ziweze kupidika wakati wote. Serikali ikishirikiana na Benki ya Dunia itafanya zoezi la kutathmini hali ya barabara za Halmashauri ili kuweza kujua urefu wa mtandao wote wa barabara. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kurahisisha upangaji wa mipango yenyе uhakika wa matengenezo ya barabara kwa kuzingatia umuhimu wake. Aidha, Mfumo wa *DROMAS* utatekelezwa katika Halmashauri nyingine 40.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la *NORAD* inafanya maandalizi ya Mpango wa Kitaifa wa Usafiri *National Rural Transport Programme (NRTP)*. Mpango huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai 2005 katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ya matayarisho itakayokuwa ya miaka miwili kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2007 utagharimu shilingi bilioni 13. Katika kipindi chote cha mradi, jumla ya urefu wa km. 15,000 za barabara zitatengenezwa. Madhumuni ya Mpango huu ni:-

- (i) Kufanya uchambuzi wa hali halisi ya mtandao wa barabara za vijijini;
- (ii) Kuboresha miundombinu hasa ya barabara za vijijini; na
- (iii) Kujenga uwezo wa Halmashauri wa kuhudumia miundombinu.

Serikali ya Norway imetenga kiasi cha shilingi bilioni 7 kwa ajili kutekeleza shughuli za Mpango kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Masuala ya Kisekta, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na programu mbalimbali za Kisekta ambazo zinatekelezwa katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Kilimo, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Ushirika na Masoko na wadau wengine, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya kilimo ngazi ya Halmashauri katika Mikoa mitano ambayo utekelezaji wake ulianza mwaka 2003/2004. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Mtwara. Semina za kuwaelimisha Watendaji ngazi za Mikoa na Wilaya zilifanyika kwa ajili ya kuwashirikisha Viongozi na watendaji wa ngazi hizo kufanikisha programu hii ya maendeleo ya kilimo. Halmashauri zilisisitizwa kuandaa programu zake za sekta ya kilimo kwa kushirikisha jamii kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuongeza uzalishaji na kupunguza umaskini. Katika mwaka 2004/2005 jumla ya shilingi bilioni 3.52 kati ya shilingi bilioni 4.0 zilizotengwa zimepelekwa katika Wilaya kutekeleza programu hizo. Katika mwaka 2005/2006, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya maendeleo ya kilimo katika Mikoa na Wilaya zilizo chini ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, Maliasili na Mazingira, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliendelea kutekeleza jukumu lake la kisera la kuhakikisha kuwa suala la kusimamia, kuhifadhi na kutunza mazingira linapewa umuhimu wa kutosha. Katika kutekeleza jukumu hili kwa mwaka 2004/2005 Ofisi yangu ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu wa Programu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misitu Nchini. Mkakati huu ambao hufadhiliwa na Serikali ya Denmark unatekelezwa katika Wilaya 12 za Mikoa ya Morogoro, Iringa, Lindi na Mbeya;
- (ii) Kutayarisha Mwongozo wa Mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu na kuisambaza Mikoani;
- (iii)Kukamilisha Mwongozo wa tathmini ya rasilimali za misitu na kuisambaza Mikoani;
- (iv)Mafunzo ya wiki mbili yalitolewa kwa Maafisa Misitu wa Wilaya 20;
- (v) Kuandaa Mwongozo wa Utawala na Fedha wa Mkakati wa Usimamizi Shirikishi na kuusambaza Mikoani;

- (vi) Mwongozo wa kuzijengea uwezo Sekretariati za Mikoa ulikamilishwa na kusambazwa Mikoani;
- (vii) Hekta 649 za uoto asili zimetengwa na kuhifadhiwa katika Vijiji;
- (viii) Kamati za mazingira na maji 56 zimeundwa;
- (ix) Vyanzo vya maji vimeainishwa na mipango ya matumizi kutayarishwa;
- (x) Miti 2,700,065 imepandwa katika maeneo yenye vyanzo vya maji na asilimia kubwa ikiwa ni miti ya asili;
- (xi) Kuhimiza Halmashauri kutunga Sheria ndogo za mazingira na kuzisimamia;
- (xii) Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira; na
- (xiii) Kuratibu programu ya usimamizi endelevu wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Ofisi yangu itaendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu katika Wilaya 19 pamoja na kufuutilia na kuhakikisha kuwa Halmashauri zinakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi inayojumuisha hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, Mpango huu umekuwa ukitekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Sweden katika Halmashauri za Singida, Babati, Simanjiro na Kiteto kuanzia mwaka 1987. Mkazo mkubwa umewekwa katika maeneo ya uzalishaji mali, mazingira na haki za jamii katika kutumia maliasili zao kupunguza umaskini. Kwa mwaka 2004/2005, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara za Kisikta, imeendelea kuratibu juhudzi za Wahisani, Halmashauri na wananchi katika kufanikisha malengo ya programu hii kwa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya programu hii ni pamoja na:-

- (i) Maendeleo katika shughuli za kuhifadhi wanyama pori;
- (ii) Mabadiliko ya tabia za wananchi na Watendaji katika kuimarisha usimamizi wa maliasili; na
- (iii) Wanawake katika maeneo ya Mradi wanashiriki katika Kamati mbalimbali za maendeleo vijijini.

Katika mwaka 2005/2006, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kufuutilia utekelezaji wa programu hii katika Wilaya husika ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyopatikana yanadumishwa.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Ardhi na Makazi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliendelea kuzielekeza Halmashauri zote nchini kufuutilia suala la ujenzi wa nyumba bora mijini na vijijini katika maeneo yaliyopimwa na yenye usalama. Aidha, kila Halmashauri iliagizwa kutenga fedha kwa ajili ya upimaji wa ardhi ili kuwa na viwanja vya kutosha kwa ajili ya wananchi.

Hivyo, katika mwaka 2005/2006, Ofisi itaendelea kufuutilia na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata viwanja katika maeneo yaliyopimwa ili waweze kujenga nyumba bora na kuweza kutumia hati za viwanja kupata mikopo kutoka katika asasi za fedha. Aidha kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ofisi yangu ilianisha nyumba zilizojengwa katika maeneo yasiyopimwa kwa lengo la kuwapatia wamiliki wake leseni ya ukazi inayoweza kutumika kupata mikopo kwa lengo la kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Ushirika na Masoko, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, imeendelea kuhakikisha kuwa dhana ya ushirika inaendelezwa kwa wananchi. Hivyo, mwaka 2005/2006, Ofisi yangu itaendelea na jukumu lake la kuhamasisha wananchi kuitia Halmashauri ili kuhakikisha kuwa suala la uanzishaji ushirika katika vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali vya wananchi linatiliwa mkazo. Aidha, itashirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko katika kufanikisha matumizi ya stakabadhi za mazao kuwawezesha wakulima kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida, katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya Sh 36,604,007,500.00 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, Mfuko wa Barabara na ruzuku kwa ajili ya Shirika la Elimu Kibaha. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 jumla ya Sh. 27,746,291,068.00 zimepokelewa na zimetumika. Kati ya fedha hizo, Sh.6,430,922,995.69 ziligharamia mishahara na matumizi mengineyo ya Ofisi Kuu na Sh.19,022,743,251.94 zilitumika kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Aidha, Shirika la Elimu Kibaha lilitumia Sh. 1,229,353,121.00 kugharimia mishahara na Sh.1,063,271,700.00 kugharimia matumizi mengineyo. Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya Sh.33,472,943,500.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, Sh. 18,297,669,600.00 ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 15,175,273,900.00 ni kwa ajili ya kugharimia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 Mikoa imepokea jumla ya Sh. 32,057,726,384.00 kwa ajili ya kugharimia mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Miji na Wilaya, Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 386,767,803,300.00 na kati ya fedha hizi Sh. 281,551,099,800.00 ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 105,216,703,500.00 ni kwa ajili ya kugharimia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 Halmashauri zimepokea jumla ya Sh.

370,349,034,791.00 kugharimia matumizi ya kawaida zikiwemo Sh. 258,396,660,291.00 za mishahara na Sh. 111,952,034,500.00 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 141,324,747,200.00 kugharimia utekelezaji wa miradi na programu chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizi Sh. 270,000,000.00 ni fedha za ndani na Sh. 141,054,747,200.00 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 jumla ya Sh. 513,604,059.00 fedha za ndani na Sh. 134,330,956,020.00 fedha za nje zimetolewa na kutumika.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mikoa pamoja na Halmashauri zilitengewa jumla ya Sh. 44,630,627,900.00 kutelekeza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi Sh. 10,771,246,000.00 ni fedha za ndani na Sh. 33,859,381,900.00 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 jumla ya Sh. 10,771,246,000.00 fedha za ndani zimetolewa na kutumika.

Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuwashukuru wananchi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, makundi mbalimbali kwa michango yao ya hali na mali waliyotoa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, natoa shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mabenki na Wahisani mbalimbali waliochangia jitihada za Watanzania za kuleta maendeleo. Mashirika ya Umoja wa Mataifa ni pamoja na *UNCDF, UNDP, UNICEF, ILO, UN Habitat*. Wahisani wengine ni pamoja na Umoja wa nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Serikali za Austria, Canada, Denmark, Finland, Ireland, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Uhlanzi, Uingereza, Ufaransa, Ujerumanu na Uswisi.

Mheshimiwa Spika, bajeti inayowasilishwa leo imeandaliwa kwa ushirikiano wa watumishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Napenda niwashukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, Katibu Mkuu Bwana Deotrephe Mmari, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Asasi na Miradi chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wafanyakazi wote wa Ofisi yangu. Napenda pia kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa Hotuba hii ambayo ameifanya kwa wakati na unadhifu mkubwa. Naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Sh. 206,594,684,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 12,700,937,500.00 ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 40,629,262,100.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kadhalika, jumla ya Sh. 153,264,484,400.00 zinaombwa kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh. 3,300,000,000.00 ni fedha za ndani na Sh. 149,964,484,400.00 ni fedha za nje. Kwa mwaka 2005/2006, Ofisi za Wakuu wa Mikoa

zinaombewa jumla ya Sh. 37,789,603,400.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 20,342,603,400.00 ni kwa ajili ya kulipia mishahara na Sh. 17,447,000,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Vilevile, Mikoa inaombewa jumla ya Sh. 45,907,578,900.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zikiwemo Sh. 6,320,673,200.00 fedha za ndani na Sh. 39,586,905,700.00 fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, Halmashauri za Miji zinaombewa ruzuku ya jumla ya Sh. 91,564,195,300.00 zikiwemo Sh. 60,950,815,900.00 kwa ajili ya mishahara na Sh. 30,613,379,400.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Halmashauri za Miji zinaombewa jumla ya Sh. 885,203,600.00 fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, Halmashauri za Wilaya zinaombewa ruzuku ya jumla ya Sh. 392,586,337,100.00 zikiwemo Sh. 268,862,316,500.00 kwa ajili ya mishahara na Sh. 123,724,020,600.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Halmashauri za Wilaya zinaombewa jumla ya Sh. 4,796,123,200.00 fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, nawasilisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Rais TAMISEMI	Sh. 206,594,684,000.00
Ofisi za Wakuu wa Mikoa	Sh. 83,697,182,300.00
Halmashauri za Miji	Sh. 92,449,398,900.00
Halmashauri za Wilaya	Sh. 397,382,460,300.00
JUMLA	Sh. 780,123,725,500.00

Mheshimiwa Spika, majedwali mbalimbali yamegawiwa pamoja na Hotuba hii ili kutoa ufanuzi zaidi wa masuala yaliyoelezwa na kutoa mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio haya ya Matumizi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2005/2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu inatokea mara moja kila mwaka, labda nikumbushe utaratibu wetu kuhusu makadirio ya kila Wizara. Yametaliwa na Kanuni Na.81 inayosema kwamba Waziri anayehusika na kuwasilisha bajeti yake siku hiyo itakapofika wakati wa kujadili taarifa ya Kamati, Mheshimiwa Waziri atatua hoja kwa maneno yafuatayo kwamba: “Sasa Bunge likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara yangu”.

Sasa yanayofuata, lakini kwa kuwa hotuba yake itakuwa tayari imekwishakuwasilishwa Mezani, muda wake wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi 30. Kwa hiyo, kinachoingia kwenye *Hansard* ni ile hotuba iliyowasilishwa mezani kwa sababu ina maelezo marefu zaidi kuliko muhtasari anaousoma hapa. Inapotokea kwamba kuna tofauti ndogo baina ya aliyosoma na ile iliyowasilishwa mezani kwa mfano ametuambia kwamba kuna Jiji la Tanga halimo kwenye kitabu chake basi masahihisho yatafanywa kwa mawasiliano baina ya Wizara yake na Makatibu Mezani lakini kinachoingia kwenye *Hansard*, kumbukumbu ya kudumu ni kile kitabu mlichogawiwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua makadirio ya Wizara hii.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni. Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa kazi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza huko nyuma nilipokuwa nikiwasilisha Taarifa ya Kamati yangu kuhusu utekelezaji wa kazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006, moja kati ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia bajeti za Wizara ikiwemo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 27, 30-31 Mei, 2005, Kamati yangu ilipitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi, Mbunge, akishirikiana na wataalamu wake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inahusisha Mafungu yafuatayo:-

Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, Dira na Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yameelezwa vema katika kitabu cha maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, cha Mei, 2005 kilichowasilishwa mbele ya Kamati. Kwa muhtasari, Dira ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi kuititia Serikali za Mitaa, inafanikiwa ili kuharakisha maendeleo na kupunguza hali ya umaskini nchini. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mwelekeo wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI umefafanuliwa majukumu ya kisera na kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa jumla, majukumu ya kiutendaji ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni pamoja na kuratibu na kusimamia tawala za Mikoa ili ziweze kusaidia Halmashauri kutekeleza wajibu wao; kuratibu utekelezaji wa sera ya maendeleo vijiji na mkakati wake pamoja na kuboresha miundo ya taaluma ya watumishi na mifumo ya kazi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Halmashauri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuititia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2004/2005, Kamati yangu ilitoa maagizo kumi na tisa. Maagizo hayo yalihu maeneo kadhaa. Nayo ni kuitaka Serikali kuufanya Mfuko wa Pembejeo usimamiwe na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa badala ya Wizara ya Kilimo; kuitaka Ofisi ya Rais TAMISEMI kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa sheria ndogo za Halmashauri hazicheleweshwi kiasi cha kukosa maana zinapokuwa zimesainiwa pamoja na kuitaka Mikoa iongeze usimamizi kwa Halmashauri ili bajeti itekelezwe kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wa kina wa maagizo haya na utekelezaji wake umo katika Kiambatisho Na. 1 katika kitabu cha Maelezo ya Waziri wa Nchi, TAMISEMI nilichokitaja awali.

Kwa jumla maagizo yote yalitekelezwa isipokuwa agizo moja linalohusu Mfuko wa Pembejeo kusimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI badala ya Wizara ya Kilimo.

Pamoja na Kamati kuagiza hivyo, bado imebainika kuwa mfuko huo hausimamiwi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa sababu hiyo, kutokana na umuhimu wa mfuko huo, Kamati kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, bado inaiagiza Serikali ifuatilie suala hili ili kuleta ufanisi zaidi wa uzalishaji katika sekta ya kilimo hususan vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati yangu ilielezwa kuwa kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiutendaji ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri; Kufanikisha ununuvi wa magari ya Wakuu wa Wilaya na magari ya wagonjwa katika baadhi ya vituo vyaa afya nchini na kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi zote na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati iliombwa iidhinishie Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, jumla ya shilingi 781,704,804,400/= zikiwemo shilingi 575,270,335,400/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 206,434,469,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mafungu 56, 70-89 na 95, ombi ambalo Kamati inapendekeza likubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa muhtasari taarifa ya utekelezaji wa kazi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2005/2006, kama ilivyowasilishwa katika Kikao cha Kamati, sasa naomba kuelezea maagizo ya Kamati kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, kwa mwaka wa Fedha 2005/2006 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Kamati yangu inarejea agizo lake la Mwaka wa Fedha wa 2004/2005 kuwa Mfuko wa Pembejeo usimamiwe na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa badala ya Wizara ya Kilimo na Chakula, ili Mfuko huo uweze kuwafikia walengwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mbili, Kamati inaagiza kuwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, izisaidie Halmashauri za Wilaya ziweze kupata vibali vya ajira mpya kutoka Utumishi ili kuziwezesha Halmashauri hizo kupata wataalamu haraka.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kamati inaagiza kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, isaidiane na Halmashauri za Wilaya katika kuhakikisha kuwa sheria ndogo kutoka Halmashauri zinachapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa wakati muafaka. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI izipitie sheria hizo na kuangalia kama hazipingani na Katiba ya nchi na sheria mama na kwamba zinakidhi haja ya Halmashauri za Wilaya au Miji husika.

Mheshimiwa Spika, nne, usimamizi wa Bajeti za Halmashauri. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa isaidie Mikoa katika kusimamia bajeti za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tano, juhudu kubwa zifanywe kuongeza bajeti ya Mikoa ili iweze kutekeleza miradi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, sita, maagizo kwa Mikoa:-

(i)Mtindo mmoja wa uandishi wa vitabu vya Bajeti. Kamati inaagiza kuwa Mikoa iwe na mtindo mmoja wa uandishi wa vitabu vyake unaoendana na mwongozo unaotolewa na vitabu vya Hazina: Kitabu cha Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo.

(ii)Malengo na Mikakati ya Matumizi ya Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework*). Katika kutayarisha bajeti, Mikoa izingatie pia Malengo na Mikakati ya Matumizi ya Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework*).

(iii) Maelezo katika miradi iliyoko kwenye Mpango wa Maendeleo. Miradi iliyoko kwenye Mpango wa Maendeleo iwe na maelezo ya kutosheleza badala ya kuishia na takwimu peke yake.

Mheshimiwa Spika, maagizo maalumu kwa Mikoa:-

(i) Mkoa wa Singida, ushirikiane na Mkoa wa Tabora kuboresha barabara inayounganisha Mkoa wa Tabora na Singida kupitia Itigi.

(ii) Mkoa wa Kagera ufuutilie kwa karibu uchimbaji wa visima vifupi na virefu vijijini ili kutosheleza huduma za maji Mkoani.

(iii) Mkoa wa Dar es Salaam:-

- Mkoa kwa kushirikiana na Serikali ufuutilie kwa makini suala la utozaji fedha za kuegesha magari unaofanywa na wakala au kampuni iliyopewa dhamana hiyo Jijini Dar es Salaam ili kuona kama fedha hizo zinakusanya ipasavyo.

- Miundombinu ya Dar es Salaam hususan barabara iboreshwe na kuimarishwa ili iendane na hali halisi ya ongezeko kubwa la watu na msongamano wa magari. Aidha, barabara zilizoharibika zikarabatiwe.

(iv) Mkoa wa Kilimanjaro:-

- Mkoa usimamie vizuri takwimu za Makisio kwenye Halmashauri ili hesabu zao ziishie mwezi Machi badala ya Desemba

.Mkuu wa Mkoa aongoze majadiliano kati ya Halmashauri na *Tanzania Building Agency (TBA)* kuhusu mgogoro wa uuzaaji wa nyumba zilizojengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali zilizoko Mashati, Rombo ili upatikane muafaka katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, taarifa hii kwa jumla imezingatia maeneo makuu matatu. Kwanza, Dira na Majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pili, taarifa ya utekelezaji ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na maagizo ya Kamati kwa mwaka huo na tatu, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2005/2006 na maagizo ya Kamati kwa mwaka huo wa Fedha. Natumaini kuwa kama yapo maeneo ambayo sikuyagusia, Wajumbe wa Kamati yangu watayazungumzia pindi watakapopata fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipatia fursa hii na Ofisi yako kwa ujumla, kwa kuratibu na kusimamia kwa karibu na hata kufanikisha uchambuzi wa bajeti ya Ofisi hii ambayo sinabudi nikiri kuwa kutokana na uzito wake ilitumia muda mrefu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaaifu), Hassan Ngwilizi (Mb), Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote, kwa maelezo yao ya ushirikiano mkubwa waliouonyesha mbele ya Kamati yangu. Nina hakika kuwa ushirikiano wao kwa sehemu kubwa umewawezesha Wajumbe wa Kamati yangu kufanikisha uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati yangu, kwanza, kwa kutumia muda wao wa ziada kuyasoma kwa kina makabrasha yote yaliyowasilishwa kwenye Kamati ambayo kwa hesabu za haraka haraka kila mjambe alikuwa na vitabu takriban thelathini na tano, vyta Mikoa na TAMISEMI yenye.

Pili, napenda niwashukuru kwa kuonyesha uwezo wa hali ya juu wakati wote wa kuchambua mahesabu ya Ofisi hii, uwezo ambao umejenga mazingira ya uandishi bora wa bajeti za Mikoa na kuboresha bajeti ya TAMISEMI kwa jumla. Wajumbe wa Kamati walioifanya kazi hii ni:-

Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo - Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahoro Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira, Mheshimiwa Dr Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba; Mheshimiwa George F. Mlawa; Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. (*Makofii*)

Mwisho kabisa, napenda niwashukuru, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Athumani Hussein, Makatibu wa Kamati hii, chini ya uongozi wa Bwana Damian Foka, Katibu wa Bunge, kwa kuihudumia vema na kutayarisha Taarifa ya Kamati mapema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, natamka kuwa naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nakumbuka kuna swali lilishaulizwa hapa Bungeni, kwa nini maoni ya Kambi ya Upinzani hayawasilishwi Mezani kama yanavyofanyika maoni ya Kamati.

Swali likajibiwa kwamba tulighafirika tu hatukuliweka kwenye Kanuni lakini tukisema tunaweza kutumia Kanuni ya 31 ambayo inaruhusu hati ziwasilishwe Mezani na Mbunge ye yote asiyekuwa Waziri.

Bahati mbaya *Order Paper* ya leo haikuonyesha hivyo lakini naomba Kambi ya Upinzani ijue kwamba kwa Wizara zote zinazokuja basi msemaji wa Wizara hiyo atawasilisha Mezani asubuhi maoni ya Kambi halafu ndio atayawasilisha kwa mdomo baadaye. Kwa leo haikufanyika lakini namwomba basi msemaji wa kambi ya upinzani kwa sekta hii awasilishe maoni ya kambi yake. (*Makofî*)

MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. DR. AMANI W.A KABOIROU – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuchukua fursa hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na Bajeti ya Taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge, kifungu 43(5)(b) na (c).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kumpoteza mwakilishi wao, Mheshimiwa Kiwanga. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuipongeza kama mfano na mafanikio yaliyopatikana katika Majimbo na Halmashauri ambazo ziko chini ya Vyama vya Upinzani katika kipindi hiki cha miaka mitano. Mifano hai iko mingi kwa yule mwenye macho ya kuona na masikio ya kusikia asiyetaka kuona hatuna namna ya kumfanya ila wananchi husika ndio watakaokuwa Mahakimu. (*Makofî*)

Kama inavyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ibara ya 45 na 46 kuwa kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mkoa na Wilaya, miji na vijiji ambavyo vitakuwa na jukumu la kuleta maendeleo katika sehemu husika kwa kushirikisha wananchi. Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndio yenye jukumu la kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili ziweze kuzisaidia Halmashauri katika kutekeleza wajibu na majukumu yake na kutayarisha na kusimamia sera za maendeleo vijijini na kuboresha miundo mbinu, hali ya Watumishi na mifumo ya kazi na kusimamia shughuli zote zinazoendeshwa kwa shughuli za Serikali katika ngazi hizo. Haya ni majukumu makubwa na mazito.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake, inatakiwa kuwa na bajeti kubwa sawa na ya Serikali Kuu yenyewe. Kwa bahati mbaya Wizara hii imepawa bajeti ndogo sana ambayo haina uwiano na shughuli zinazofanywa. Pamoja na bajeti kuwa ndogo, Wizara hii na hasa Halmashauri huwa hazipati fedha kwa wakati ili kutekeleza majukumu yake kwa kadri ya ratiba ya utekelezaji waliojipangia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Wizara hii pamoja na sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya bajeti za kutosha yenyewe

uwiano sawia ili ziweze kutekeleza majukumu makubwa waliyonayo katika ngazi hizo za Serikali.

Kambi ya Upinzani inatamka wazi kuwa Serikali Kuu bado inaingilia Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Katiba haiko wazi kuhusu Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Halmashauri za Wilaya zimebanwa hazina uhuru wa kutosha na zinaingiliwa na watawala kutoka Serikali Kuu. Wakuu wa Wilaya wanaingilia utendaji wa Halmashauri za Wilaya na kudhoofisha demokrasia.

Kama suluhisho la muda mrefu na la kudumu kwa manufaa ya mustakabali wa Taifa, ni vema cheo cha Mkuu wa Wilaya kikafutwa na kazi zote za Ofisi ya Mkuu wa Wilaya zikajumuishwa na kazi za Mkurugenzi wa Halmashauri. (*Makofi*)

Halmashauri za Wilaya zipewe mamlaka na uhuru zaidi. Mikoa ya sasa inapaswa kuunganishwa kuwa michache kuwezesha ufanisi wa kazi na pia kuleta ushindani wa kiuchumi mionganoni mwa Mikoa ndani ya nchi. Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza gharama nyingi zinazotumika katika ngazi hizo badala ya kuelekeza moja kwa moja kwenye ngazi husika ambapo ndiko kuliko na sehemu kubwa ya Watanzania wa kawaida na maskini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, sasa narejea kwenye hotuba ya makadirio iliyowasisilishwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, sera na mkakati wa maendeleo Vijijini. Elimu kwa umma, juu ya mkakati wa maendeleo vijijini haijatolewa kwa upana kama ilivyoahidiwa, matokeo yake kama mikakati mingine mkakati huu umeishia kwenye makabati ya Ofisi za Serikali na kuwa nyumba za buibui. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mkakati ulio wazi wa kutoa elimu hii.

Mathalani semina iliyofanyika Dodoma mwaka 2001 na kuhuduriwa na Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya, imeishia bila kushuka chini na hivyo kuwa pato la wakubwa bila kuwanufaisha wananchi wa kawaida katika vijiji vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Mfumo huu kinadharia unalenga kutoa madaraka kwa wananchi wa ngazi za chini na kupanga, kusimamia, kutekeleza na kutathmini shughuli za maendeleo katika maeneo yetu.

Lakini taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa wananchi wengi bado hawajanufaishwa na mfumo huu. Kimsingi, Halmashauri nyingi zilitakiwa ziwe zimeshanufaika na mpango huu.

Mpango wa uboreshaji unaoendelea unaonekana kuendelea bila kuwa na mwisho na bila kuwa na matokeo ya moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida japo fedha nyingi sana zinatumika katika mpango wa maboresho.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ratiba iliyo wazi ya utekelezaji wa mpango wa maboresho. Tungependa Wizara ilifahamishe Taifa ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa mpango huu, kazi gani hasa zinatakiwa kufanywa na hadi sasa zimetumika fedha kiasi gani kwa mpango wa maboresho.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona bado kuna mapungufu makubwa katika mifuko ya wanawake na vijana. Matokeo yake ni kwamba Halmashauri nyingi zimeonekana kurudisha sehemu kubwa ya fedha bila kuwapatia walengwa au walengwa hao kunufaika na mikopo hiyo. Mikopo iliyotoka sehemu nyingi imetolewa kinyemela na sehemu nyingine kisiasa bila utaratibu unaojulikana. (*Makofî*)

Kwa vile hakuna mafunzo ya kina yanayotolewa kabla ya kukopeshwa, vikundi vya wanawake na vijana wengi wameshindwa pia kurejesha na wameichukulia mikopo hiyo kama hisani au fadhila. Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Wizara husika itoe mwongozo na maelezo ya wazi ili mifuko hii iweze kunufaisha sehemu kubwa ya Watanzania bila ya mizengwe ya aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo yote, Kambi ya Upinzani ikishanda uchaguzi mwaka 2005 itafanya yafuatayo:-

- Mikopo itatolewa kwa uwazi zaidi. (*Makofî*)
- Taarifa za mwito za kuchukua mikopo zitatoka katika vyombo vya habari kwa wingi kama ambavyo taarifa za zabuni na kwa upande wa wananchi ambao hawafikiwi na vyombo vya habari njia zao za asili zitatumika. (*Makofî*)
- Kwa kuwa mikopo inayotolewa ni kidogo sana na haikidhi mahitaji ya uzalishaji wa miradi ya uzalishaji mali inayojitosheleza, hivyo katika mwaka wa kwanza madarakani tutafakari na kupanga upya viwango vya fedha vinavyotolewa kama mikopo ya wanawake na vijana, mifuko hii itaundwa kwa sheria badala ya maelekezo ya kiutawala ili iweze kutekelezwa kikamilifu.

Sasa hivi kuna mchanganyiko kwani wapo wanaosema mifuko hiyo muda wake umeisha kutoka na tamko la *ALART*. Tunaitaka Serikali itoe ufafanuzi wa kina kuhusu kauli hizi zenye kuleta utata. (*Makofî*)

- Ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na uendeshaji wa miradi kwa wanawake na vijana wanaopewa mikopo, umewapelekea wengi kushindwa kuirejesha kutokana na miradi hiyo kusuasua.

Kambi ya Upinzani ikichukua madaraka ya nchi itahakikisha kwamba utoaji wa mikopo utakwenda sambamba na upewaji wa elimu ya ujasiriamali na uendeshwaji wa miradi kwa wanufaika. Itabidi Serikali tuviwezeshe kifedha na kiufundi vikundi vya kuweka na kukopa pamoja na asasi zisizo za Kiserikali ziweze kusaidia katika kutekeleza lengo hili. (*Makofî*)

- Inasikitisha kwamba kwa kisingizio cha kutingwa na shughuli nyingi za maendeleo, Halmashauri nyingi zimeshindwa kufikia lengo la kuchangia 10% ya bajeti kwenye mfuko wake wa wanawake na vijana. Halmashauri inapaswa kuelewa kwa vitendo kwamba ukosefu wa mitaji ni chanzo kikuu cha wanawake na vijana kushindwa kujiajiri na hivyo kutopea katika lindi la umaskini.

Hivyo tunatarajia katika mwaka wa kwanza wa fedha wa 2005/2006, tukiwa madarakani, Halmashauri zitatimiza ahadi zake. (*Makofii*)

Tunatarajia pia katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itawasilisha pendekezo la kuongeza asilimia ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana katika bajeti ya Serikali Kuu na pia kuweka kiwango maalum katika bajeti za Halmashauri kwa nia ya kusaidia kuondoa umaskini kwa vitendo badala ya kuwa na hotuba nzuri kila mara lakini katika utekelezaji kunakuwa na mafungu madogo yasiyotosheleza kabisa. (*Makofii*)

Bado Ofisi za Wabunge hazihudumiwi ipasavyo kama ilivyoahidiwa hivyo tuingiapo Ikulu Serikali itatafakari upya utaratibu unaotumika katika mwaka wa fedha 2005/2006 tutahakikisha tunafanya mukutano kati ya Wabunge na wadau mbalimbali wanaohusika na suala hili ili kubuni muafaka zaidi wa kuhakikisha Wabunge wanakuwa na ofisi zinazowastahili. Kuwepo kwa ofisi za Wabunge zinazostaili ni kiungo muhimu cha kuleta demokrasia na maendeo katika mikoa na wilaya. Aidha Ofisi za Wabunge zinapaaswa kuwa karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, maslahi kwa Madiwani bado ni duni hali ambayo imechangia kushindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na wengine kujiingiza katika ufisadi wakati wa mchakato mzima wa tenda.

Kambi ya Upinzani iingiapo madarakani Novemba 2005 itafanya yafuatayo:

Masurufu ya madiwani yataongezwa ikiwemo kutafakari kuwapa mshahara wa kila mwezi unaojitosheleza katika bajeti ya mwaka 2005/2006 kiwango kilichopendekezw ahakitoshi, hivyo lazima bajeti hii huko mbele tutaifakari upya.

Madiwani hawatatozwa kodi wanaopoingiza vifaa vinavyowasaidia katika kutekeleza majukumu yao ya msingi hususani usafiri. Aidha wenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijijini itabidi tuwaingize katika utaratibu wa kulipwa chochote kwani ndio wahimili wa mipango yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ofisi na Nyumba za watendaji wakuu katika wilaya na Mikoa. Hali ya Ofisi na Nyumba za Watendaji Wakuu katika Wilaya na Mikoa bado ni mbaya, tunaamini sasa tuthmini imekwisha fanyika ya kutosha na pesa ambazo zikekuwa zikikusanywa miaka ya fedha iliyopita kimefikia kiwango cha kuridhisha. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali yetu mpya itaanza ukarabati. Tutachukua fursa hii kutoa angalizo kwa Serikali inayomalizia kipindi chake isiendelee kuza nyumba hizi. Angalizo letu hili limesukumwa na uamuzi wa kifujaji wa Serikali Kuu

kuuza nyumba za walipa kodi kwa watendaji wake kwa bei za kutupa na hivyo kuleta adha kwa watendaji wapya kwa upande mmoja na shauku ya watendaji wa TAMISEMI kutaka nao kuuziwa nyumba hizo kwa upande mwininge.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Sekretariati za mikoa. Kuwepo kwa migongano ya kisheria katika utekelezaji wa majukumu ya Sekretariati za mikoa bado kunaendelea na kukwaza ufanisi wa shughuli za maendeleo. Kambi ya Upinzani inaona ipo haya ya muswada wa mabadiliko ya sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 kuletwa Bungeni mapema katika mwaka wa fedha 2005/06 kwa lengo la kufanya marejeo na marekebisho makubwa, ni dhahiri kuwa nia na lengo lililikusudiwa la kufanya marekebisho muundo wa Mikoa kupitia sheria Na. 19 halikufanikiwa.

Badala ya kupunguza idadi ya Watumishi katika ngazi hiyo na kuimarisha ngazi ya Wilaya sehemu nyingi nia hiyo imezungukwa na wataalamu waliotegemewa kwenda Wilayani hawakwenda, na ngazi za uwajibikaji hadi sasa kwa Wizara nyingine imebaki kuwa kiini macho. Sekretariati zimebakni majikumu ya ushauri lakini hawana nyenzo za kutosha na wala hawana nyenzo za usafiri kufika kwenye Wilaya husika. Kwa kiwango kikubwa Mkoa bado ni gharama kubwa kwa taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Demokrasia na Urawala Bora ndani ya vijiji. Tunapongeza uamuzi wa Serikali kutenga fungu kwa ajili ya kupanua demokrasia na utawala Bora ndani ya vijiji ikiwemo kwa kuwafundisha watendaji na kuongeza ushiriki wa wanavijiji. Tunapongeza Serikali pia kwa kuchukua jukumu la kuwalipa mishahara watendaji wa Vijiji. Hata hivyo uzoefu katika mpango wa MMEM unaonyesha kwamba ni asillimia 40 tu ya pesa zinazolengwa huwafikia walengwa. Asilimia 60 zinapotelea njiani kutokana na ujisadi na ufujaji. Tunawahakikisha Watanzania kwamba Serikali itakayoundwa ya Upinzani itahakikisha fedha zote zinawafikia walengwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Uchaguzi wa Mitaa uliofanyika Novemba 2004 ulileta aibu kwa Taifa na mzaha kwa demokrasia. Katika hotuba yake ya bajeti iliyopita Waziri anayehusika alifafanua kwamba Wizara yake haisimamii uchaguzi huu kwani inawajibu wa kuandaa kanuni tu. Alifafanua zaidi kwamba uchaguzi unaendeshwa na Serikali za Mitaa zenyewe. Lakini kilichotokea ni tofauti. Mosi, kanuni zilisainiwa na Rais kwa nafasi yake na hivyo kukinzana na matakwa ya Sheria. Hii inafanya kuwe na hoja kwamba uchaguzi ulikuwa batili tangu mwanzoni. (*Makofî*)

Pili, TAMISEMI ilitaka daftari la wakazi litumike wakati wapinzani tulitaka daftari la kudumu litumike matokeo yake Mahakama ikakubali pingamizi la upinzani kuwa madaftari ya wakazi yasitumike ingawa hata daftari la kudumu halikutumika.

Tatu, kutokuwa na daftari kulichangia uchaguzi kwenda hovyohovyo. Muda mrefu ulitumika katika uorodhesajji, wa nanchi wengi walishindwa kujitokeza kupiga kura kutokana na ugumu wa zoezi la kujirodhesha na vurugu zilizokuwa ikiendelea na kuna taarifa za matukio ya kuvurugwa kwa uchaguzi.

Nne, taarifa za matokeo zimekuwa zikitolewa nusu nusu na pengine mpaka sasa chaguzi zinaendelea kurudiwa. Wasimamizi na wasimamizi wasaidizi alifanya walivyotaka, na hivyo kufanya uchaguzi kuendeshwa bila hata kutumia kanuni zenyewe ambazo Serikali ilitoa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inawasilisha hoja zifuatazo:-

Serikali ikiri kwa ukamilifu zaidi kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulikwenda hovyohovyo na hivyo kuhatarisha demokrasia na amani katika mchakato wake mzima. Japo Serikali imeitoa matamko ya kuwa uchaguzi umeenda kwa amani na utulivu lakini hali halisi ni kinyume na yalyotendeka ni kinyume kabisa na demokrasia katika maeneo mengi. Afichaye ugonjwa kifo kiakuja kumwumbua. Ni vema Serikali ikakubali kufanya tathmini ya kina ya matukio mbalimbali badala ya kung'ang'ania kuwa uchaguzi hui ulienda kwa taratibu sahihi.

Tunarejea tena kusikisitiza kwamba daftari la kidumu la wapiga kura litumike katika chaguzi zote nchini ukiwemo uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kwa kuwa imedhihirika wazi kwamba TAMISEMI na Serikali za Mitaa havina miundo na mifumo muafaka kwa ajili ya kuendesha uchaguzi, kuanzia mwaka wa fedha 2005/06 Serikali ya Upinzani itaanzisha mchakato wa kuhamisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutoka TAMISEMI na Serikali za Mitaa kwenda kuwa chini ya Tume ya Uchaguzi, kuanzia chaguzi ndogo zinazoendelea sasa katika ngazi ya serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Serikali za Mitaa. Bado kuna upungufu mkubwa wa mapato ya Serikali za Mitaa kutohana na kodi za maendeleo kufutwa. Fedha za fidia zinazotolewa na Serikali Kuu hazifikii viwango vilivyokuwa vinakusanywa na Halmashauri nydingi na hivyo huduma katika maeneo hayo zimeathirika kwa kiwango kikubwa. Kambi ya Upinzani inawasilisha hoja zifuatazo:

Wizara za Serikali Kuu zinapewa sehemu kubwa sana ya bajeti ya Serikali kuliko Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali mpya ya Upinzani itaanza mchakato wa kuongeza bajeti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwemo kutafakari kuridhia mfumo unaotumiwa na nchi mbalimbali ambapo mbili ya tatu (2/3) ya bajeti inakwenda katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mfumo wa kuzipatia Serikali za Mitaa vyanzo vingine vya mapato utatekelezwa kama suala la haraka.

Serikali yetu itafanya haraka mpango wa kuhuishwa mfumo wa kodi kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Kwa hivi sasa serikli za Mitaa zimeachiwa vianzio vichache sana na hivyo kunyima kufanya yale mambo ambayo yangeliweza kufanywa na Serikali hizo kwa mamlaka yake na nydingine kulimbikiza madeni makubwa ambayo mwisho wake utakuwa ni kupelekwa mahakamani.

Ushuru uliofutwa bado unaleta tata katika maeneo mengi. Sehemu nyingi ushuru uliofutwa bado unakusanywa na Halmashauri za Wilaya, hata pale unapokusanywa kazi zake pia hazionekani, mathalani hapa Dodoma pamoja na ushuru unaokusanywa katika vituo vya Mabasi hali ya Stendi ni mbaya sana. Hii pia inaonekana katika kituo cha mabasi cha Mwenge Jijini Dar es Salaam. Ushuru ukikusanywa unatakiwa ulenge katika kuborsha huduma na si vinginevyo. Tungependa Serikali itoe Tamko kuhusu aina ya Ushuru unaotakiwa kutozwa kwani suala hili bado linaleta utata mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Hesabu za Halmashauri nasikitisha kuona kwamba bado kuna halmashauri zinapata hati za ukaguzi ambazo haziridhishi na nyingine zinapata hati chafu kabisa katika nchi yetu. Miaka yote, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu anaendelea kulalamikia hali ya matumizi ya Fedha katika Halmashauri zetu mbalimbali.

Kambi ya Upinzani inatoa kauli ifuatayo:-

Kuanzia siku tutakapoingia madarakani ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali itakuwa ikiwasilishwa kwa Spika wa Bunge kama ilivyo katika nchi zingine za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) badala ya kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais ili hatimaye iweze kujadiliwa na Bunge na Bunge kuelekeza hatua za kuchukua badala ya kutoa tu ushauri kama ilivyo sasa.

Suala la uchafu na usafi wa hati za hesabu za Halmashauri si mchezo wa kukosoana na kupongezana tu kwani linahusisha pesa za walipa kodi na sheria za nchi. Serikali ya sasa itoe ripoti kamili ni hatua gani zimechukuliwa kwa wote waliohusika na mapungufu yaliyojitokeza katika hesabu za Halmashauri katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Haiwezekani mabilioni ya fedha ya wananchi yapotee hivihivi hakuna kinachofanyika au hakuna kesi iliyofikishwa Mahakamani ikaffia mwisho wake. Isitoshe kesi zote za Serikali zinashindwa kwa vile ushahidi muhimu haufikishwi Mahakamani au watendaji wanalindana katika kesi hizo kwa vile watendaji ndio watoa ushahidi wakubwa.

Serikali ni lazima ichukue hatua kali na kutoa taarifa haraka kwa Bunge kuhusu hatua inayochukua kwa watu hawa, kwani wakati tunaenda kukopa mabilioni ya fedha, mabilioni mengine yanapotelea katika njia za ajabu na wanaohusika wanaachwa wakidunda tu. (*Makofî*)

Mfumo wa kompyuta wa mahesabu ya halmashauri (*EPICAL*) unaongeza mapungufu ya ripoti kwa kutofautiana mara kwa mara na Kanuni za awali. Hivyo tuingiapo madarakani mfumo huu wa kompyuta utaboreshwu ikiwemo kutoa tenda ya wazi ya kutengeneza mfumo wa kompyuta (*computer software*) wa mahesabu ya Serikali za Mitaa.

Asasi na miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa pamoja na nia nzuri ya uboreshaji wa Serikali

za Mitaa na jitihada za Serikali na wadau wengine katika kutekeleza mradi huu bado mafanikio yaliyotarajiwa hayajafikiwa. Kambi ya Upinzani inawasilisha hoja zifuatazo:-

Wananchi wakitupa ridhaa ya ya kuongoza Serikali, Oktoba 30 uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa utaenda sambamba na kuzipa mamlaka ya kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maandalizi ya Bajeti ya taifa kuanzia awali katika ngazi ya chini kabisa. Halmashauri zitapewa fursa ya kutathmini na kuingiza vipaumbele vyao tangu awali. Kwa kuititia vipaumbele vyao ndipo vipaumbele vyta Serikali Kuu kama afya ya msingi, elimu na maji vitatekelezwa kikamilifu.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006 kuna haya ya kufanya tathmini kuhusu matokeo ya fedha na ruzuku ambazo zimetolewa kwa halmashauri mpaka sasa. Wizara haijatekeleza ahadi yake ya kutoa mafunzo kwa Wabunge kuhusu programu ya uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Serikali yetu mpya itatekeleza jambo hili kwa vitendo katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Kuna haja ya kufanya tathmini na marejeo katika mwaka wa fedha 2005/2006 kuhusu majukumu na mamlaka ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya ili kuyawianisha kwani kumekuwa kukitokea misuguano baina yao katika Wilaya mbalimbali na hivyo kukwaza mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Pamoja na nia nzuri ya mradi wa MMEM matokeo yake yamekuwa mazuri kwa idadi (*quantity*) badala ya ubora (*quality*). Hii imechangiwa na watendaji wengi kuutazama mradi huu kama zana ya kisiasa badala ya chanzo cha ustawi wa vijana wa Tanzania. Kambi ya Upinzani inawasilisha hoja zifuatazo:-

Tuingiapo madarakani Serikali italitazama kwa kina na kuchukua hatua za haraka kuhusu msongamano uliopo katika mashule. Katika hali ya sasa ubora wa elimu upo kitanzini iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa. Walimu wengi pia wamezidiwa kazi. Mahali pengine darasa sasa lina wanafunzi 100 badala ya 40 walimu hawana nyumba za kutosha na hakuna mikakati iliyowazi kunusuru hali hii.

Mfumo wa zima moto wa uandaaji wa walimu kwa muda mfupi na kuwasambaza kufundisha unatengeneza bomu la wakati. Mwaka wa fedha 2005/2006 lazima ulenge kutoa mafunzo kamili kwa walimu la sivyo tutarejea makosa tuliyofanya huko nyuma.

Hatuna tatizo na hatua ya dharura iliyochukuliwa lakini ni lazima kuwekwe mkakati unaoeleweka wa kunusuru hali hii. Kuna malalamiko ya matumizi mabaya ya fedha za MMEM. Ripoti za TAKURU, Haki Elimu na wadau wengine zinataja rushwa, ujisadi na ufujaji ambao umepunguza ubora wa majengo ambao umepunguza ubora wa majengo na vitende kazi pamoja na fedha kushindwa kufika ka walengwa katika kiasi kinachostahili. Serikali tunaitaka itoe taarifa kuhusu tuhuma hizi mapema iwezekanavyo kinga ni bora kuliko tiba.(*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa hadharani taarifa ya tathmini mbili zilizofanywa na Timu ya wataalam iliyoongozwa na mwingereza Bwana Alen Peny kuhusu MMEM. Taarifa tuliyonayo kutokana na taarifa isiyo rasmi ni kuwa fedha nyingi zimetumika vibaya sehemu kadhaa ya nchi yetu. Wakati wa majumuisho kambi ya Upinzani ingelipenda kupata taarifa rasmi ni viongozi wa ngazi katika ngazi mbalimbali za elimu wakiwemo Maafisa Elimu, Wakurugenzi watendaji wa Wilaya, walimu wakuu wa shule na hata Kamati za shule waliohusika na kashfa hizo. kambi ya Upinzani ingelipenda kujua pia ni hatua gani zimechukuliwa kuziba mapengo yaliyotokea katika mfumo huo, ambao kimsingi ni mzuri lakini umekosa maelekezo sahihi.

Kambi ya Upinzani inadhani katika sehemu nyingi mkataba ambao Serikali yetu na *IDA* haukutekelezwa kikamilifu ni jambo ambalo linaweza kuchafua jina la Serikali na nchi yetu mbele ya macho ya Jumuiya ya Kimataifa. Ni vema kukinga kuliko kutibu.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa Masuala ya Kisekta, kambi ya Upinzani inawaahidi Watanzania kuwa masuala yafuatayo ya Kisekta yatazingatiwa zaidi tuingiapo madarakani. Maendeleo ya kilimo, utekelezaji wa programu ya maendeleo ya kilimo utahusisha utoaji wa motisha katika sekta ya usindikaji wa mazao ya kilimo. Halmashauri za Wilaya zitawezeshwa kuweka mazingira ya uwekezaji katika usindikaji wa mazao yapatikanayo ndani ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho baada ya kutoa maoni hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuchukua tena nafasi kutoa shukrani za dhati kwako binafsi kwa kunipa nafasi hii. natoa pia shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Brig. Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mbunge, Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge na Ndugu Mmari Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii muhimu na ngumu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Brig. Gen Hassan Ngwilizi.

Kwanza kabla ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake nzuri aliowasilisha Bungeni hivi leo.

Mheshimiwa Spika, nitatoa sababu kwa nini nasema hivyo kwa sababu yapo mambo ambayo yamesemwa na wenzetu wa Upinzani lakini maelezo tunayo na kama wamesoma hii taarifa, maelezo yote yamo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwanza kwa ruksa yako nitoe pongezi za dhati kwa Rais wetu Mheshimiwa Benjmini William Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote akiwa Rais wa nchi yetu. Nataka pia nimpongeze Makamu

wetu Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye amekuwa ni msaidizi wake mkuu. Wakati huo huo nimpungeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alitoa taarifa yake nzuri ya miaka 10 aliilotumikia nchi hii. Kwa kweli ilikuwa ni taarifa nzuri na mimi nampongeza kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote hicho.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani ni vizuri nikatumia nafasi hii kumpungeza pia kwa niaba ya wenzangu wa Bunge nimpungeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri Ndugu yetu Pinda kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote. Mheshimiwa Waziri lazima nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge ya kwamba kati ya Manaibu waliokuwa wakijibu maswali vizuri Bungeni. Mheshimiwa huyu Pinda alikuwa mmojawapo. Amekuwakilisha vizuri wakati wote ulipokuwa haupo alijibu kwa ufasaha, kwa utulivu na ufahamu kabisa wa masuala yote. Hivyo usiwe na wasiwasi kabisa ulikuwa na Naibu wako mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii kumpungeza Katibu wako Mkuu Ndugu Mmari, ambaye amekuwa msimamizi mkuu wa shughuli katika Wizara yako. Mmari amekuwa pia ni Katibu Mkuu ambaye kwa kweli amejitokeza kuwa ni Mtumishi hodari amefanya kazi yake vizuri na ninashukuru Rais alipomwongezee muda ili aendelee kukusaidia alifanya kazi kwa kujua ni kiongozi anayefaa kufanya hivyo napenda nimshukuru kwa hilo. (*Makofi*)

Watumbishi wote wa Wizara wamefanya kazi yao vizuri nawapongeza. Sasa labda nitumie nafasi hii pia kwa sababu bila wasaidizi wako mikoani usingeweza kufanya kazi yako vizuri. Niwapongeze Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote. Iko dhana ya kudhani kazi ya Mkuu wa Mkoo au Mkuu wa Wilaya haina faida katika nchi hii. Lakini wanaosema hivyo ni wale ambao hawajawahi kupata fikra ya kujua nini wajibu wa Mkuu wa Mkoo na Mkuu wa Wilaya. Hakuna kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi kwa hali hii tuliyonayo, kama nafasi ya Mkuu wa Mkoo na Mkuu wa Wilaya. Msione utulivu tulionao katika nchi hii wanafanya kazi usiku na mchana Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiwaachia Watendaji peke yao nchi inaweza kushindwa kutawalika. Ndiyo maana Rais anapoteua Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa ni kwa ajili ya kumsaidia ili angalau kurekebisha baadhi ya matatizo ambayo yanawenza kujitokeza katika maeneo yao. Sasa umuhimu wao mimi nasema Rais wala asibabaike aendelee kuwateua hata huyu atakayekuwa aendelee kuwateua wawepo tunawahitaji katika nchi yetu. Pia nisipe nikasahau. Nitumie nafasi hii kumtakia kheri, baraka na mafanikio katika uchaguzi ujao Mheshimiwa Rais mtarajiwa, Mheshimiwa Col. Jakaya Kikwete na mgombea mwenza Dr. Ali Mohamed Shein na pia Rais wetu wa Zanzibar. Nina imani kabisa hao ndiyo watakuwa Marais wa nchi hii hakuna mwingine. (*Makofi*)

Sasa baada ya kusema hivyo, rambirambi nimekwisha zitoa katika kikao cha mwanzo. Nilipokuwa nasikia maoni ya wenzetu upande wa upinzani sikuelewa kama walipata nafasi ya kupitia kitabu chote hiki. Tatizo unapoandika hotuba bila kujua mwenzako ameandika nini unaweza kuja na vitu vya ajabu ambavyo majibu yake yapo

tayari, walipokuwa wanatoa maoni na mimi nilikuwa napitia haraka sana kitabu hili, yote yaliyozungumzwa yamo humu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala zima ambalo linashughulikia mambo ya mikopo ya Serikali za Mitaa, kuimarisha mifuko ya Mikopo ya Akina Mama, kuandaa mipango ya kutumia vizuri Watendaji, kuimarisha Utawala Bora, ukiangalia yote ya mfuko wa Akina Mama na Vijana namna utakavyoongezwa, kuboresha Muundo wa Serikali, Demokrasia na Utawala Bora katika Vijiji, Uchaguzi wa Serikali na ushauri uliotolewa yote hamo humu sijui tulikuwa tunazungumza nini.

Mheshimiwa Spika, Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri atarahisishiwa kujibu haya kama utatumia kitabu chake mwenyewe ili isionekane umeongeza mengine lakini mengi ni ushauri na hii ndiyo Ilani ya Uchaguzi yote yanayozungumzia ndiyo ilani ya uchaguzi. Tunaanza kuitekeleza na tutaitekeleza kwa nguvu zote.

Sasa baada ya kusema hayo Mimi nitumie nafasi kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikalli kwa ujumla kwa kuturuhusu angalau sasa mji wetu wa Sumbawanga kupata hadhi ya Manispaa. Tumepewa hadhi ya Manispaa kwa sababu si ya kupendelewa kwa sababu tuna kila haki ya kupata na nitatoa sababu tatu kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako, Mji wa Sumbawanga ni kati ya miji mitatu ambayo ilipewa hadhi ya kuwa miji misafi katika Tanzania, Sumbawanga ikiwemo. Sumbawanga kwa taarifa yako ni kati ya miji ambayo kwa kipindi kirefu Halmashauri zetu za Wilaya zilifanya tathmini na kupitia Wizara ya Elimu shule bora zilizofanya vizuri. Shule za msingi, shule bora zilitoka Sumbawanga. *The best three* kati ya shule zote zaidi ya 10,000 katika Tanzania, zilitoka Sumbawanga, katika Tanzania si katika Mkoa wa Rukwa.

Lakini Sekondari bora *10 best* zimetoka Sumbawanga. Sasa Kantalamba ilikuwa mojawapo imetoka katika Mkao wetu ni mji ambao kwa kweli unastahili kila aina ya sifa na Manispaa sasa tumepata mtaona sasa tutakavyoruka, tutakuwa *the best acha mambo* ya kilimo ambayo kilimo sasa *we are the best one now* tulikuwa *among the best* kati ya mikoa minne lakini sasa tunaongoza sasa tutapaa. Safari hii ukisikia Rukwa inaruka itaruka kweli katika misingi hiyo chini ya uongozi wa Mheshimiwa wetu Luteni Mstaafu ambaye kwa bahati nzuri yuko hapa. Ninadhani wengi mniamfahamu kwa sababu ni mchapa kazi wa siku nyingi, Mkuchika wengi tunamfahamu. Ametufanya kazi nzuri na mimi nataka nimpongeze kwa dhati amefanya kazi nzuri katika mkoa wetu tuna imani kabisa tutaendelea kushirikiana naye kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Sasa nilikuwa na mambo matatu ya kuomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Ukiishapata hadhi ya Manispaa lazima na mazingira yabadilike, nilitaka niiombe Serikali kama haikuweka kwenye Bajeti basi ione umuhimu wa Manispaa na mambo makubwa matatu yanayotakiwa.

Kwanza ni suala zima la miundombinu, tukianza na barabara. Barabara za Mji wa Sumbawanga licha ya *main road* peke yake ambayo kwa kweli ina lami kabisa kilomita chache lakini za Mjini kuzunguka Mji wa Sumbawanga hakuna hata nusu kilomita ambayo ina lami. Sasa hadhi ya Manispaa kwa kweli inaendana pamoja na barabara kuwa nzuri, tungeomba Serikali ione uwezekano kutupa upendeleo maaluma katika kipindi hiki angalau tupate angalau tupate hata kilomita mbili au tatu zisambaze katika maeneo ambayo ni korofsi pale mjini katikati sokoni, tukienda kule Majengo, tukienda kule Kizwite, tufike Sumbawanga wenyeji, Izia sehemu zote hizo angalau wapate hata kidogo lami. Hadhi itaanza kuonekana sasa, Manispaa Sumbawanga imeweza kupata.

La pili ni suala zima la kuwa na taa barabarani. Ni suala ambalo huwa ni muhimu sana kwanza kwa usalama lakini pia ni kwa ajili ya mazingira ya kufanya Mji wenyeve uonekane mzuri. Mji wa Sumbawanga ni kati ya miji peke yake ambayoimepangwa vizuri haina *scoters* ni mji peke yake ukienda kila mahali na wengi Waheshimiwa Wabunge mmetembelea Mkoa wa Rukwa hata wenyeji katika vijiji wanajipanga wenyeve katika mistari hawangoji kulazimishwa, ni tabia ya watu wa Rukwa wanapenda kupanga mambo yao yanakwenda kwa mipango hawaendi hovyohovyo. Sasa hilo tulidhani ni vizuri mkaliangalia namna ya kutusaidia. Pia suala la maji lipewe umuhimu (*Makofi*)

Lakini pia hatuna hospitali. Tuna hospitali ya Mkoa na hospitali ya Mkoa inakuwa ina masharti inakuwa kama ya Rufaa, wote kutoka Mpanda, kutoka Nkasi, kutoka Sumbawanga Vijijini na Sumbawanga Mjini wote wanategemea hospitali hii. Sasa tatizo tulilo nalo ni kwamba hatuna hospitali yetu wenyeve isipokuwa zahanati ndogo. Ni vizuri ili mazingira hayo yaendane na mazingira ya Manispaa ni vizuri tukaangalia. Akina mama wanasumbuka sana pale Sumbawanga Mjini wanapokwenda kwenye zahanati halafu atoke moja kwa moja kwenda Wilayani. Ukienda hospitali ya Wilaya ni lazima aende Mkoani na Mkoani inakuwa ni kama Hospitali ya Rufaa, katika mazingira hayo tunapata matatizo makubwa sana. Ni vizuri sasa Serikali ikaangalia tukawa na hospitali yetu wenyeve pale mjini halafu baadaye wakawa wanapelekwa kama rufaa katika hospitali ya mkoa. Hilo ni ombi lingine. Tunaomba mitambo na magari ya kufanyia kazi. Hatuna gari, tuna gari moja katika Halmashauri yetu ya Mji ni vizuri yakapewa kipaumbele kwa sababu itakuwa tuna hadhi tu lakini bila vifaa vya kutendea kazi. Tungeomba hilo liangaliwe katika hali hiyo ambayotunadhani ni nzuri. (*Makofi*)

Nataka pia nitumie nafasi hii pia kwanza kumshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na *RAS* wetu ya kwamba sisi Wabunge wenzenu wameshatujengea Ofisi ya Wabunge. Ofisi ya Wabunge wote watatu wa Sumbawanga Mjini, Kalambo na Kwela tumejengewa ofisi ambayo itakuwa sasa na hadhi ya Kibunge.

Sasa katika misingi hiyo nadhani wenzetu tutakuwa tumewawahi wengine ambao wamechelewa. Wengine hata samani hawajapata lakini nataka niupongeze uongozi wa mkoa wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba wametekeleza agizo la Waziri, lakini pia la Serikali ya kwamba kila Mbunge kwa kweli lazima awe na ofisi na awe na hadhi. Kwa hilo nataka niwapongeze pia wametufanya kazi nzuri katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa la muhimu ni maslahi ya Madiwani. Hili limekuwa ni kero, ni kero si kwa Madiwani wenyewe lakini hata baadhi yetu Wabunge tunapobanwa na Madiwani ya kwamba hivi mnatusaidia vipi. Mimi nataka tukaliangalie vizuri suala la maslahi ya Madiwani maana inaweza kusababisha pia tukaendelea kupata madiwani ambao si wataalamu sana wa utendaji wa kazi. Mtu ambaye ni mtaalam ana *degree* zake hatakubali kuomba udiwani kwa sababu sharti mojawapo ni kwamba ni lazima uache kazi nyingine urudi kwenye Udiwani. Sasa kwa nini aache afuate shilingi 30 wakati ndiyo pasho yake kwa mwezi.

Wabunge miaka 10 iliyopita watu walikuwa hawashabikii sana Ubunge, lakini tangu viposhoposh vimeanza watu sasa wanatafuta tafuta kwa udi na uvumba nafasi ya ubunge. Watu wako radhi kwa njia yoyote aache kazi yoyote aingie kwenye Ubunge, binadamu haishi kwa mkate peke yake, ni mazingira na maslahi anayopata na Madiwani mkitaka tuwe na madiwani wazuri zaidi wenyewe utu na uzoefu wa kila namna tujitahidi kuhakikisha tunaangalia maslahi yao na ndiyo inatuletea hasa uhasama kati ya Madiwani na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine Mbunge unadhani Diwani ni msaidizi wake lakini wakati mwangi anakuona wewe kama adui yake na hata mikoani huko tunapigana vikumbo na madiwani wengine badala ya kusaidia Mbunge ndiyo anakuwa mwanzo wa kuanza kupambana na Mbunge huyo badala ya kuona huyo mimi ni msaidizi wake nimsaidie katika kila hali ndiyo anakuwa wa kwanza kuhakikisha anakung'oa katika uongozi wa Ubunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi tunakwenda wapi? Hii ni chuki tu ya kawaida au ni chuki ya maslahi? Tunatafunana wenyewe kwa wenyewe! Hali hiyo sio nzuri. Lazima tuangalie sababu na mazingira tuliyonayo, Madiwani na wenyewe waanze kufikiriwa wapate angalau posho nzuri kama si mishahara kwa sababu wanaweza kutufanyia kazi nzuri zaidi kuliko akiwa anakuja huku hapati chochote. Hata kusimamia utendaji wa kazi itakuwa na wasiwasi. Sasa naona ni vizuri Mheshimiwa Waziri huko Wizarani akaliangalia hilo, linaweza kutusaidia tukapunguza haya matatizo ambayo yamejitokeza.

Mheshimiwa Spika, najua imebaki dakika moja. Nataka niitumie hiyo kwa kumwombea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Mheshimiwa Pinda kila la kheri. Najua wote mnakwenda kutafuta kinyang'anyiro huko Vijijini, naomba tutakiane kila la kheri, turudi salama, tuje tukutane katika nyumba mpya, kwa sababu nasikia Mheshimiwa Spika amesema hapa tutahamia kule kwingine. Kinachotakiwa ni kutakiana kila la kheri ili wote turudi salama na Mwenyezi Mungu atatujalia tatarudi salama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nami fursa hii kwa mwaka huu 2005 ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kwanza kabisa, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mafia kwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudini kubwa za kufufua uchumi wa nchi pamoja na kuleta umoja wa Kitaifa katika nchi yetu. Hakika nampongeza na namwombea kila la kheri Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, baraka tele na upendo kwa jamii nzima ya dunia, sio ya Tanzania pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina budi nikiwa kama Mtanzania, mwanasiasa, mpigakura na mwanapwani kuweza kuhakikisha natoa pongezi zangu za dhati mimi binafsi na pia kwa niaba ya wananchi wa Mafia kumpongeza na kumtakia kila la kheri kaka yetu, kiongozi wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na ninaamini, kwa hali jinsi tunavyoiona Mitaani, basi Mwenyezi Mungu ameshamweka mahali ambapo naamini atatuongoza vizuri na awe Rais mwenye mapenzi na watu na Mungu amjaalie ahadi zake ziweze kutekelezeka kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa tena pongezi kwa Mawaziri wa Fedha na Mipango kwa jinsi walivyoandaa hotuba zao nzuri zenye kuweza kufanikisha hasa linapozungumzwa neno MKUKUTA. Naamini sasa Mafia tutakomboka pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Pia, sina budi kuwapongeza Waziri Brigedia Jenerali Mstaafu Ngwilizi pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Pinda kwa jinsi wanavyozifanya shughuli zao katika kutekeleza ahadi au Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa wananchi wa Tanzania kwa sababu tunazungumzia Wizara zote, lakini wao ndio washika bendera wa hayo maendeleo kule Wilayani. Naamini wana kazi nzito, lakini walipewa nafasi hizo na Mheshimiwa Rais kwa kuamini kwamba wataweza kuzitekeleza na zimetekelzeza.

Mheshimiwa Spika, haraka haraka pia naomba nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kifo cha Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga. Mwenyezi Mungu aijaalie roho ya Marehemu huyu ilale mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Mafia ni kisiwa kama inavyofahamika kijiografia na sisi tunaoishi kule hatukupenda, lakini ndio Mungu aliifanya jamii yake iende kukaa Kisiwani iwe sehemu ya maisha yao. Tanzania inafahamu kwamba Kisiwa cha Mafia ni moja ya Kisiwa chake na ni Wilaya iliyopo katika Mkoa wa Pwani. Sasa upweke huu unatufanya tunapata shida nydingi sana.

Yamezungumzwa mengi na kama nilivyosema, Wizara hii ya TAMISEMI inajumuisha Wizara zote. Ikiwa Kilimo, itapeleka TAMISEMI ili imfikie mwananchi Kijijini na hata ujenzi kwenye barabara na kila kitu. Sasa nitaomba niende Sekta hadi Sekta na nitaanza na suala la barabara kwa sababu sasa hivi ndio adha kubwa kabisa ya wananchi wa Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza miaka mingi sana tatizo la ujenzi wa barabara. Tatizo la barabara za Mafia ni udongo tuliokuwanao, sijui unafanyaje! Lakini nafikiri pia upo udongo ambao unaweza ukajenga barabara za Mafia na zikawa imara. Kutoka katika Kijiji cha Kirongwe kwenda katika Kijiji cha Bweni Kilometra kama 35, kutoka Kilindoni Mji Mkuu wa Wilaya ya Mafia pana udongo uliotumika ambao umechanganyika na mawe, ni imara na mpaka leo hapajavurugika. Sasa sijui Wizara ya Ujenzi inataka udongo huo usitumike au hao wataalam wake wanassema utumike wapi mpaka wao wanawaambia kwamba huo udongo wa Mafia haufai kutengenezea barabara. Sasa tufanyeje na Mungu ndio aliyetujaalia huo? Lakini upo udongo ambao una kifusi, ukipatikana huo, naamini barabara zetu maisha yote zitakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kingine kikubwa ambacho kinatupa adhabu, ni hawa wakandarasi wanaoletwa. Sitaki kusema vibaya, lakini hii karatasi ninayo hapa ina matatizo ya wakandarasi wanaoletwa kupitia *TANROADS*. Vigezo wanavyotumia ni vya kawaida ambavyo vinakubalika na sisi tunawapokea, lakini tatizo linakuja hawa wakandarasi wanapokuja kule wanakuja wao na kimfuko? Samahani kama hiki. (*Hapa kielelezo husika kilionyeshwa Bungeni*)

Anakuja amekiweka kwapani basi, hana kitu kingine chochote anachokuja nacho Mafia. Sasa hivyo kweli hizi barabara zitatumika vipi? Zitajengeka vipi ili ziwe imara? Kwa sababu kama jembe litatumika ni la Mafia, kama mfanyakazi, ni wa Mafia, hana kitu anachonunua au anacholeta kutoka nje. Ndio maana tunaomba, Wizara ya Ujenzi inaelekea kama kidogo ina mtihani, sisemi haitaki, nasema ina mtihani kutohuna na sheria ile ya Mfuko wa Barabara.

Sasa tunaomba kupitia kwako, Wilaya ya Mafia mwaka jana tumepata cheti safi, sasa basi kwa heshima hiyo tunaomba katika huu mfumo wa uboreshaji wa Wilaya, basi Wizara hii sasa hivi itusaidie kutupa Shilingi milioni 120 au milioni 150 tuanzie kulipia vifaa vya barabara ili tuweze kutengeneza barabara zetu wenyewe. Hao wakandarasi watakoletwa watatumia vifaa vile kwa kuvikodisha, sio bure. Vitalipa kwa kipindi cha miaka mitatu tu.

Mheshimiwa Spika, huu Mfuko wa Barabara pia watusaidie kutuombea ili tuweze kupata kwa sababu bila hivyo tutalalamika, mwisho tena binadamu hata kama si mimi akija mwingine inaweza kumtoka lugha mbaya, ikawa tena ameivunjia heshima Serikali, itakuwa sio vizuri. Ndio maana tumejitahidi sasa hivi kuomba kila wakati. Tunaomba vifaa vyetu vya barabara Wilaya ya Mafia, tumieni upendeleo, Serikali hii ninaamini kwa makusanyo inayokusanya haiwezi kufilisika au kupoteza dira yake ya maendeleo kwa nchi nzima kwa Shilingi milioni 200, haiwezekani! Kwa hiyo, kwa heshima, tunaomba kupitia Bunge hili, tupatiwe vifaa vya ujenzi wa barabara. Tukipata Shilingi milioni 200, sisi tutahakikisha vifaa vyote kamili vitapatikana na barabara zetu zote zitakuwa nzuri na zitarejeshwa kwa kipindi kifupi kwa sababu hawa wakandarasi watakuwa wanakodi.

Mheshimiwa Spika, kuna Kampuni moja inaitwa *TANHOPE*. Kuna jamaa jina lake anaitwa Kileo alikuja kule Mafia. Matokeo yake nadaiwa mimi pesa hizi. *Total* zipo karibu Shilingi milioni saba, ndio katika kushikanashikana akalipa nusu, bado nusu. Kuna huyu Mwalimu Yesaya masikini ana ki-guest chake pale, kakaa pale anadai Sh. 205,000/=. Wewe mtu mdogo wa Kijiji kama huyu uende kumdhulumu Sh. 205,000/=! Haya yote ni kwa sababu ya kuleta wakandarasi ambao hawajiamini, wanakuja kubabaisha, tunapowagomea, matokeo yake wanakimbia na pesa za watu.

Wengine waliodhulumiwa ni Abdallah Jabey Sh. 738,000/=; Hassan Makunda Sh. 798,000/= na Rashid Abdallah Sh. 137,000/= kwa sababu ya wakandarasi ambao hawana dira wala mwelekeo. Haya yote yatakosekana kama tutapata vifaa vyetu na ninyi mkiingia Mkataba na Halmashauri au hawa wakandarasi wakija kusimamia pale kwa sababu sisi tutalinda vyombo vyetu na tutalinda barabara zetu, naamini haya yote hayatatokea.

Sasa kwa huyu mkandarasi, nasubiri Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, nitamwambia kupitia kitengo chake cha Bodi ya Wakandarasi, hii kampuni ya *TANHOPE* ichukuliwe hatua na irejeshe pesa za watu haraka sana. Tunaomba mtusaidie hizi pesa za hawa jamaa zirudishwe haraka sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kila siku nazungumza kwamba kilimo ni uti wa mgongo, lakini hebu njoo Mafia. Mafia tunalima minazi, tunayo ardhi ya kulima mbogamboga, tunalima mihogoto, mpunga, mazao mengine na korosho, lakini hawa Maafisa Ugani bila ya kuwa na nyenzo watafika viyi kule Vijiji kwa wananchi?

Tunaomba kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Wilaya ya Mafia ipatiwe japo gari moja ya usafiri kwa ajili ya Idara ya Kilimo kwa sababu bila kupata hilo gari kila siku tutakuwa tunalaumiwa, Maafisa Kilimo hawafiki Vijiji, watafika na nini wakati hawana usafiri? Mafia tunategemea gari moja ya Idara ya Elimu. Kila Idara inakwenda hapo hapo na wao wenyewe wana shughuli zao, ndio maana unakuwa mtihani mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba tupatiwe gari moja kwa Idara ya Kilimo ili hawa Maafisa Ugani waweze kuwafikia wananchi. Mafia miaka kumi na tano au ishirini iliyopita tulikuwa na matrekta, lakini bahati mbaya mambo ya Vijiji yakawa yamevurugika. Matrekta yale yalikuwa ya mikopo yakawa imepotea. Sasa tunaomba basi safari hii kupitia Wizara hii, Idara ya Kilimo huko TAMISEMI iende Wizara ya Kilimo kuomba angalau Mafia tupatiwe matrekta mawili tu, wala sio mengi ili tuweze na sisi kufanikisha kulima kwa wingi mazao yetu.

Kwa mfano, kama mwaka juzi, tulilima viazi japokuwa kwa jembe la mkono, lakini tuliiza mpaka Lindi. Mwezi wa Ramadhani Mkoa wa Lindi sisi tuliulisha viazi vitamu. Sasa kama tutapatiwa matrekta, mambo yetu yatakuwa makubwa sana kule Mafia.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, Mheshimiwa Waziri amezungumza katika kitabu chake kuhusu Shirika la Masoko la Kariakoo. Mazao ya pale yanayopelekwa nafikiri nazi ni zao moja kubwa kabisa na mapato makubwa yanapatikana kuititia nazi japokuwa hili zao limekosa bahati. Kila siku tunaambiwa litaundiwa Bodi, imekuwa wimbo tu. Lakini naamini baadaye mwaka huu labda Waziri atatamka kwamba zao la nazi litaundiwa Bodi pamoja na mazao mengine.

Sasa tunasema Shirika hili la Masoko linajitahidi kufanikisha na kukusanya mapato mbalimbali, lakini upande wa nazi bado. Naomba Mheshimiwa Waziri apitie aangalie eneo linalouziwa nazi likoje. Nazi ikipata mvua inaharibika, ikipigwa na juu itapasuka na sisi ndio riziki zetu zinapopitia pale. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aliagize Shirika la Masoko ili liweze sasa hivi kutengeneza sehemu nzuri kwa ajili ya kuhifadhi nazi za mkulima wa Mafia, Rufiji, Lindi na sehemu nyingine zinazolima nazi. Hilo likifanikiwa na sisi tutaweza kufarijika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, naomba bila kupoteza muda nimshukuru Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Ukiwaona Ditopile Mzuzuri. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa namshukuru sana kwa jitihada zake anazozifanya katika Wilaya ya Mafia katika kusimamia kutatua migogoro mbalimbali iliyokuwemo katika Wilaya hiyo. Naomba kuititia kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nimshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwani amejitahidi kutusaidia kuondoa matatizo makubwa kabisa ambayo kama yasingewezekana, basi Mafia tungekosa mapato mengi sana, lakini kutokana na juhudhi zake, Mafia tunakusanya au tutakusanya mapato makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisipoteze muda mwingi, naomba niwashukuruni wote na pia kuwashukuru Watendaji wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa Mkurugenzi wao. Miaka mitano imekwisha, wamenipa ushirikiano, wananchi, Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wote wa Chama na Serikali wa Wilaya ya Mafia bila kumsahau Mkuu wangu wa Wilaya Ali Mohammed Libaba, Viongozi wangu wa Chama Mkoa, Mwenyekiti wangu Bwana Mlao, Katibu wangu Mama Makilagi pamoja na Katibu wangu wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi Bwana Said Mbarak.

Hawa wote naomba niwashukuru pamoja na Viongozi wote wa Chama kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Kijiji na wananchi wa Mafia nawashukuru kwa heshima waliiyonipa lakini na mimi nasema nimewaonyesha juhudhi zile ambazo wao wenyewe watakuwa mashahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini watanipa tena nafasi hii ili niendelee kuzidisha maendeleo katika Wilaya yetu na kuipa sifa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Naamini hata Viongozi wanaamini kwamba sikuwadhalilisha au sitowasemesha vibaya kwamba Chama cha Mapinduzi Viongozi wake Wilaya ya Mafia hawakufanya vizuri. Hata Wapinzani wanapokuja kule, kazi yao kusema tu wanashindwa kutwambia nini hatukufanya. Kila Idara tumeingia na tumeifanyia kazi, ajira, elimu, afya na maji.

Mheshimiwa Spika, kilichotushinda ni barabara na ninasubiri unisaidie sana baadaye kwa kunipa nafasi katika Wizara tatu, nazo ni Mawasiliano, Ujenzi na Maliasili. Naomba usiache kunipa nafasi hiyo, nina yangu ambayo nataka kuyasema kwa manufaa ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia na wewe nakutakia kila la kheri katika maisha na familia yako. (*Makofi*)

MHE. OSCAR T. MLOKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, ningependa nitoe salaam zangu za rambirambi kwa mpendwa wetu aliyetutoka wakati tunakaribia kuanza Mkutano wetu huu wa mwisho, Marehemu Abu Kiwanga ambaye namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningependa kutoa pongezi nyingi sana kwa chaguo la CCM la kumweka mpendwa wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi pamoja naye Dr. Ali Mohammed Shein kwa nafasi ya Mgombea mwenza na pia Mheshimiwa Karume kwa nafasi ya Urais kule Zanzibar. Nawatakia kila la kheri hapo mwezi wa kumi ili waweze kulisogezza jahazi hili la Chama cha Mapinduzi likaenda mahali pake panapostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri pamoja na mawasilisho ambayo yapo mbele yetu leo. Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Wizara nyeti sana kwa sababu inabeba jukumu zito la Halmashauri zetu zote za nchi hii pamoja na Mikoa yake. Ningeweza kuifananisha na kule sokoni huwa wanasema kama ni gunia, hili gunia ni lumbesa ambalo kulibeba kwake uwe kwa kweli ni mtu jasiri wa namna yake, vinginevyo utadondoka. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa kuiendesha Wizara hii mpaka tumefikia hapa tulipo katika jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hasa za Miji ni kioo cha nchi yetu, lakini zitaonekana kuwa ni kioo tu pale zinapoonekana miundombinu yake inavutia na kuvutia kwa Miji hasa Manispaa ni kuwa na barabara za lami na si majengo. Barabara za lami ndio sifa pekee ambayo kwa kweli itamfanya mtu aseme kwamba kwa kweli huu ni Mji unaostahili sifa za namna yake. Bahati mbaya sana barabara za lami għarama za ujenzi wake ni kubwa sana.

Barabara za lami za tabaka la chini kwa ubora zinaitwa *surface dressing*. Hizi bila Shilingi milioni 150 kwa kilometra hajawa barabara. Kwa hiyo, utaona jinsi ilivyokuwa vigumu kwa Halmashauri zetu kuweza kumudu kutengeneza barabara za lami. Ukienda ile ya tabaka la kwanza ya kiwango cha kwanza ile ya *asphalt concrete* hii ina għarama ya kuanzia Shilingi milioni 250 hadi Shilingi milioni 300 kwa Kilometra moja. Kwa hiyo, bado inaongeza ugumu kwa Halmashauri zetu kuweza kumudu matengenezo ya barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, sina uhakika ni Halmashauri gani ya Mji, Manispaa au Jiji ambayo imeweza kutengeneza barabara zake yenyewe bila kumtumia mfadhili kama atakuwa yupo kuweza kutengeneza hizi barabara kwa sababu ya gharama zilivyokuwa kubwa. Hivyo, utakuta kwa Mji kama wa Morogoro tulikuwa na barabara nyingi ambazo zilikuwa za lami toka tumepeata uhuru, lakini sasa hivi sio barabara tena, tumeamua kuzipiga *grader* ili angalau basi yale mahandaki ambayo yalikuwa yanafanya hata mtu wa kwenda kwa miguu kushindwa, kuweza kuyaondoa kwa utaratibu huo.

Pale tulikuwa na barabara kwa mfano, kama unakwenda Shule ya Sekondari ya Kilakala, zamani ilikuwa inaitwa *Marian College*, ile barabara ilikuwa ni ya lami. Lakini sasa hivi mtu ukimwambia ilikuwa ya lami, hawesi kuamini kwa sababu hakuna hata dalili kwamba ilikuwa ni ya lami kwa upande ule. Nyingine ni kama Kingaru, Rwegasore, Boma, Saba Saba, Uhuru, Nkomo na hata eneo la Mji mpya pale.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi ambacho ni kichekesho, ni barabara ya Boma. Hii ni barabara inayokwenda kwenye Makao Makuu ya Mkoa kule ambako iko Ikulu ndogo ya Mkoa mahali ambako Viongozi wa Serikali na wa Kitaifa wanapaswa kwenda. Barabara hii si lami tena, badala yake tunalazimika tukisikia Kiongozi wa Kitaifa anakuja kuziba mashimo yake kwa udongo. Hakuna Chuo chochote kinachofundisha barabara ya lami uweke viraka kwa udongo, lakini nadhani hali yetu inatulazimisha tutafute Shule ambazo hazipo za kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na ombi kwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba, ni vyema ikaacha maeneo mengine yote lakini barabara ambayo inakwenda Ikulu ndogo mahali ambapo Rais kama anakuja sharti akapumzike, tuiwekee umuhimu wa kwanza angalau basi kwa kutumia hata zile fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zinakuja kidogo kidogo sana, maana huwa wanaleta Shilingi milioni 60 au Shilingi milioni 70 ambazo hazitengenezi hata nusu Kilometa ya barabara ya lami.

Kwa hiyo, tunaomba basi zije na maelekezo kwa sababu ukileta moja kwa moja kwenye Halmashauri, kwamba hizi fedha za Mfuko wa Barabara, inatakiwa itengenezwe barabara, sisi tutakimbilia kutengeneza barabara za changarawe kwa sababu ndizo zinazoonekana na ndizo zinazopitwa na watu wengi. Lakini hii barabara ya lami ambayo fedha ulizoleta zitakuwa hazitoshi hata kutengeneza Kilometa moja, tutaona kama kuchukua nusu kilo ya sukari ukatumbukiza kwenye pipa la maji, hutaona hata *impact* yake. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana itazamwe barabara hii ambayo inakwenda kwenye Makao Makuu ya Mkoa na Ikulu ndogo ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara nyingine katika Mji wa Morogoro ambayo imekwepesha magari makubwa yanayokwenda stesheni kupeleka mizigo yasiweze kupita katikati ya Mji na pengine kuharibu daraja lile la *Shan Cinema* ambalo juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alilitolea jibu zuri, lenye mafanikio na matumaini. Barabara hii inaitwa Mei Mosi. Barabara ya Mei Mosi ndiyo inayokwepesha magari mazito yenye tani zaidi ya kumi na tano mpaka tani 80 iweze kupeleka mizigo mizito stesheni na kuipakia kwenda sehemu zinazostahili.

Kwa uzito wa barabara hii na kwa umuhimu wake, nilikuwa nadhani pia vile vile hapa Wizara itazame sehemu hii kwa jicho la husuda ili angalau basi iweze kupata tabaka la lami na kuweza kukwepesha magari haya mazito yasiharibu Mji wetu. Barabara hii haina umbali mkubwa sana, ni kama Kilometra 1.6 sita au kilomita mbili hivi. Kwa hiyo, nadhani kama ni lami ya daraja la pili ya *surface dressing* nadhani haitafikia hata Shilingi milioni 300 itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu miundombinu ndani ya Mji. Nikienda ukurasa wa 10 wa Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameellezea miundombinu mbalimbali ambayo Miji kadhaa imepata kupitia kwa wafadhili mbalimbali, nayo imepitia kwenye Mradi wa Uimarishaji Huduma za Mji. Mimi nishukuru kwamba, tumepata barabara moja nzuri ya kuingia katikati ya Mji kutoka Msamvu, ile barabara imepata tabaka la lami kupitia mradi huu.

Kwa hiyo, nazipongeza sana juhudi hizi ambazo zimefanywa katika Mji wetu wa Morogoro. Lakini pia tuna ujenzi wa Kituo cha Mabasi pale Mjini ambacho katika utaratibu huu huu kilipata pesa kidogo na kikatengenezwa. Sasa hivi kimeshaanza kutumika, lakini kimetumika kwa kweli si kwamba kimekamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo kile cha Mabasi unahitaji Shilingi bilioni 4.5, lakini gharama za awali tu ambazo tumezitumia pale kwa kukifanya angalau mabasi yaanze kupakia na kushusha abiria, tumetumia kama Shilingi milioni 500.

Kwa kweli haifiki hata moja ya kumi ya gharama ambazo zinastahili zitumike pale. Lakini kama nilivyoanza kusema ni kwamba, Halmashauri haiwezi kwa namna yoyote kutimiza lengo hilo kutohana na kipato chake kuwa duni. Hivyo, nilikuwa naomba tena Wizara kwa sababu ndiyo mhimili wa Halmashauri, basi itutafutie wafadhili ili tuweze kukamilisha azma ile ambayo ipo pale.

Mheshimiwa Spika, kwa vile kengele ya kwanza imeshalia, naomba nizungumzie la mwisho. Naomba nimshukuru Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuanzisha au kwa kuzipandisha Halmashauri za Manispaa tatu za Arusha, Mbeya na Tanga kuwa Majiji kuanzia Julai Mosi. Naamini kabisa kwamba vigezo vilivyotumika vinastahili na vinakidhi mahitaji yanayotakiwa, lakini nadhani baada ya hatua hiyo kukamilika, Dodoma kama Makao Makuu ya nchi, ndio itakayofuata kwa kupandishwa hadhi hiyo.

Lakini pia kwa sababu Morogoro iko katikati ya Dar es Salaam na Dodoma, hakuna atakayekosa kupita Morogoro. Nadhani pia nayo inastahili kuwekwa katika vigezo vilivyokuwa vinatazamwa hatimaye nayo iweze kuwa Jiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba niseme naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofit*)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa

TAMISEMI. Pili, niipongeze hotuba ya Waziri Kivuli, mzungumzaji aliwewasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa kuonyesha wazi nini Kambi ya Upinzani imepanga kufanya pindi wananchi wakitupigia kura mwezi Oktoba, tarehe 30.

Kupitia Bunge hili, tunataka kuwahakikishia wananchi kwamba pamoja na mikwara, pamoja mambo mengi, sisi hiyo haitatuzuia kuueleza Umma ukweli, haitatuzuia kutoa njia mbadala ambayo tunaamini inaweza ikawanusuru Watanzania dhidi ya umaskini, maradhi na ujinga ambavyo vimekithiri zaidi ya miaka 43 hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Bwana wetu Yesu Kristo alipokuwa anawahutubia wanafunzi wake, alikuwa akitoa mifano mara nyingi na kila mara alipotoa mifano au mafunzo yake alimalizia kwa kusema kwamba na mwenye masikio na asikie. Naamini wale tunaowaeleza wanasikia, wana masikio na wana macho wanaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, kazi kubwa tunayoifanya hapa ya kuisimamia Serikali na kuishauri na kuikosoa ni sawa na mchezo wa mpira ambapo timu inakuwa *home ground* na wakati mwengine inachezea mchezo wake nje ya uwanja wa nyumbani. Ndani ya Bunge kama hili ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi ni wa Chama cha Mapinduzi, ninaamini inatumika kama *home ground* yao, lakini upande wetu wa Upinzani *ground* yetu naamini ni Umma mkubwa ulioko huko nje unaojua na kufuatilia nini kinachotendeka katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la mapato duni katika Halmashauri zetu, hilo jambo halina utata, ni kama jinsi Waziri wangu kivuli alivyolizungumza, ni kero! Pamoja na kazi nzuri ya Serikali ya kuondoa kodi zenyet kero kwa wananchi, kuweka utaratibu mzuri wa leseni, lakini siyo siri kwamba mara nyingi hatua hizi zimekuwa zinachukuliwa kwa dharura mno bila kuhusisha Halmashauri husika na matokeo yake kunatokea *deficit* kubwa katika mipango ya Halmashauri. Hivi sasa limezungumzwa suala la madeni.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri yangu pamoja na utaratibu huo mzuri wa Serikali uliozungumzwa ni kwamba hivi sasa ina madeni zaidi ya Shilingi milioni 60 na katika bajeti yake ilitegemea kama utaratibu usingebadilika labda ingepata Shilingi milioni 200 kupitia kwenye leseni. Sasa chini ya utaratibu uliotumika kujaribu kutafuta wastani wa miaka tofauti ni kwamba tunapata Shilingi milioni 85. Sasa hii ni kasoro kubwa kwa sababu unapochukua wastani, kuna mwaka ambapo Halmashauri inakuwa imefanya vizuri na kuna mwaka ambapo inakuwa imefanya vibaya. Sasa unapofanya wastani huwezi kupata picha sahihi ya lile ambalo unakuwa umelilenga. Kwa hiyo, utaratibu huu ni bora urejewe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba ndani ya utaratibu wa Wizara hii katika suala la maboresho, elimu imekuwa inatolewa kwa Viongozi wetu. Lakini ningeomba kwamba ni vizuri hiyo *syllabus* inayotolewa kwa viongozi wetu ikawekwa wazi tukaifahamu. Kwa sababu nina wasiwasi kwamba *syllabus* aidha ina mapungufu au huenda wanaokwenda kwenye mafunzo hayo wengine labda akili zimechoka kwa

sababu kuna mambo mengine yanayokuja kujitokeza ambayo ni kinyume na utawala bora. Jambo ambalo naamini ni msingi wa kuwepo maboresha ya *councils* zetu na kuboresha *system* nzima ya kiutawala.

Mheshimiwa Spika, tukiwa kwenye Kamati, nilizungumzia mmojawapo kule Dar es Salaam kwamba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuna wakati huwa tunashindwa kumwelewa anapohutubia, huwezi kujuu kama anapozungumza anazungumza kama kada wa Chama, anazungumza kama Mkuu wa Mkoa, anazungumza kama mkereketwa hachanganui mambo yake na watu hawamwelewi. Katika *statement* yake moja, aliwahi kuzungumza kwamba yeze Upinzani utakuja kutawala kwenye Mkoa wake siku atakapoacha Ukuu wa Mkoa.

Mimi nafikiri hiyo siyo *statement* ya mtu anayetegemewa kuwa ni Mkuu wa Mkoa ambaye anatawala watu wa aina mbalimbali na watu wa Vyama mbalimbali na wasiokuwa na Vyama. Sasa jamii tunaichanganya.

Mheshimiwa Spika, mimi ninafikiri, aidha ni aina ya mafunzo yanayotolewa, *syllabus* sijui inajikita katika mambo gani! Katika kulithibitisha hilo, mimi ndani ya Kamati nilijaribu kuitia bajeti ya Mkoa wa Dar es Salaam ambayo leo imewasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri ili ipitishwe na Bunge.

Nilijaribu kuzungumza ndani ya Kamati kwamba jamani hebu nendeni haya mambo mkayarekebishe ili muweke takwimu sawa. Bahati nzuri aliyemwakilisha *RC* - Dar es Salaam siku hiyo ni Kaka Ditopile akatoa maneno matamu *as usual*. Lakini akasema kwamba hayo mambo yatarekebishwa. Akasema, “Unajua mtu ukishaoga maji yakamkolea, anajikuta amekolewa na asitoke bafuni.” Sasa ndani ya makadirio hayo kilichozungumzwa kwenda kurekebishwa hakikurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini siku ya jana bahati nzuri wakati nimerejea usiku ingawa kuna mtu mmoja alisema kwamba nimekimbia Bungeni, hili ni pamoja na yeze kutotumia vyombo vyake kama Waziri Mkuu ambapo naamini ana uwezo huo kujuu huyu Waziri Mkuu Kivuli yuko wapi na kwamba ameondoka ndani ya Bunge hili na ruhusa ya Spika na inafahamika aliko mpaka siku ya jana, yeze anapozungumza uongo. Lakini hiyo yote nafikiri ni uwezo wa mtu kuweza kupanga na kutambua mambo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 26 wa kitabu chake, marekebiso hayo mpaka usiku wa kuamkia leo wakati ninadai kitabu hiki nikaletewa, kinasema: “Mkoa unaomba fedha Sh.20,620,000/= kwa ajili ya ununuzi wa thamani mbalimbali kama vile viti, meza, *cabinet*, *shelf* kwa matumizi ya Ofisi. Inaendelea inasema, hii ni pamoja na kuwashudumia Makatibu Tawala Wasaidizi katika kumsaidia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.” Sasa nikasema, Wallahi tunakwenda wapi? Kama tunakwenda na mdundiko wa bajeti ya namna hii, twende na mdundiko wa bajeti ambayo ni ya kumsaidia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ni Mgombea mmojawapo wa Urais! Hii ni balaa! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini watendaji hawakukosea waliotayarisha hii bajeti, wamefanya kile kilichokwenda na maelekezo ya kutoka juu. Ndiyo maana hatu pamoja na kujaribu kuwaelezea wakati wa Kikao cha Kamati, bado dhamira imeendelea kuwa ile ile. Naamini kwamba hii tu ni kuonyesha wazi nini kilichomo ndani ya Bajeti nzima kwamba huenda maelekezo yametolewa, vitu vimefichwafichwa ndani ya bajeti hii kujaribu kusaidia hili.

Namshukuru sana Mheshimiwa Yussuf Makamba, shemeji yangu kwa kuliweka wazi hili. Inasemekana kwamba hii bajeti bila shaka mafungu yametengwa humu ndani kwa ndani kwa ajili ya kusaidia suala hilo la Mgombea wa CCM.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unaosema kwamba mtu mzima akidanganya anaweza akaua. Sasa nimeisoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini jukumu mojawapo linazungumzwa kwamba kazi yake kubwa ni kujenga na kuimarisha demokrasia na utawala bora. Nampongeza. Lakini Watendaji wetu wa chini tunaowaongoza wanafuata mfumo na tabia ya sisi tulioko juu. Kama sisi ni waongo na wanafiki kule chini, utamdhiliti vipi mtu asiwe mwongo na asiwe mnafiki?

Mheshimiwa Spika, sasa kuna bwana mkubwa mmoja hapa Mheshimiwa Seif Muhammed Khatib, katika hotuba yake wakati *ana-wind up* anasema na ninamnukuu: “Ni dhahiri kwamba hotuba ile aliyotoa Kiongozi wa Upinzani hakuandika yeye, imeandikwa Mtendeni Unguja na ushahidi ninao kaletewa kwa *Fax* usiku hapa, kaja kaisoma. Kwa hiyo, huyu katumwa tu.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mtu mzima akidanganya anaweza akaua. Huku kujenga na kuimarisha demokrasia na utawala bora hauwezi kuimarishwa kwa kuzungumza upuuzi upuuzi hapa na uongo. Sasa kupitia Kanuni kifungu namba 50(1) nitaomba mtu huyu kweli kabisa athibitishe. Atoe uthibitisho kwamba hotuba ya Kiongozi wa Upinzani inaweza ikawa imetoka Mtendeni. Vile vile, kama atakuwa amedanganya, awajibike na kama atathibitisha kupitia Bunge hili, natamka rasmi kabisa, nitajivua Ubunge pamoja na kwamba kuna kitita cha milioni ngapi sijui kinategemewa kupatikana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo kubwa ninalotaka kuzungumzia ni hili la kuimarisha demokrasia na utawala bora. Ni vyema tukazungumza ukweli na tukawa mfano kwa watu wengine. Mimi napenda kuwashukuru Walimu wangu, walinfundisha vizuri katika Vyuo vyote nilivyopitia; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Manchester University* na bahati nzuri na Walimu wangu wengine kama Dr. Ibrahim Msabaha, yuko hapa anajua nilivyokuwa nashusha vitu. Kwa hiyo, sina tatizo la kuandaa mambo haya na kusimamia Kambi kuivusha na kufanya lile ambalo Watanzania wanategemea nilifanye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuwezesha Kamati za Bunge kufanya kazi yake. Wakati wa uhai wa Bunge hili, Kamati yetu iliweza kujipangia shughuli ya kwenda kuchunguza mahesabu ya Mkoa wa Pwani. Lakini ilikuwa ni balaa kwamba hakukuwepo na Bajeti au mafungu ya kutosha ya kuweza kwenda kuifanya kazi hiyo vizuri. Sasa mimi naamini kama tunataka tuweze kuishauri Serikali na kuidhibiti vizuri,

suala la kuwezesha Kamati za Bunge kufanya kazi zake vizuri, naamini litakuwa ni jema.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nasema hivi bahati nzuri wakati na-*quote* hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa, sikutunga maneno yangu kutoka kichwani, ni kitabu kabisa ambacho kilichapishwa na Mchapishaji Mkuu wa Serikali na picha ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa hii hapa ya kitabu chenyewe. Kwa hiyo, si maneno niliyotunga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, unajua mtu akifumaniwa, tatizo lake moja kwanza linaloweza kumkabili hata akiponyoka, anaweza akajisahau akavaa chupi ambayo siyo yake. Sasa akifika hata nyumbani anaweza akajikuta anafumaniwa mara ya pili na mke wake kwa sababu ya kufanya kosa hilo. Maadam tumesema kwamba iko siku ambayo sisi tutamtaka Mheshimiwa Waziri awe ameweka wazi nyaraka zote zinazohusiana na suala la wazee wa *East African Community*, tumetaka siku nne kabla, naamini hata kama atakuwa hajafanya hivyo, ukweli utadhihirika. Sisi tutawasilisha nyaraka zinazohusika kwa wote watakaotaka kuujua ukweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia General Hassan Ngwilizi.

Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Brigedia General Hassan Ngwilizi kwa hotuba yake nzuri ambayo haikuwa na inda ndani yake na aliiweka kama Serikali hakuna, hata mahali pamoa alizungumzia mambo ya Chama, aliiweka kama Serikali na ndiyo sababu inaitwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tawala na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuielimisha jamii ya Watanzania mtiririko wa Ugavana tulionao. Mwenyekiti wa Kitongoji ni Gavana, Mwenyekiti wa Kijiji ni Gavana, Afisa Mtendaji wa Kata ni Gavana, Afisa Mtendaji wa Tarafa ni Gavana, Mkuu wa Wilaya ni Gavana, Mkuu wa Mkoa ni Gavana, kutokea pale mwingine hayupo tena, isipokuwa kuna Gavana mmoja tu ambaye ni Rais mwenyewe. Wengine wote waliobaki ni wa masuala ya utawala tu.

Katika Ugavana huu, haruhusiwi kamwe kuingiliana na masuala ya kisiasa. Yanapoingiliana kwenye masuala ya siasa ni kwamba huyo Gavana ambaye kwa mfano ni Afisa Mtendaji wa Kijiji, amechaguliwa na Kijiji kizima kwamba yeye ni Mwenyekiti wa Kijiji, ndani mle kuna watu wa itikadi za *TLP*, yeye kama ni CCM ndani kule kuna itikadi za *TLP*, kuna itikadi za CHADEMA, kuna itikadi za *NCCR* wote hana budi kuwatendea haki. Lakini akiingiza mambo ya Chama atakuwa hawatendei haki wale waliomweka madarakani.

Mheshimiwa Spika, nimetafuta sheria ya Taifa hili. Wanasheria wengi nimekutana nao, Wanasheria wa Wilaya, Mahakimu, Wanasheria wa Mahakama Kuu, nikatafuta kwenye Katiba ni wapi imeandikwa kwamba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ni Viongozi wa kisiasa, yaani *Political Leaders?* Sikupata! Nikajiuliza, huyu kiongozi mkubwa kabisa kiasi hiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu anayetawala Mawaziri wote, anakuja hapa Bungeni anatuambia kwamba Maafisa Wilaya na Maafisa Mikoa ni Viongozi wa Kisiasa, amepata nguvu hizi kutoka wapi? Hapo baadaye nitataka kujua amepata wapi nguvu hizi na kama amepotosha wananchi hana budi kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, kwa upotoshaji huo, matokeo yake nimeyaona. Kwanza, imefikia mahali karibu nishindwe kusimamia majukumu yangu katika Jimbo la Vunjo. Jimbo la Vunjo nimejikuta nipo chini ya Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya amepewa rungu mbili, rungu ya dola mkono wa kulia yenye kilo tano, rungu ya Chama mkono wa kushoto yenye kilo tano. Kila ninalofanya anatumia rungu moja ya kulia au kushoto ya kisiasa au ya Kiserikali. Nasema, kama mimi sikufundishwa vizuri masuala mazima ya nidhamu ya kijeshi, ningelikuwa nimeishia jela. Kwa matendo anayotenda huyo Mkuu wa Wilaya James Ole-milya. Kwa kuwa inafikia mahali inaitishwa Mikutano au harambee, anakuja amevaa mavazi ya sare ya CCM. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana aliingia kwenye Kanisa moja Mwika Kusini, Kijiji cha Kondeni ambapo Kanisa lile lilimwomba Katibu Mkuu wa CCM kwa uwezo alionao na rasilimali alizonazo aweze kuchangia Kanisa hilo jipya linalojengwa pale Kondeni. Nilitegemea kwamba angelikuja kama Katibu Mkuu wa CCM amevaa suti ya Jumapili kwenda Kanisani. Alipanga mipango yake yote huko akaja kwa kishindo na kitimtim cha *uniforms* za CCM, mapikipiki na magari yote ya CCM, akaingia kwenye Kanisa la Mungu kusali na Wakristo mle ndani.

Alipoingia mle ndani, akafanya harambee na watu wake aliokuja nao zaidi ya 50, akasema, "Kwa ujumla wetu tutatoa mifuko 50 ya sementi." Akasimama Katibu wa CCM Wilaya ya Moshi, akasema: "Hapa napo kuna Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vunjo, sijui ana nini la kusema." Nilijua sasa kazi ya Mungu imeishaingiwa na doa, ibilisi ameishaingia ndani humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilichokifanya, nilimwambia Mheshimiwa Mchungaji Kiongozi, Wainjilisiti, Wazee wa Usharika na Wanausharika, ninaomba tusome Hagai mlango wa kwanza, mstari wa saba hadi nane katika kujenga nyumba ya Bwana. Inasema hivi, naomba kunukuu: "Bwana Mungu wa Majeshi asema hivi, "zitafakarini njia zenu. Pandeni milimani, mkalete miti, mkaijenje nyumba, nami nitaifurahia, nami nitatukuzwa, asema Bwana wa Majeshi." Mwisho wa kunukuu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilichokifanya, niliona tu ninyenyekie chini ya Miguu ya Bwana Mungu na Yesu Kristo ambaye namwamini na nikawaambia kwamba, nitakwenda kwenye Mlima wa Dodoma, Bungeni, nitakwenda kukata tani ya sementi niwaleteeni hapa. Walishangilia Kanisa zima na kunyanyuka kwa vifijo na kwa raha zote. Akasimama Mjumbe mmoja kutoka CCM, akasema hiyo ni mifuko 20 ya sementi tu. Wakazidi kushangilia kwa kuwa watu 53 wameingia mle eti wamekuja kufanya harambee ya Kanisa lile chini ya mfuko mmoja kila mmoja wao!

Mheshimiwa Spika, nasema katika kutenda kazi hizi, tumwogope Mungu na kumpenda badala ya kutanguliza maslahi ya itikadi mbele.

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Vunjo, mimi ni Mbunge kwa tiketi ya *TLP*, hii hapa. (*Hapa Kadi ya Chama cha TLP ilionyeshwa Bungeni*)

MBUNGE FULANI: Naipenda.

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, baada ya kupata kadi hii, nimeiweka mfukoni, ninakuwa ni Mbunge wa madhehebu yote, itikadi zote, viumbe vyote vilivyo hai na ambavyo siyo hai na wote nawatendea haki. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: *Very good!*

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, ninayo Makanisa ya Lutheran Sharika 30, *Roman Catholic* Sharika 12 na Misikiti saba. Nataka kuwashakikishieni kuwa hawa wote kwamba ninawatendea haki. Michango ambayo nimechanga kwa ajili ya Sharika hizi na Misikiti hii, ndugu zangu wale wa Vunjo wanaifahamu na nina hakika wanafurahi kwayo na kamwe sitachoka kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, hawa Viongozi ambao wametajwa ambao ni Magavana aliwazungumzia vizuri sana Mheshimiwa Paul Kimiti ya kwamba angalau kwa sababu tumewahi kuwaweka madarakani, basi Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ipange mipango yake ya kibajeti ili hata Mwenyekiti wa Kitongoji ambaye ni Gavana, apate angalau kitu kidogo cha kumpa *morale* ya kwamba naye ni mmoja katika Magavana katika Serikali hii. Hilo naliomba liwekwe kwenye mipango yenu na lifanyike kama nilivyokuwa nimeomba.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na vikwazo katika kutekeleza majukumu haya katika Jimbo la Vunjo ambapo mafanikio yake ni makubwa mno na matokeo yake Jimbo lile na yale yote katika Mkoa wa Kilimanjaro wanajionea vivu na mtu anayelionea vivu ni yule yule Baba yetu, Rais. Niseme katika hilo sijawahi kuona. Naomba tu nitakapomtaja msije mkamfanya kizingiti akakosa haki zake au mkamwonea vibaya.

Mimi Gavana ambaye namtambua katika Mkoa wa Kilimanjaro ni Mheshimiwa Mama Hilda Ngoye peke yake. Mama Hilda Ngoye ni Gavana sijamwona hata siku moja akishabikia chochote wala lolote. Maendeleo mengi ameyaleta katika Mkoa wa Kilimanjaro na amenisaidia sana katika Jimbo la Vunjo, amenisaidia sana katika mashule hayo ambayo mimi ninayamiliki ambapo nina Shule za Sekondari 32 katika Jimbo la Vunjo. Shule za Sekondari 30 zina wanafunzi tayari wawili mwaka kesho wataingia darasani. Shule za Sekondari 32 zote hizi Mheshimiwa Hilda Ngoye amehimiza kuchangia Shule hizi ili wanafunzi wetu waweze kuingia madarasani.

Mheshimiwa Spika, hakika ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hilda Ngoye, popote alipo apokee sifa na shukrani kwa kazi yake nzuri. Isiwe kusema hivyo ni wao kutokujua kwamba yeze ni mtendaji kazi mzuri katika Serikali na kwamba nafasi hii ya Ukuu wa Mkoa aliyonayo ni *promotion* ya kumfanya yeze awe Waziri hata kama ni Serikali ya Mseto. Hata kama ni Serikali ya Upinzani, Rais atakayekuwepo katika Serikali ya Upinzani ambaye hakika tutampata, hataacha kumuenzi Mheshimiwa Mama Hilda Ngoye.

WABUNGE FULANI: Haa!.

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Hiyo ndiyo sababu hakuna mwenye sifa zilizobobea kama Mheshimiwa Augustino Mrema katika Taifa hili kati ya wote katika kinyanganyiro hiki. Kwa kuona hivyo, nasikitika tena kusema kwamba tumwingize Mheshimiwa Rais hatiani. Mheshimiwa Rais ni Amirijeshi Mkuu, *command in chief*, haruhusiwi kushikamana na Chama chochote. Yeye akaona kwamba achukue kofia zote mbili matokeo yake amekwenda pale Dar es Salaam kwenye hoteli moja akachangia zaidi milioni 162 eti kunyonga upinzani Mkoani Kilimanjaro. *That is political assassination.* Sikutegemea Amirijeshi Mkuu atakwenda tena kwenye mambo ya kisiasa bila kuwaachia wale Wenyevitii wa Mikoa wa Chama cha CCM na wengine kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hilo ni kosa na atalijutia kwa sababu hakika kazi ambayo anafanya Mheshimiwa Freeman Mbewe, haiwezekani wamuache! Kazi anayoifanya Thomas Ngawaiya Moshi Mjini, hatakubali aachwe! Kazi anayofanya Major Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, ni kuhakikisha kwamba Kata za Marangu, Mwita, Himo na Kahe wanaendelea na kazi vizuri. (*Kicheko*)

Ninamwomba kwa upande wa tambarare Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa aangalie suala zima la umwagiliaji, walitaka kukata pale eti liwe Jimbo la Tambarare, wangelipata taabu dunia nzima ingelishuhudia kwa sababu Kaskazini ndiko maji yalipo. Sasa kukata tambarare na mimi nikiwa Mbunge wa Kaskazini maji yote nitafanya kwenye maeneo ya tambarare Kaskazini. Chini tambarare hawatapata maji itakuwa *hazard!* Itakuwa fujo! Itakuwa njaa tupu kwa wananchi wa Ukanda wa Tambarare. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kosa lingine la kunadi vitu ambavyo havistahili na Waandishi wa Habari mnafanyaje. Mkiona Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa anafanya makosa msiandike. Hapa ameandika Mheshimiwa Hassan Ngwilizi. (*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

WABUNGE FULANI: Hapo hapo.

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwenye ukuta kule, muda bado. Kwa kuwa huyu Jenerali ni Mkuu wa Majeshi....

SPIKA: Hapana, Kengele ya pili.

MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumwaga sera zangu ndani ya Ukumbi wa Bunge ambao mimi ninauheshimu na nisingependa uwe wa siasa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe tu pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi kubwa na ngumu wanaoifanya ikizingatiwa kwamba Wizara hii ndiyo Wizara kubwa inayogusa wananchi wengi katika mambo mengi. Ukizungumzia afya, unagusa Wizara hii, ukizungumzia elimu kwa maana ya utendaji unazungumzia Wizara hii, ukizungumzia barabara unazungumzia Wizara hii. Kwa kweli ni Wizara yenyе majukumu makubwa.

Mheshimiwa Spika, labda nianzie na eneo la Watendaji wa Vijiji. Ningependa nisisitize tu kwamba baada ya uamuzi wa kuwaajiri Watendaji wa Vijiji na wa Kata kwa maana ya kuingizwa katika ajira ya Serikali Kuu kwa kweli tumepata tatizo kubwa ambalo tusingelitegemea litokee la kuwapatia mishahara.

Mheshimiwa Spika, hawa ni watu wanaoshika fedha nyingi, mambo mengi ya Vijiji yanapitia mikononi mwao na mambo mengi ya Halmashauri yanapitia mikononi mwao. Hawa ni watu wazima wenyе familia, lakini kwa muda mrefu hawapati mishahara yao. Mshahara ni haki ya mtu, mshahara ni uhai, hao wengi wanasomesha watoto, wana matatizo ya binadamu kama afya, lakini wanapokaa miezi kumi na kitu hawajapata malipo, kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Mwaka jana Bunge hili lilipitisha fedha lakini kwa sababu tusizoelewa hawakulipwa zile fedha.

Mwaka huu tena zimeombwa fedha. Ni imani yangu kwamba hazitakwenda kwenye njia nyingine na watalipwa haki zao zote. Zile za awali zilipwe mara moja na hizi nyingine zilipwe kila mwezi kama mishahara mingine yote inayolipwa. Sioni ni kwa nini mshahara wa mtu uweze kuwekwa afanye kazi kwa kujitolea. Serikali inatakiwa kujitolea, sio mtu kujitolea. Kwa maana hiyo, ningependa kabisa hili eneo la Watendaji wa Vijiji liangaliwe sana pamoja na kwamba fedha nimeziona kwenye bajeti, lakini uhakika wa kutolewa naomba niusisitize.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kugusia eneo la Utawala Bora. Katika eneo hili, kwanza nirudie ile hoja, niisisitize na kwa kuwa mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, hiki kilichoko katika kitabu cha Dar es Salaam kwa kweli kimetustua; mara nyingi tunapoambiwa kwamba CCM itashinda inawezekana sasa tumepata ushahidi wa kwamba inashinda kwa kutumia mbinu zilizo mafichoni kama ilivyo hapa. Katika kitabu cha Serikali inapoandikwa kwamba tunatenga fedha kuwashudumia Makatibu Tawala Wasaidizi katika kumsaidia Mheshimiwa Kikwete, inatutia wasiwasi mkubwa na huu si mfano wa Utawala Bora hata kidogo. (*Makofi*)

Utarala Bora ni kutoa haki kwa Vyama vyote hata kama vingekuwaje, vipate uwanja ulio sahihi. Ningependa Mheshimiwa Waziri atusaidie baadaye katika majibu yake, ni kwa nini katika taarifa ya Dar es Salaam Mheshimiwa Kikwete anaingizwa? Tunajua Mheshimiwa Kikwete ni Waziri, fedha hizi zingeingia kwenye Wizara yake, tusingekuwa na mashaka kwa sababu yeje ni Waziri.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zingeliingia hata kule kwenye Ofisi ya Rais tusingekuwa na mashaka kwa sababu tungejua kwamba labda kuna mambo ya kusaidia. Lakini inapoingia kwenye Mkoaa, na kifungu kilichotumika ni 3110304 na iko katika Mikoa yote na kifungu hiki kinaonekana kwa vitu hivi hivi ambavyo viko Dar es Salaam, labda inawezekana hatuna uhakika kama Mikoa mingine nayo imeandika isipokuwa imesahau tu jina la Kikwete. Tunataka uhakika na tunataka maelezo ya kina ni kwa nini huyu Mgombea anapewa nafasi na kutengewa Shilingi 20 milioni kutoka kwenye kodi ambayo sote tunalipia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Utarala Bora, ningependa pia nigosie suala la kesi zinazohusu Halmashauri zetu mbalimbali. Ni kweli wizi unatokea mambo mengi yanapotea na watusika wanapelekwa Mahakamani. Lakini uzoefu tuliuopata ni kwamba kesi hizi nyingi baada ya kuzipeleka, ushahidi huwa haupelekwi. Mheshimiwa Waziri ni shahidi, kule kwetu Karatu kuna watu waliwasimamisha na kweli wamepelekwa Mahakamani. Lakini bahati mbaya sana hati zote muhimu za ushahidi hazipelekwi Mahakamani. Serikali ni moja, kosa hili labda kimsingi si la Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa sababu kwa upande wa kupeleka vielelezo ni Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna kesi ambazo zimetupiliwa Mahakamani na tunafurahi na tunamshukuru Mheshimiwa Chiligati kwa msaada wake mkubwa aliotupatia. Amefuatilia, Polisi wanashangaa kwamba hata Hakimu wakati wameomba ushahidi amekataa kuwapa Rufaa. Sasa Serikali ni ile ile moja, Hakimu anakataa kuwapa Polisi. Lakini Hakimu naye anasema, Polisi hawakupeleka ushahidi Mahakamani, faili lilikuwa tupu. Sasa lilipelekwa nini Mahakamani? Mheshimiwa Waziri atusaidie katika hili. Serikali inasimamia vipi watendaji wake na tumegundua hata pale wanapokwenda kutetea, ushahidi mwangi unatolewa na wenyewe watendaji, lakini tumegundua kwamba kumbe na watendaji wakienda huko wanaacha makusudi kutoa ushahidi fulani na matokeo yake ni kwamba kesi hizi sasa zinafutiliwa mbali na watusika wanarudi.

Nina kesi iliyo hai na mmoja amekwishaachiwa na Mahakama na amerudi na sasa anataka arudi kwenye ajira. Lakini taarifa iliyoletwa kwetu sisi na Polisi ni kwamba Mahakama imekataa kutoa faili ili hukumu hiyo waweze *kui-appeal*. Ni kesi inayomhusu bwana mmoja Mtendaji wa Kata anaitwa Bwana Anni Sule. Tusipoangalia haki za wananchi, fedha nyingi za wananchi zitaendelea kunyonywa, wakati huo tunaendelea kukopa fedha zinazotoka nje kumbe zilizoko ndani tunaacha ziendelee kumezwa na watu na sisi hatuchui hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii inahusika pia na hati chafu pamoja na hati isiyoridhisha. Ni kweli kwamba tumefanya hatua kubwa, hati bora zimeanza kuongezeka. Lakini kwa uwiano, haziridhishi bado. Hata zile chache hatuelewi ni kwa nini bado zinaendelea kuwa chache. Serikali imekwishaahidi Mtendaji wa Serikali akifanya makosa anashughulikiwa. Lakini utaratibu wa kushughulikia wale ambao kwa makusudi hawatekelezi wajibu wao, hatuoni kama ina hatua yoyote ambayo inakwenda mbele mpaka unapiga kelele na hata unapiga kelele sana lakini baada ya kelele sana hakuna kitu kinachofanyika.

Tunaomba katika hili, Serikali iwe makini na Waziri awe makini zaidi ili tuweze kuona kwamba hati hizi chafu ambazo ni mabilioni ya fedha na wakati huo huo tunakopa mabilioni na wakati huo huo mabilioni yanapotea. Nadhani tuna tatizo kubwa katika kutokufuatalia mali zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kitu juu ya Sekta ya Elimu. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa katika mpango wa MMEM. Lakini katika mpango wa MMEM tusipoangalia tutakuwa tumezalisha bomu. Tunafurahia wakati huu jinsi tulivyoendelea ni sawa na Maaskari ambao wanataka kuteka nchi, wameteka Mji mmoja, wameteka Mji wa pili, Mji wa tatu wakaanza kula karamu. Sisi sasa tuko kwenye hatua hiyo. Tutasherehekea lakini tuna matatizo makubwa kabisa katika mpango wa MMEM. Pita popote!

Mimi nimepita kwenye Wilaya zisizopungua 70 katika nchi hii kila mahali, unakuta kuna matatizo, Walimu hawana nyumba za kutosha. Lakini tumewaongezea mzigo mkubwa Walimu, wana idadi kubwa ya watoto lakini wakati huo huo maslahi ya Walimu nayo hayaongezeki kwa kiwango hicho.

Sasa unakuta Mwalimu anapaswa kufundisha hata mbili kwa siku. Mwalimu anafanya kazi asubuhi na jioni bado hatuna kiwango chochote maalum tulichompangia Mwalimu huyu, hatumpi motisha pamoja na kwamba dalili ilioonekana ya watoto kufaulu, nina hakika tunasema idadi imeongezeka lakini ukitazama ni miaka saba nyuma ndiyo imeleta matunda, sio hii ya sasa tunayofanyia kazi. Hii ya sasa tutaiona katika miaka inayokuja na nadhani kuanzia mwaka 2007 na 2008. Kwa hiyo, tukitazama na kusema sasa tumefanya hatua kubwa tutajidanganya.

Mheshimiwa Spika, *quality* na *quantity* ni vitu viwili tofauti. Ubora wa elimu ndio kitu kikubwa kuliko chochote duniani, tusipende kutazama zaidi uwingi wa vitu, tutazame ubora wa kile tunachokifanya. Mimi napenda kuthamini ubora kwa sababu dunia hii ni ya elimu, dunia hii ni ya sayansi na teknolojia na dunia hii ni ya mashindano. Hatuwezi kwenda kushindana kama vijana wetu watapita kwa kuwa wamepita tu darasani. Kuingia darasani peke yake haisaidii kama ubora wa elimu hautakuwepo.

Lakini tuna tatizo pia katika ubora hata wa nyumba tulizojenga. Nimepata kwa njia yangu, tathmini iliyofanywa na Bwana Allen Penny ambaye amesemwa pia na Msemaji wa Upinzani na tumeisoma.

Tumesoma vile vile tathmini iliyofanywa na Hakielimu. *Quality* ya nyumba tulizojenga haiendani katika sehemu nyingi na *quality* ya fedha tulizokopa. Tumekopa mkopo mkubwa sana, ni wazi tumepata fedha za hisani, tumepata wafadhili wetu wametusaidia, lakini sehemu nyingi *quality* ya kazi iliyofanyika haiendani na ubora ambao tungeutegemea. Kama baada ya miaka mitatu, minne tena tutaanza kujenga hizo nyumba na tunalipa fedha itakuwa si kazi sahihi ambayo tumeifanya. Tungependa tathmini zote hizi ziwasilishwe kwa Wabunge waweze kuziona katika maeneo yao.

Kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba tuliambiwa sisi tuonwe na wale watu waliokuwa wanafanya tathmini, tumechengwa. Wakurugenzi mara nyingi walikuwa wanatuficha. Sina hakika ni Wabunge wangapi kama wanajua hii tathmini ilifanyika. Lakini sisi wengine tulifuatwa kwa sababu ilionekana *contradiction*. Kwangu mimi darasa waliloonyeshwa ni darasa lililotengenezwa kwa mpango mwingine, sio darasa la MMEM. Lakini imeandikwa *credit* kwamba ni la MMEM. Sasa haya ni mambo ambayo lazima tufanye uhakika na tushirikiane Wabunge na Wizara ili tuweze kujua kwamba kazi inayofanyika kweli kwa fedha tulizokopa.

Waheshimiwa Wabunge, tusipoangalia tutakuja kujuta katika mambo haya kwa sababu sisi tusipende tu kuangalia wakati sisi ndio wenye dhamana ya wananchi. Fedha zimekopwa, vitu vinajengwa kwenye maeneo yetu sisi tunafurahi lakini hatuangalii ni kitu gani kinachofanyika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kugusia eneo la maji. Katika eneo la maji nimeligusia pia kwa maandishi katika mchango wangu kwa Mheshimiwa Waziri. Ninapenda nipate jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu tunapenda kuondoa umaskini katika nchi yetu, tunakopa fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali, tunaomba hata Wabunge waombe fedha katika maeneo mbalimbali, lakini hata zinapopatikana kutumika inakuwa shida.

Sasa ningependa kujua, kwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha yuko hapa, ningependa kupata taarifa ya kina kwa sababu hatua zote tumezichukua mpaka Ofisi ya Rais. Ningependa kujua ni kwa nini maji yanayotakiwa kupelekwa hospitalini zaidi ya mwaka mmoja inashindikana. Mkuu wa Wilaya anajua, Mkuu wa Mkoa anajua, Ofisi ya Rais inajua yote haya yanashindikana na wafadhili hawa ni wafadhili wakubwa katika Wilaya yetu, wana miradi mingine nje ya huo Mradi wa Maji zaidi ya Shilingi milioni 300.

Ningependa kujua kabla hatujaharibu uhusiano wetu, napenda kujua Serikali inatoa kauli gani. Nadhani nimetoa ufanuzi. Vinginevyo nitapenda kama sitapata jibu kwenye hili, kwa kweli sitaunga hoja mkono. Pamoja na kwamba nakubaliana na hotuba ya Waziri, lakini kwa hili sitaunga hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile nigosie suala la mradi wa *Quick Start*. Mradi wa *Quick Start* ni Mahakama ulilenga kuenezwa nchi nzima ukaanzia Mkoa wa Arusha na Manyara. Mwanzo wa Mkoa wa Arusha na Manyara umechezewa na baada ya kuchezewa mradi huu sasa haujaenea kwenye Wilaya nyingine wala Mikoa mingine.

Wabunge sina hakika kama wanajua, lakini sisi kwetu tumepiga kelele sasa sijui ni mara ya ngapi nauliza suala hili. Naona kuna kurushiana mpira kati ya Wizara ya Sheria na Wizara ya TAMISEMI kwa sababu fedha hizi zilikusanya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Makatibu Tarafa. Kuna vitabu zaidi ya 149 vimepotea. Mwananchi wa kawaida au hata Mtendaji wa Kijiji akipoteza kitabu kimoja cha stakabadhi anawekwa *lock-up*. Lakini Makatibu Tarafa ambao ndio wanapaswa kuwa mfano, wamekaa na vitabu na havionezekani kwa zaidi ya miaka mitatu hawachukuliwi hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, hivi ni thamani ya mamilioni ya fedha hatujui kama viro, hatujui walikusanya, lakini nina taarifa kwamba mahali pengine fedha zilikusanya bila risiti. Sasa Katibu Mkuu amepelekewa barua nadhani zaidi ya miezi mitatu hatujapata taarifa ni kitu gani kinaendelea. Ningependa nipate taarifa kamili sasa ni kitu gani kinaendelea katika hali hii ya utata wa fedha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningegusia kwa kifupi sana juu ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na takwimu nzuri sana alizotoa Mheshimiwa Waziri, kwanza nashukuru Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Wizara yake inatoa kanuni tu halafu haifanyi mengine.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ili na mimi niweze kutoa mchango wangu wa mawazo katika Wizara hii ambayo naiheshimu sana, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha kutoa pole kwa ndugu zetu wa Kilombero kwa kuondokewa na ndugu yao mpendwa, Mbunge mwenzetu Abu Kiwanga. Napenda pia nichukue nafasi hii kutambua kwamba Chama cha Mapinduzi kimepita katika mchakato na kimempata mgombea wake wa Urais.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wote waliohusika kwa njia moja au nyingine katika utaratibu mzima. Tulikuwa na Wagombea 11 na wagombea wale walivyofanya walionyesha jinsi ambavyo demokrasi imekuwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. Hali hii inaendelea kwa Vyama vyta Upinzani na hii inaonyesha kukomaa kwa demokrasia katika nchi yetu. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete na mgombea mwenza Ndugu yetu Dr. Ali Mohamed Shein pamoja na ndugu yetu Mheshimiwa Abeid Amani Karume ambaye atatuwakilisha Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wangu leo kuwashukuru wananchi wa Jimbo la langu la Siha kuwaambia ahsante sana kwamba kwa kipindi cha miaka mitano walinipa nafasi hii adimu ya kuwakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninasema kwamba ninawashukuru sana kwa sababu nafasi hii si ya kawaida, nimeweza kushirikiana nao na sasa tunafikia hatua hii ya mwisho.

Napenda kusema hapa mambo ambayo niliyashuhudia na nitoe ushuhuda. Serikali ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa imefanya mambo makubwa katika nchi hii. Mimi sitaki nianze kuibuka hapa na *sweeping statements* kwamba hamna kitu hapa. Nataka nthibitishe kwamba katika Jimbo langu la Siha, mimi nimeyaona mabadiliko makubwa ambayo yametokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, elimu tunasema kwamba tumeweka asilimia 20 pale ndani, lakini sio asilimia 20 tu ya bajeti. Elimu inatolewa kwenye maendeleo ya jamii, kilimo, inatolewa katika Wizara mbalimbali. Mimi nataka niseme, hata kama tumefanya hivi tulivyofanya, kwa nchi ambayo imepania kuondoa umaskini tulitakiwa twende hivyo. Cuba wananchi walikuwa hawaendi madarasani, Cuba wanakaa chini ya mwembere. Walikuwa wanakwenda chini ya *Fidel Castro* wanachukua tochi, taa, jiko wanawafundisha watu Elimu ya Watu Wazima. Wape watu elimu!

Mimi ni muumini wa kina Marx mnafahamu. Marx yuko *very clear*, alikuwa anasifu Ubepari. Marx ambaye ndiye Askofu wa ujamaa nikawa *interested* nikataka nisikie anasema nini. Akawa anasifu *capitalism* akasema, naomba ninukuu: “*One good thing about capitalism is that, it develops the levels of the productive forces*”. Jambo moja zuri sana katika Ubepari Marx anasema ni kwamba inaendeleza viwango vyatitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nchi hii tunataka kuwapa watoto wetu urithi, tuwapeleke watoto Shule wakasome. Hata kama unasema hii *it-a-dilute*, pale hakuna Maabara, hakuna nyumba za Walimu *at this level*, kama unataka kuondokana na umaskini *give them education*. Tuwapatie watoto wetu elimu wasome na tumefanya hivyo.

Katika Jimbo la Siha tumeanzisha Shule za Sekondari 10 kwa mpango huu ambao nazungumza. Kama isingekuwa ni *clear policy* ya Serikali katika jambo hili tusingelikia hapa tulipofika. Napenda kusema kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha na napenda kusema kwamba Brigedia Ngwilizi sisi tunaiheshimu Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nilitoa mfano wa Grants kipindi kilichopita kwamba Abraham Lincoln alikuwa anamtumia Grants kila wakati. Akaulizwa kwa nini unampenda huyo mtu mgomvi mgomvi na nini? Kwa nini unampenda huyu mtu machachari wa ajabu ajabu? Akasema, “Kila tulipokwenda kwenye vita, Grants alihakikisha kwamba tumeshinda.” Kwa hiyo sisi kila tulipoingia katika mapambano ya kupeleka elimu, afya, huduma za jamii nilimwona Brigedia Ngwilizi akisimama na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa hatuwezi tukakaa hapa tukaanza kusema hakuna kitu pale kimefanyika. Kila mahali Tawala za Mikoa tuliona inaingia kila mahal inafanya .

Napenda kutoa ushuhuda hapa kwamba imefanyika kazi kubwa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza akatembea kifua mbele akiulizwa Rais Benjamin

William Mkapa unajivuna nini? Anasema najivuna kwa sababu nimetoa elimu kwa watoto wangu, halafu apinge mtu hiyo.

Mheshimiwa Spika, nime-overhear mambo hapa. *Political Parties* kazi yake ni ku-capture political power na political power ni kukamatwa dola. Unaposema huyu Rais amekuwa Rais, ukasema aelee hapa juu asiwe na jicho lake kule chini ni a contradiction. *Political Parties* kazi yake ni ku-capture political power. Ukishapata political power lazima sasa uwajibike kwa watu waliokupigia kura.

Rais Benjamin William Mkapa hawezi kukaa pale juu, lazima awe na jicho lake pale Hai (*District Commissioner*). Rais Benjamin William Mkapa hawezi kukaa pale juu bila kuwa na Mkuu wa Mkoa pale chini ambaye atafanya kazi hiyo. Lakini wanasema lazima kuwe na clear line of demarcation inayoonyesha kwamba hii ni Central Government na hii ni Local Government na hili jambo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa limeainisha.

Tumeambiwa kwamba DC akae pembedi pale aache mambo yaende eyes on, hand off. Mimi nimeiona hiyo jitihada inafanyika hapa sikuona tatizo lolote. Politics katika developing countries is all about allocation of resources. Ndiyo maana ya politics. Hapa hatuzungumzii mambo ya mchezo, hapa tunazungumza wewe miaka mitano unatakiwa uwaambie watu ni kwa nini hukuweza kufanya hili na lile na huna pale infrastructure, kule chini watakuchinja! Mimi nangoja siku moja nione mtu na najua kwamba ziko Halmashauri huko Sweden na kwingine ambazo zinafanya bila ya kuwa na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, lakini bado mkono wa Serikali kwa maana ya kuleta amani na utulivu, unajitokeza pale wazi wazi. Huu ndio mchango wangu. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba baada ya pale, decentralisation ilimaanisha giving more powers to the people. Wape watu madaraka zaidi. Kama ni fedha za MMEM peleka kule Kijijini, kama ni fedha za MMES peleka kule Shulen. Hii habari ya kusema kwamba zitakwenda kuliwa na nini watu watajifunza tutaweka pale system itasimamia fedha zile kuhakikisha kama zinakwenda kule. Wapelekee wananchi kule.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nisaide katika hilo na for your information mimi ninayezungumza I was once upon time a District Commission Sir. A District Commissioner is the incharge of all government affairs katika eneo linalohusika. Ukimwondoa namna hii, hakuna incharge pale, utapata matatizo makubwa. Kwa kusema hivi wala sio kwamba nataka kumdhailisha mtu nataka tu kutoa contribution yangu ya knowledge niliyonayo. Mimi ni mtu wa Political Science na Public Administration. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka nikumbushe kwamba katika nyumba hii mimi mwaka jana nilisimama hapa nikazungumzia kuhusu maombi ya wananchi wa Jimbo la Siha, kumwomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awapatie Wilaya.

Wakati nilipomaliza mazungumzo yangu, Baba Spika ukasema “Mungu ibariki nchi ya Siha.” Iko hapa kwenye *Hansard* na wewe ukatoa baraka zako zile.

Leo Mzee wangu tunaondoka na Rais alitoa ahadi tarehe 21 Machi, 1997, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja *Visitation Secondary School* na wananchi wa Jimbo la Siha walimlilia. Alikuja tena tarehe 18 Februari, 2002 tukamtumia Mzee wetu pale anaitwa Samwel Marisha akam-quote na akamkumbusha kuhusu ahadi ambayo alitoa katika Jimbo la Siha la kupatiwa Wilaya ya Siha. Leo nimekuja hapa na Biblia nataka nifanye kama Mzee Makamba lakini sitaisoma.

(*Hapa Biblia ilionyeshwa Bungeni kama kielelezo*)

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Nataka tu ni-quote, Mathayo mlango wa 14 ambapo wanamzungumzia Bwana mmoja anaitwa Mfalme Herode. Mfalme Herode alimchukua mama mmoja anaitwa Herodia. Herodia alikuwa ni mke wa Philipo ndugu yake. Mfalme huyu siku moja akaja bwana mmoja anaitwa Yohana Mbatizaji. Akamsakama sana kuhusu kitendo cha kumchukua mke wa nduguye na kitendo kile kikamuudhi mfalme mwenyewe na kikamuudhi Herodia mwenyewe.

Nitamaliza tu dakika tano zinanitosha. Ikawaudhi, kwa nini huyu anatusakama? Siku moja ya *birthday*, siku inafanyika sherehe pale, Herodia binti yake akacheza vizuri sana na baba yake akafurahi sana. Baba yake huyu wa kambo sasa akamwambia nitakupa kitu chochote utakacho. Huyo binti wakati wa kuomba hicho alichotaka kuomba, akafanya *consultation* na mama yake. Akaenda akamfuata mama yake yaani Herodia akamwambia, mama leo baba aliahidi mbele ya watu wengi sana kwamba atampa zawadi Herodia.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba wewe ni Mkristo kwa hiyo jambo hili unalifahamu na wale ambao wanamsema Nabii Issa mnalifahamu. Akamwambia, nakuomba unipe ushauri nikamwombe nini baba. Akarudi akamwambia sasa nimepata mahali pa kum-fix Yohana Mbatizaji. Nenda kamwombe kichwa cha Yohana. Basi, akarudi kule akamwambia baba nakuomba kichwa cha Yohana Mbatizaji. Yule mfalme alisikitika sana kwa sababu alimjua Yohana Mbatizaji ni mtu mwema na ni Nabii. Akajisikia vibaya kwamba ni kwa nini alifanya ahadi ile, lakini sasa jambo lile alilisema mbele ya watu. Akafika mahali akatoa maelekezo kwamba kwa vile nilisema mbele ya watu na watu wamekaa pale wanamwangalia, kikaletwa kikombe kilichowekwa kichwa cha Yohana. Ndivyo ile hadithi ilivyokwisha na ndivyo Yohana alivyokufa.

Mheshimiwa Spika, mimi simwombi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kichwa cha Yohana. Hatuwezi kumwambia na wala hatumlaumu Rais wetu kabisa. Ninachofanya hapa ni kukumbushia ahadi yake Mzee wangu kwa sababu huyu baba sasa anaondoka. Nawaombeni wazee wangu mnisaidie, pale Siha watanimaliza Nitakwenda kuwaambia nini? Mese nitawaambia nini? Ngaronyi nitawaambia nini? Nsherehehe nitawaambia nini? Kishisha nitawaambia nini? Rau-Kisangara nitawaambia nini? Wanri na Mae nitakwenda kuwaambia nini? Lekirmuni, Odonyo Moroki, Olkolili, Oli Melili nitakwenda kuwaambia nini? Naomba Mzee wangu, Brigedia wewe ni mtu mkubwa.

Umwambie Rais kwamba huyu bwana anakumbushia jambo hili. Nawaombeni wazee wangu! (*Kicheko/Makofi*)

Kama mfalme Herode, mfalme wetu hapa duniani sisi ni Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Kwa unyenyekevu mkubwa, namwomba asiondoke na namwamini, najua huyu ni mtu ambaye ni mashuhuri, ni mtu ambaye akisema jambo amelisema, nichukue nafasi hii kumwomba. *Your Excellency, the President of the United Republic of Tanzania, I request you on behalf of the people of Siha to say Yes.* Useme tu ndiyo.

Wewe Mzee wangu Spika wakati mwingine unakaimu hapa si unisaidie tu baba? Unisaide umwambie yule jamaa anakukumbushia. Naomba nikumbushie jambo hili. Nitakwenda kuwaambia nini Londrosi? Nitakwenda kuwaambia nini Ngare Nairobi? Nitakwenda kuwaambia nini kule Simba? Nitakwenda kuzungumza nini Bagamoyo? Maeneo haya ni maeneo ambayo yako nyuma.

Mheshimiwa Spika, siku ile mliniambia kwamba usilie. Mimi nasema leo nawasilisha kilio cha wananchi wa Jimbo la Siha kukumbushia ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla hajaondoka Mzee wangu. Ahadi ile ilitolewa na mtu mkubwa, Brigedia. Ukimshauri vizuri, ukizungumza naye vizuri, ukimweleza, mimi wakati mwingine namtafuta simpati. Hapa nina makabasha na nina barua nimemwandikia na kila kitu nimeshapeleka na nyinyi nimeshawaleteeni. Ninawaombeni sana mnisaidie. Mimi naunga mkono wala sisimami kwenye Kamati kupinga jambo hili. Mimi vyovyote atakavyoamua Rais kama hamtaki nirudi huku ndani mseme, shauri yenu, lakini nimelisema hapa mbele yenu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba suala la Wilaya ya Siha lisichukuliwe kwa masiara nalileta ombi hili mbele yako. Hii ndiyo nafasi yangu ya mwisho. Baada ya kusema maneno hayo ninawaombeni wazee wangu Wabunge wenzangu pitisheni jambo hili, pitisheni hii hotuba, pitisheni haya makisio kwa sababu ndani yake ndiyo vinazaliwa hivyo vitu vyote nilivyoviomba hapa. Mimi naunga mkono hotuba yako nzuri. Naunga mkono na nasema kwamba sitasimama hapa kuzuia jambo lolote. Nitaunga mkono. (*Makofi*)

SPIKA: Rais akisema neno moja tu roho yako itapona. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusaidia kupambana na

umaskini na kusukuma gurudumu la maendeleo, kwani Wizara hii ni muhimu sana na ndiyo Wizara ambayo iko karibu na wananchi kuliko Wizara yoyote ile. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi ngumu na nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe salamu za rambirambi kwa familia na ndugu wa Waheshimiwa wenzetu waliotutangulia mbele ya haki, Mheshimiwa Mussati, Mheshimiwa Kapteni Kasapira, Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria na Mheshimiwa Kiwanga. Tumwombe Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu niliyonayo leo hii ni moja tu. Hoja yenye we inajielekeza kwenye umuhimu wa kuhakikisha Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji wanapewa chochote kulingana na Sheria zetu tulizozitunga, lakini vile vile na kuangalia uwezekano wa kuboresha maslahi yao kwa njia moja au nyingine.

Sote tunafahamu na hakuna ubishi, unaposema mpango wa ujenzi wa madarasa umefanikiwa, maana yake unachosema ni kwamba, Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji walifanya kazi nzuri ya kuwahamasisha wananchi ili waweze kutoa mchango wao. Ndicho kitu unachosema! Unaposema kwamba *TASAF* imefanikiwa, maana yake unasema kwamba Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji walifanya kazi nzuri. Unaposema kwamba Sensa ilifanikiwa, maana yake unasema Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji walifanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Unapobuni mradi wowote ule wa maendeleo na ukasema lazima mradi huo utekelezwe katika ngazi ya Vijiji na Vitongoji, unachosema, unaamini Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji watafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika uchumi, huwa kuna kitu kinaitwa *opportunity costs*. Nitatoa mfano. Ukienda kuangalia mpira uwanjani, kuna ile gharama unayolipa kuingia kwenye uwanja kuangalia mpira. Hiyo ni gharama, Wahasibu na watu wengine huwa inawahangaisha sana. Lakini mchumi hana muda wa kuangalia hilo. Mchumi anaangalia gharama utakayoingia kwa kutofanya shughuli nyingine.

Ukiwa unaangalia mpira, kwa sababu huwezi ukawa unazalisha, kwa hiyo mchumi hana sababu ya kujua ni kiwango cha Shilingi ngapi utalipa. Hiyo ni kazi ya Wahasibu, mchumi anaangalia *opportunity costs*. Sasa hawa Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji wanapokuwa wanasmamia shughuli za maendeleo ipo *opportunity costs* kubwa, kwamba kama alikuwa na shamba ambalo alitakiwa kulima, hata kwenda shambani kulima, kama alitakiwa kuangalia mifugo yake hataangalia mifugo yake. Sasa hii gharama kubwa isiyoneka moja kwa moja, ni nani anaifidia kwa njia moja au nyingine?

Ndipo inakuja umuhimu sasa wa kuangalia Wenyeviti hawa wa Vitongoji na Vijiji ili kazi kubwa wanayoifanya na gharama kubwa wanayoibeba kwa kutofanya shughuli zao nyingine za maendeleo katika ngazi ya familia, basi si vibaya tukianza kufikiri jinsi ya kuwaenzi na kuwapatia chochote kwa nia ya kutambua mchango wao.

Haitoshi kusema hapa Bungeni kwamba kazi nzuri wanafanya; haitoshi kusema kwamba Wenyeviti wetu ni wazalendo; haitoshi!!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda nichukue nafasi hii kutoa sababu kumi za kwa nini nafikiri hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wafikiriwe na tuhakikishe wanapewa chochote kama shukrani yetu kwao kwa kazi nzuri wanayofanya kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kwanza, hawa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji kwanza wanatambulika kisheria. Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 ilishaagiza huko nyuma kwamba asilimia 20 ya mapato yote yatakayokusanywa kwenye eneo husika, basi itakwenda kwenye Vijiji na Vitongoji kwa nia ya kuwawezesha hawa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji angalau kupata sabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo tulilonalo ni kwamba, kuwa na Sheria ni jambo moja na kuitekeleza Sheria ni jambo lingine. Natambua kwa sababu nipo kwenye Kamati ya Serikali za Mitaa, tatizo kubwa ambalo limekuwa likitukabili na kila siku tukiziagiza Halmashauri ni kuhakikisha zinarejesha asilimia 20 ya mapato ya Halmashauri yaliyotokana na Vijiji. Kwa hiyo maeneo mengi hazirejeshwi kwa sababu fedha ikashakusanywa ni ngumu sana kuirejesha tena kwa wananchi. Ndiyo tabia ya Serikali kote duniani, kwamba fedha ikishakusanywa, kuirejesha inakuwa ngumu.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunayo sheria nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri anaweza akasimama hapa akasema, tulishaweka Sheria, ipo kuhakikisha asilimia 20 ya mapato yanarudi huko kwa ajili ya sabuni na posho kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Ukweli wa hali halisi kinachotokea ni kwamba, fedha hizo hazirudi na ukweli mwingine ni kwamba fedha ikashakusanywa ni ngumu sana kurejeshwa tena kwa kazi hiyo.

Kwa hiyo, ukiangalia Sheria utaona kwamba mambo yako sawasawa, lakini ukienda kwenye *ground* utakuta mambo hayako sawasawa. Ni Bunge hili pekee ambalo linatakiwa lione hali hiyo na liishauri Serikali kufanya marekebisho ili tuwawezeshe hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji angalau kuweza kupata sabuni. Kwa hiyo, nalisema hilo kwamba Sheria ipo na tunaitambua, lakini utekelezaji wake ni asilimia sifuri mpaka 20 wanapotitahidi. Lakini maeneo mengi fedha hizi hazirejeshwi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, kama Serikali imeona umuhimu wa kuhakikisha Wenyeviti Watendaji wa Vijiji na Vitongoji, wanalipwa mishahara moja kwa moja na Serikali Kuu. Sioni kama ni jambo baya kama Serikali hiyo hiyo ikitumia busara hiyo hiyo kuhakikisha hii asilimia 20 ambayo walitakiwa wapate hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji itoke Serikali Kuu na kwenda moja kwa moja kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili waweze kupata haki yao kama ambavyo tulishaona umuhimu wa kuweka Sheria.

Sababu ya tatu, nilishaieleza katika utangulizi kwa hao Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, wanafanya kazi ngumu na hakuna anayelipinga hilo. Kazi ngumu maana yake ina gharama yake, Wachumi tunasema *opportunity costs*. Kwa hiyo, hatutakiwi kufumba

macho na kuacha mambo yaendelee, kwa sababu tukiachia siku moja tutakuja kukosa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji na maana yake Sera zetu nzuri tulizonazo za kuhakikisha tunapambana na umaskini Vijijini hazitatekelezeka na zitakwama kwa sababu ndogo ambayo tungeweza kuirekebisha.

Sababu ya nne, kama nilivyosema, wanasimamia miradi ya maendeleo. Lakini sababu nyingine ya tano ni kwamba asilimia 20 ambayo tulikuwa tunesema kwamba lazima iende kule, haiendi. Huo ni ukweli, ukiangalia hata mahesabu ya Mkaguzi wa Serikali za Mitaa yanaonyesha wazi Halmashauri karibu zote zinadaiwa pesa nyingi za Vijiji.

Lakini sababu ya sita ni kwamba, unapokuwa kwenye Mikutano ya hadhara, unaeleza jinsi mapato ya Serikali yalivyoongezeka kutoka bilioni 25 mwaka 1995 kwa mwezi hadi bilioni kati ya 150 mpaka 155 kwa mwezi. Huyu Mwenyekiti wa Kijiji na Kitongoji anakutazama sana anasema Mheshimiwa Mbunge sawa nimekuelewa, sasa baada ya haya mapato kuongezeka namna hii, hamwezi kutufikiria. Sasa hoja ya mapato kwa kweli ni ngumu kuitumia kuwaambia hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kwamba hatuwezi kuwalipa hiyo asilimia 20 kwa sababu mapato ni kidogo. Ni ngumu!

Kwa sababu unapoelezea kwamba kuna mafanikio ya utekelezaji wa Ilani, kuna mafanikio yaliyopelekea kuongezeka kwa mapato ya Serikali, huyu Mwenyekiti wa Kijiji na Kitongoji ambaye ameshiriki katika kuwezesha mafanikio hayo, hakuelewi kama mwisho wa siku hanufaiki moja kwa moja na mapato hayo. Nasema hanufaiki moja kwa moja kwa sababu unaweza ukasema Shule ikijengwa na yeze Mwenyekiti wa Kijiji atanufaika, barabara zikijengwa Mwenyekiti wa Kitongoji atanufaika. Ndio, lakini hapa dhana ni kwamba, huyu ana jukumu kubwa zaidi analolifanya na kwa sababu hiyo, yeze kama binadamu lazima aone anavyonufaika moja kwa moja na mafanikio hayo na hiyo ndiyo maana ya utawala bora.

Kwa hiyo, hoja pekee ambayo unaweza ukaitumia kutoendelea kuwafikia Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji ni kwamba, maana ya kwenye uchumi huwa tunasema siku zote fedha hazitoshi na kwa hiyo, lazima kuhakikisha kwamba unakuwa na *preferences* na *una-make choices* kwamba lazima ufanye maamuzi na uamue unaanza na kipi, unamliza na kipi. Kwa hiyo, kama unamwambia Mwenyekiti wa Vijiji na Vitongoji kwamba mapato yameongezeka, lakini bado hatujaona umuhimu wa kukupa chochote maana yake unamwambia unapoweka *preferences* za Serikali, huyu Mwenyekiti wa Kitongoji anakuwa chini sana kiasi kwamba hafikiwi kuingizwa kwenye utaratibu huo.

Sasa nasema, ukifikiria hivyo Mwenyekiti huyu wa Kijiji na Kitongoji atakudharau na ataona unachosema kwamba mchango wako unatambulika, ni maneno tu ya kumfurahisha, lakini ukweli ni kwamba hautambuliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, tunaposema utawala bora ni pamoja na kugawana vizuri mapato yanayopatikana. Haiwezekanai tukawa na watu tunaoshirikiana nao kuzalisha, lakini mwisho wa siku tunapokuja kwenye mapato, tunawaacha moja kwa moja.

Sasa utawala bora usiishie kwenye kufunga suti na kwenye majukwaa na *conferences* ya kimataifa tu, twende mpaka kwenye Vijiji na Vitongoji tuwafikirie Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili waweze kuelewa kwamba tunaposema utawala bora tunamaanisha kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unaweza ukawa challenged, ukasema mbona Serikali za Vijiji zinaweza kukusanya fedha, lakini tutakuwa tunajidanganya kwa sababu Bunge hili tumeshapiga marufuku kodi nyingi zisikusanywe na kwa sababu hiyo Serikali za Vijiji tumeziondolea uwezo wa kuweza kuamua wazikusanye kwa ajili ya Wenyeviti wao wa Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi tuliopo hapa Dodoma ndiyo tumeondoa uwezo huo, lazima tuwe wa kwanza kuhakikisha tunawezesha Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema, kama tutahakikisha hii asilimia 20 au zaidi ya hapo au tukiweka utaratibu mzuri wa kuwezesha Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji wanapata posho yoyote, basi tutaweza kuwapa ari mpya ya utendaji kazi na kwa sababu hiyo, falsafa yetu mpya ya kuanza kazi kwa ari mpya, kwa nguvu mpya na kasi mpya. Naomba tuipeleke mpaka Vijijini na katika Vitongoji tuwawezeshe hawa kwa posho kidogo ili na wao waweze kufanya kazi kwa ari mpya, kwa nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. NJELU E. M. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwanza kwa kuwasilisha hoja vizuri ambayo ni nzuri sana na vile vile, nimpongeze yeye pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wao wote kwa kazi nzuri za jumla ambazo wanazifanya katika Wizara hiyo.

Baada ya kusema hayo, nina maombi mawili ya mwanzo. La kwanza, limeshazungumzwa na wenzangu, lakini nilitaka niliseme tu kwamba hao Ma-WEO Vijijini wamekuwa kwa muda mrefu hawajalipwa mishahara yao na wenzangu wamelisema hapa. Lakini sisi katika Kamati ya Fedha tulipokuwa tunamwuliza Waziri wa Fedha, alisema fedha zimetolewa zimepelekwa kwenye Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa.

Sasa mimi ningependa kujua, hizo fedha mmeshazipokea na wanalipwa sasa au hapana? Kwa sababu Waziri wa Fedha alisema hela zimetumwa na watakuwa wamelipa malimbikizo yao yote kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Sita.

Sasa tunataka tujue kama hizo hela mmeshazipokea na mnawalipa. Kwa sababu siyo suala la kuingiza kwenye Bajeti, za Bajeti ni msimu ujao lakini za malimbikizo ya

nyuma, Wizara ya Fedha imesema imekwishatoa na tungependa hao Ma-*VEO* wote na Ma-*WEO* wote wanaostahili kulipwa walipwe katika kipindi hiki.

La pili, katika Ibara ya 62, Mheshimiwa Waziri umezungumzia taratibu za kuweza kugawa Kata au kuandikisha Vijiji. Sisi tulileta mapendekezo ya kugawa Kata katika Wilaya ya Chunya, Kata ya Chalangwa, Kata ya Makongorosi, Kata ya Mkwajuni na Kata ya Galula.

Nilipofika Wizarani mwaka jana wakaniambia kwamba kulikuwa na nyaraka fulani zinakosekana katika mafaili kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako. Nilipoongea na Mkurugenzi wa Halmashauri yangu akazileta zile nyaraka lakini toka wakati ule hatujapata jibu lolote. Sasa maadamu tulishatimiza taratibu zote ambazo zinatakiwa, nini kinazuia hizo Kata zisigawiwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Chunya ni kubwa sana na Tarafa zake ni kubwa na Kata zake ni kubwa. Ma-*WEO* wetu wanapata shida sana kuzitembelea kutoka Kijiji hadi Kijiji kingine na hawana usafiri na sehemu nyingine wanapata hakuna watu. Wilaya kubwa ina maeneo mengine hakuna watu, inabidi apite kwa wasiwasi kukutana na simba, nyati na wanyama wengine. Kwa hiyo, tungeomba hizi Kata zigawiwe ili tupunguze tatizo kwa hawa watendaji wetu.

La tatu, hili nalichukua kutoka katika Ibara ya 41 linalohusiana na Utawala Bora. Kwanza, napenda niipongeze Wizara kwa *ku-improve* mahesabu kwa kuboresha mahesabu ya Halmashauri za Wilaya kwamba sasa Halmashauri 39 ziliweza kupata hati safi na nyingine 50 zikapata hati zenye masharti.

Mheshimiwa Waziri, lakini hakutaja Halmashauri zilizopata mahesabu machafu 27. Hizo zilipata hesabu chafu nazo ni 27 na katika hizo mmoja wao ambayo ni Wilaya ya Misungwi mahesabu yake kwa maelezo ya Ma-*Auditor* yalikuwa ya hovyo, kiasi kwamba hata *ku-form opinion* walishindwa. Wilaya nyingine ya Mtwara Mikindani, hata kuwasilisha mahesabu kwa Wakagazi walishindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujuu Wizara inachukua hatua gani kwa watu wa namna hiyo? Kwa sababu sio vyema tu kusema kwamba *tume-improve* hapa ingawaje bado. Hata hivyo bado. Tunachotaka ni kwamba baada ya maboresho yaliyoanzishwa, haya tunatazamia kwamba Halmashauri zetu ziwe na mahesabu mazuri ili hela wanazopelekewa na kazi wanazozifanya ziweze kufanyika vizuri zaidi.

Lakini sasa ukisoma taarifa za Mkaguzi ni mbaya sana katika Halmashauri nyingi, hata juzi tulipata hati za masharti, mahesabu yao na maelezo yao ni mabaya sana. Sasa Wizara inachukua hatua gani kwa maana ya kuboresha, kwamba baadaye ziwe na hali nzuri?

Lakini pia kwa wale ambao walizembea wamefanya kwa makusudi kabisa. Mnachukua hatua gani? Hawa ambao hawakupeleka hata mahesabu, hawa ambao

mahesabu yao ni ya hovyo mno kiasi kwamba Mkaguzi anashindwa hata ku-form opinion, Wizara inachukua hatua gani?

Lakini pia katika wale waliofanya vizuri ningependa kuipongeza Mikoa miwili, Mikoa wa Kilimanjaro na Mikoa wa Dar es salaam ambayo Halmashauri zao zote zilipata hati safi zote katika Mikoa ile miwili. Lakini pia kuna Mikoa, ukichambua zile hesabu kuna Mikoa ambayo hakuna Halmashauri hata moja iliyopata hati safi. Mikoa wa Lindi, Halmashauri zote, hakuna iliyopata hati safi. Mikoa wa Manyara hakuna hata Halmashauri moja iliyopata hati safi. Mikoa wa Mtwara hakuna hata Halmashauri moja, Mikoa wa Shinyanga hakuna hata Halmasahuri moja, Mikoa wa Singida hakuna hata Halmashauri moja na Mikoa wa Tabora. Wote hapa wamepata hati zenye masharti ama hati chafu katika Wilaya hizo.

Sasa Wizara inafanya nini? Inachukua hatua gani kuweza kuhakikisha kwamba mambo kama haya hayajirudii tena? Ni muhimu sana, kwanza inawezekana kukawa na tatizo la Wahasibu. Tunajua Halmashauri nyingi zina tatizo kubwa sana la Wahasibu. Sasa ninyi katika Wizara mnazisaidia vipi Halmashauri kuondokana na tatizo la upungufu ama ubovu ama kutokuwepo kwa Wahasibu wenyе sifa zinazostahili?

Kwa sababu katika hili suala, najua inawezekana mnawa-*train* watu, lakini *training* kama unam-*train* mtu ambaye *basic education* ya mwanzo haina nguvu, siyo nzuri, hata ukimpeleka kwenye kozi ni vigumu sana kuja *ku-cope* na mambo ya sasa. Ni vizuri mkawa na utaratibu, tujue mnaajiri kila mwaka Wahasibu wangapi ili waweze kuimarisha Halmashauri zetu za Miji, Jiji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda pia sasa baada ya kuzungumzia hayo, nizungumzie suala lingine ambalo nilizungumza mwaka 2003 ambalo linahusiana na Utawala Bora, pia ambalo linahusiana na nidhamu na linahusiana na kutambua ngazi za madaraka.

Natolea mfano wa Chunya. Kule Chunya kuna mwananchi mmoja aitwaye Ramadhan Kadu, alinyang'anya mbao zake na Mkuu wa Wilaya na sababu ya kumnyang'anya ni kwamba walimkuta na mbao nyingi. Sasa kuwa nyingi, maana yake nini sijui! Walikuta mbao wakasema ni nyingi zikakamatwa. Walipompeleka kwenye Mahakama, Mwanasheria wa Serikali (*DPP*), akasema hana kesi ya kuendelea na mtu huyo, yaani *Nolle prosequi*. Aliporudisha wao wakasema haiwezekani huyu mtu ilibidi apatikane na hatia. Wakasema haiwezekani, wakabisha, kwa lugha nyingine wakakaidi.

Kwa hiyo, kikao cha Halmashauri ya Wilaya cha Madiwani nilijaribu kuelezea kwamba suala hili *DPP* akisharudisha akisema hana kesi, basi mnaacha mpaka mtakapopata labda ushahidi mwingine baadaye labda mnawenza mkaanza upya.

Lakini pale pale lazima muache, wakasema haiwezekani. Nikaja nikalizungumza hapa mwaka 2003. Waziri Masilingi baada ya kulielewa akaagiza kwamba mbao zirudishwe mara moja na ninayo Hansard hapa ilikuwa tarehe 15/07 2003 kwenye hoja

ya Waziri Mary Nagu. Hata baada ya agizo hilo, *DC* akakaidi akasema, haiwezekani, akabaki na zile mbao. Baadaye faili wakarudisha tena kwa Mwanasheria.

Baada ya mawasiliano Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akaagiza kwamba mbao zirudishwe, hakuna kesi ambayo Serikali inataka kuendelea nayo, wakakaidi. Wewe mwenyewe Waziri baadaye ukatoa agizo. Nilipozungumza na wewe ukaniambia umetoa agizo. Ukatoa agizo kwamba zile mbao zirudishwe. Sasa nakwambia mbao hazijarudishwa mpaka sasa, pamoja na maagizo yote.

Tarehe 16, mwezi huu nilipokuwa naongea na wewe pale nje, nikakwambia mbao hazijarudishwa ukasema nilishatoa agizo. Nikasema pamoja na agizo, lakini yule mtu bado hajarudishiwa mbao, ukasema labda aende Makakamani.

Sasa mimi najiuliza sikuelewa maana yake nini, aende Mahakamani kwa nini? Unataka kusema nini wewe mwenyewe? Unataka kutuambia kwamba umeshindwa? Maana yake sikuelewa mimi. Umeshindwa kwamba sasa huyu *DC* hawezekaniki, huna la kufanya zaidi ya hapo, ye ye ameisha kuwa mbabe zaidi kwamba sasa nendeni Mahakamani?!

Mheshimiwa Waziri, nilishindwa kukuelewa Mheshimiwa kwamba aende Mahakamani! Hili suala liko mikononi mwako, liko ndani ya uwezo wako. Sasa kusema aende Mahakamani, akafanye nini? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naomba uongee na kiti badala ya Waziri.

MHE. NJELU E. M KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, namweleza Spika. Hili suala lipo ndani ya uwezo wa Waziri. Kilichotakiwa ilikuwa ni kukazia agizo la Waziri Masilingi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora, kukazia agizo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kukazia agizo lake ye ye mwenyewe kwamba tunataka utekeleze maagizo tuliyokupa. Sasa ukituambia aende Mahakamani, ni kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshindwa, Waziri Masilingi ameshindwa, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ye ye ameshindwa.

Kwa hiyo, huyu Bwana hawezekaniki, nendeni Mahakamani. Ni utaratibu wa wapi? Angekuwa mtu huyu hayuko ndani ya Wizara yako ningeelewa. Lakini sasa yuko ndani ya Wizara hii, ni vigumu sana mimi kukuelewa.

Mheshimiwa Waziri, lakini pia kama ukishindwa, tuchukue kwamba utasema umeshindwa kukazia agizo lako wewe mwenyewe. Agizo la Mahakama nani atakazia? Kwa Sababu Mahakama inaweza kutoa amri lakini anayekazia ni *Executive*.

Mahakama huwa inatoa tu amri kwamba iwe hivi, lakini wanaokwenda kutilia mkazo agizo hilo, amri hiyo ya Mahakama ni *Executive*. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile itarudi kwako tena utilie mkazo. Kama hukuweza kukazia mkazo, sasa nani atakayetilia mkazo hapo baadaye?

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, mimi naamini kwamba hili suala liko kwa Wizara yako na mwenye mamlaka ya kulitolea uamuza na kulimaliza ni wewe mwenyewe katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa.

Kwa hiyo, naomba utupe maelezo leo ya mwisho kwa sababu imeishachukua miaka miwili na huyu bwana alikuwa anajenga nyumba ya wageni ndiyo maana akakusanya zile mbaao na tangu walipomnyang'anya mbaao zake na nyumba ya wageni ile hajamaliza mpaka leo.

Wakaanza kuzusha maneno, Kasaka na yeze ana mbaao mle ndiyo maana anamtetea huyu mtu. Nataka nitamke hapa leo kwamba mimi sina ubao hata mmoja kwa mtu yule na wala kabla hawajakamata mbaao zake sikujua kama alikuwa na mbaao. Lakini mimi kama Mbunge, mtu anapooneewa bila sababu, ninajiona ninao wajibu wa kuliweka hili suala bayana ili Serikali ione kasoro ziko wapi na ichukue hatua za kumrekebisha huyu bwana na mbaao zile zirudi kwa mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nimeshangaa sana kwamba anatoa halafu *DC* anashindwa kutekeleza. Nitoe mfano jinsi ya umuhimu wa watu hawa, wanasheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kule Marekani miaka ya 1970, wakati Nixon alipokuwa na kesi ile ya *Water Gate*, alipopeleka Makachero wake kwenye jumba la *Water Gate*, Bunge lilianza kuchunguza ile kashfa na liliomba lipewe nyaraka na *tape* za Ikulu ili liweze kuthibitisha kama madai yale ya tuhuma zile ni ya kweli ama siyo ya kweli. Rais Nixon akakataa, lakini aliyemuamuru atoe zile *tape*, alikuwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Marekani. Akasaini *order* ya kumtaka Rais Nixon atoe zile *tape* na akazitoa na ndiyo maana waligundua kwamba kumbe kweli alipeleka Makachero kule *Water Gate*.

Sasa leo sisi Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatoa agizo, *DC* anakaidi kwa mwaka mzima na tunafika mahali tuanze kusema kwamba nenda Mahakamani; Mahakama itafanya kitu gani? Angekuwa ni mtu ulikuwa unasuluhisha mtu wa nje ambaye sio mtumishi wa Serikali, tungelewa. Lakini ndani ya Watumishi wa Serikali, haieleweki!

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili suala leo tupate ufumbuzi wake ambaao uwe ni wa mwisho tusiendelee tena kuvutana kwa kitu ambacho tayari kilishatolewa maagizo na wewe mwenyewe na sasa hivi kinachotakiwa ni wewe kutilia mkazo na suala hilo liishe tulisahau tuangalie mambo mengine huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipenda nizungumzie masuala haya ili Waziri atakapokuwa ana-*wind-up* aweze kunipa maelezo. Mimi sina tatizo na hoja yake. Hoja yake ni nzuri, Wizara yake inafanya kazi nzuri. Wanajitahidi sana kuimarisha Halmashauri zetu.

Katika programu zetu za maboresho mnaimarisha Halmashauri vizuri ila hili suala la kufunza Wahasibu na baadhi ya Watendaji muhimu katika Halmashauri zetu, hilo mlilitie mkazo kwa sababu mpaka sasa bado hali ni mbaya. Wenzangu mmeshayazungumza hapa, kwa kweli baadhi ya utekelezaji wa MMEM katika Halmashauri zetu bado ni mbaya. Baadhi ya majengo yaliyojengwa hayana sifa zinazolingana na fedha zilizotumika. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa ningependa nitumie nafasi hii, kuungana na Wabunge wenzangu walionitangulia kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao Hayati Abu Kiwanga. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, ningependa nitumie nafasi hii kuwapongeza wenzetu wana CCM 11 walijitokeza kugombea nafasi ya Urais chini ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu kwa kufanya hivyo wameboresha mchakato wa demokrasia katika nchi yetu. Tufikirie kama wasingejitokeza. (*Makofi*)

Katika hili, tatu, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na wana CCM kugombea nafasi hii ya Urais wa nchi yetu na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Mgombea Mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kugombea nafasi ya Urais kwa awamu ya pili. Wote tunawataki mafanikio mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo ningependa nipongeze Wizara hii kwa hotuba hii nzuri kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii ya TAMISEMI. Lakini kwa sababu mengi yamesemwa labda mimi nijikite kwenye mambo makubwa matatu. Moja ni lile lililoko ukurasa wa 24 kuhusu matumizi bora ya ardhi, pili, Sera ya Maendeleo Vijijini na tatu uanzishwaji wa Miji Midogo, Miji, Manispaa na kadhalika kama ilivyo katika ukurasa wa 36. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili badala ya kutumia muda mrefu ningependa nitoe tahadhari kwamba Watanzania, tukikiuka misingi, misingi itatukiuka. Suala la *urbanization* au kukua kwa Miji katika nchi yetu sasa haliwezi kuepukwa. Kwa mfano, Wilaya ya Njombe hivi sasa ina Vijiji zaidi ya 20 vyenye ukubwa wa *size* ya Kibaigwa hapa jirani viko Vijiji vya Kifanya, Uwemba, Mtwango, Illembula, Kidugala, Makoga na kadhalika vyote hivi vina ukubwa kama wa Kibaigwa. Suala la kuijuliza hapa ni kwamba, je, Sera ya Miji ni nini kwa siku zijazo katika nchi yetu? Je, unaweza kuwa na Miji 20 ndani ya Wilaya moja? Kwa kuwa tunaanza sasa ni vizuri tukaanza kutazama na kujifunza kwa wenzetu walioendelea. Hilo ni pendekero la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekero la pili, kutokana na uzoefu wetu wa kuunda Miji au Miji Midogo na matatizo tunayoyapata kusubiri Wilaya au wahusika waombe tufuate kama Waziri, alivyoanza sasa kwamba Wilaya yoyote yenye watu zaidi ya 300,000 igawanywe. Kwa kutumia utalaamu huo huo kwa sababu hakuna taarifa ambazo kwa dunia ya kisasa unaweza kushindwa kuzipata kuhusu idadi ya watu, ukubwa wa

eneo, jiografia ya eneo, napendekeza kwamba tuunde Kamati ya wataalam wa kudumu ndani ya Wizara watakaokuwa wanakagua nchi nzima na kupendekeza kwamba kijiji X kinafaa kuwa Mji Mdogo, Wilaya X inafaa igawanywe, Mkoa X unafaa ugawanywe badala ya kusubiri maombi yatoke huko.

Kwa njia hiyo, itashirikiana na wataalam hawa, Wizara ina-*initiate* wazo au Mkoa halafu wanakaa pamoja na kuamua kuliko kusubiri mambo yatoke upande mmoja kwa sababu hii ni nchi yetu wote.

Kwa mfano, kama watu wa Mkoa wa Arusha, wasingeleta maombi ya kugawa Arusha uwe Mikoa miwili, je, Serikali Kuu ingenyamaza tu kwa sababu hawajaleta maombi? Tujifunze kutokana na hilo ili kuzuia miji yetu isiwe Soweto. Miji inaharibika kwa sababu ya kusubiri mambo kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipaka ya Wilaya zetu na Mikoa iliekwa na wakoloni. Lakini kwa kuwa ni nchi moja na huru, huu ni wakati mzuri wa kuangalia baadhi ya maeneo ambayo yaligawanywa na wakoloni kwa makosa au kwa kuangalia tu labda makabila. Leo utakuta eneo la Wilaya limepindapinda kama nyoka. Unapita kwenye Mkoa X unaingia kwenye Mkoa mwingine tena kwa watu wale wale. Kwa mfano, kuna wakati mimi nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Anna Makinda, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ilibidi afike Njombe mpaka Songea ili aende akatembelee Ifinga na kurudi tena Songea na kulala Njombe kabla ya kurudi Morogoro kwa kwenda kutembelea eneo dogo la Ifinga mpaka baadaye tukaamua kwamba Ifinga iende Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika Mkoa wa Iringa kuna eneo la kijiji kinaitwa Kigulu. Hiki kiko Wilaya ya Makete, inabidi uende Mbeya, halafu Tukuyu ili uende ukawasalimu na kurudi Tukuyu tena na kurudi Iringa wakati ni nchi ile ile na huwezi kuambatisha Tukuyu kwa sababu wanasema eti sisi ni wa Makete au ukienda Mbeya ukifika Igawa ni Mbeya, ukienda mbele kidogo Kifumbi ni Makete - Iringa, ukienda pale Chimala ni Mbeya. Sasa yule mtu wa Kifumbi hapa nyuma anatakiwa aende Makete, yule wa Chimala aende Mbarali. Nchi ile ile, watu ni wale wale, nadhani katika kurekebisha mambo haya Wilaya na mipaka tungeangalia baadhi ya mambo kama haya na kuyarekebisha kusudi watu wasipate taabu kwa sababu ya kwenda Wilayani Makete wakati Mbarali iko hapo hapo. Wengine wanakwenda Mbarali wengine, wanakwenda Makete wakati nchi ni ile ile. Nadhani ni wakati mzuri wa kurekebisha mambo kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa napendekeza kwamba kwa sababu ya mazingira yanavyokwenda hivi sasa wakati umefika wa kutazama matumizi ya ardhi katika nchi yetu, tusipoangalia nchi nzima itajaa vijumba vidogo vidogo tu. Mji wa Dar es Salaam utaungana na Mkoa wa Mororogo, utaungana na Mkoa wa Tanga na Mkoa Arusha and the whole of this country itajaa vijumba tu vimejaa kila mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanuka kwa miji katika nchi yetu kunaambatana na kuongezeka umaskini kwa sababu unawanyang'anya ardhi wakulima wadogo. Ni

vizuri tujue kuwa rasilimali kubwa tuliyonayo sisi Watanzania ni ardhi. Sasa pale Mbweni tumejenga vijumba vidogo vidogo na hapo juu Mwangaza tumejenga vijumba vidogo vidogo na kwa nchi yetu ndiyo inavyozidi kuendelea hatothamini ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kujenga nyumba za ghorofa tunaendelea kueneza tu vijumba vidogo vidogo na Mji unakuwa mpana sana kiasi kwamba gharama kama za maji, simu, umeme zinakuwa ni kubwa sana kwa sababu inabidi usambaze eneo lote hilo, kumbe ungekuwa eneo dogo gharama za kusambaza simu, mabomba, *wire* ingekuwa ndogo kwa sababu eneo ni dogo. Sasa miji yetu yote ya Tanzania ndiyo inavyozidi kwenda na gharama ni kubwa sana kuendesha miji yetu kwa sababu ya sera mbaya ya ujenzi wa nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu ni nini? Dar es Salaam unavyozidi kupanua Dar es Salaam ndiyo unazidi kuongeza umaskini kwa watu wetu kwa sababu wale Walugulu na Wazaramo walikuwa wanalima bustani pale wamenyang'anywa na wanasogea mahali pengine tena wanazidi kunyang'anywa na hiyo ndiyo sera ya nchi yetu nzima. Ukitembea nchi zilizoendelea siku hizi kuna dhana ya *gardening* ndani ya miji. Maeneo yenye ardhi nzuri yanaachwa kwa ajili ya bustani, ndani ya miji. Lakini kwetu sisi hapa ni kutenga eneo la viwanda wakati viwanda vyenyewe hatujengi, eneo la viwanda na kadhalika, lakini eneo la bustani kwenye *prime land* inachukuliwa unaona ni majumba tu au majengo tu. Wenzetu kwenye ardhi mbaya ndiko wanakojenga majengo, kwenye ardhi nzuri inakuwa ni kwa bustani. Kwa hiyo, watu wanakuwa na bustani na ajira, miji badala ya kufikiria kujenga viwanda ambavyo haviwezi kujengwa. Nilikuwa napendekeza katika matumizi ya ardhi kama *nilivyo-quote* hapa ingependa ni baadhi ya mambo ya kutolewa miongozo na kusimamiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *it is high time* Wizara inakuwa na Kamati ya wataalam ya kukagua maendeleo ya Vijiji na Miji, kama tunavyoangalia mahesabu kwa sababu kama tukibaki hivi hatuangalii maendeleo ya Miji wala Vijiji tutafikia wakati tutashindwa, wawe wanapita kwenye Mji X wanaangalia dosari zake na kusema unapendekeza mambo gani yafanywe kusudi nchi yetu iweze kwenda mbele vinginevyo kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Njelu Kasaka tutabaki na *Halleluya approach*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtaalam mmoja wa utawala alisema kwamba katika maskini kuna tatizo la kitu kinachoitwa, *hydro governments*. Mdudu *hydra* ana uhai uliotapaka mwili mzima, kwa hiyo, kila kipande kina uhai, kwa hiyo, Serikali ina uhai, kila mahali, kila mmoja ana madaraka, ana wakili na Waziri lakini ukienda kwa *Attorney* atakupeleka kwa *DC*, kwa *DC* hakuna *centralized authority* kwa hiyo, kuna matatizo ya namna hiyo ambayo yanatakana na umaskini wetu. Mambo ni magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sera ya miji kutokana na hali hii ingezingatia hili suala la kukua kwa minyonyoro ya miji, (*conurbations*). Mahali kama Makambako kama isinge kuwa miti ile ya Taniwati kati ya Mtwango na Njombe Mji wa Makambako

ungeungana na Njombe na huenda Mji wa Makambako ungeungana na Chimala na kwa upande wa juu labda ungeungana na Kilombero.

Sasa hizi *conurbations* bila kuwa na *plans* za kutazama mbali na kwa sababu nchi nyingi sasa wanazo *laboratories* nchi ambazo zimeendelea zina vitu vya namna hiyo, kwa nini tusijifunze kutoka kule na kuanza kuwa na sera? Nilikuwa napendekeza kwamba tuwe na *commissioners* wawili, *Commissioner* wa Mji atakayekuwa anaangalia hii Mji Midogo, Mji Vijiji, Manispaa na wa Vijiji. Hivi Vijiji ndiyo viwanda mama. Tusipoangalia umaskini huu nao utazidi kukua kwa sababu ardhi yote itakuwa imejaa majengo na hakuna mtazamo wa kutazama mbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi nashukuru kwamba Wizara imeamua kuweka Mji Midogo iwe Mji. Tuliomba Makambako na Njombe iwe Mji, Njombe, nimeongea na wahusika nadhani kuna uwezekano wa kuwa Mji, lakini Makambako kuna mashaka kidogo kwa sababu tu ya utaratibu tu wa urasimu. Makambako *is the fastest growing town* katika *Southern Highland*. Ni Mji unaokua kwa kasi kubwa kuliko Mji wowote ule katika Nyanda za Juu Kusini. Hivi sasa una watu zaidi ya 52,000, ndiyo lango la kuingilia Kusini na Kusini Nyanda za Juu, ndiyo sebule ya Mkoa wa Iringa. Pale ndiyo inapita reli ya *TAZARA*, *TANZAM ROAD*, *TAZAMA* na yote hayo. Hivi sasa kuna watu zaidi ya 52,000 lakini ni kijiji. Juzi tu ndiyo wamebatiza Mji Mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uwe na sifa za kuwa Mji usiwe na *population* chini ya watu 30,000. Sasa wale wako 52,000. Sasa tunasubiri mpaka uje uharibike ndipo tuje tubatize kuwa Mji. Nilikuwa napendekeza Wizara ingeangalia mambo kama hayo kusudi tujiepushe na matatizo ambayo yanaweza yakatupa shida siku za baadaye. (*Makofi*)

Mwisho nimalizie kwa kusema kwamba sera ya kujenga nyumba katika nchi yetu sijui ni ipi, ni Serikali Kuu kujenga nyumba kama za Mbweni na Mwangaza na kuwauzia wafanyakazi na kwenda mahali pengine kujenga na kuwauzia wafanyakazi kama Shirika la *National Housing* au vipi?

Pamoja na nia nzuri hii *quality* ya nyumba, mpangilio wa nyumba katika Mji yetu, lazima tuangalie. Uzunguni Dodoma ilijengwa miaka mingapi iliyopita, bado mambo ni mazuri lakini pale Mwangaza nyumba zimeshikama kama za manamba katika karne ya 21. Kwa kweli si vizuri. Ni lazima tujenge *an architectural garden town*, siyo *concrete jungle*. Eti mradi nyumba au bora nyumba. Hapana tuangalie vizuri. *Prime land* kama ile kwa kweli tungejenga majengo mazuri siyo *barracks* yaani majumba ambayo yameshikamana. Hii ni nchi yetu, tuisubiri watu wafe ndipo tuenze kuwasema. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niitumie nafasi hii kwa kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha aliyejikuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero, ndugu yetu Marehemu Abu Kiwanga. Salaam hizi ziwafikie wananchi wote wa Jimbo la Kilombero pamoja na familia ya Marehemu. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Niitumie basi nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote cha miaka 10. Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kila mwaka alikuwa anaibuka na nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka siku moja niliwahi kuchangia hapa nikasema ningekuwa na uwezo ningeweza kushawishi Bunge hili kurekebisha Katiba ili Mheshimiwa Benjamin Mkapa aweze kuongezewa siku za kuongoza nchi hii. Nakumbuka nilipingana sana na Mheshimiwa Njelu Kasaka mpaka magazeti yalituandika mara kadhaa waki-*challenge* hoja zetu. Lakini nilikuwa na nia njema tu kwa sababu kazi zake kwa kweli zilijionyesha wazi na zimetuletea mfano mzuri katika nchi za Kimataifa mpaka zimefika mahali zimetutufia madeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wa kimbunga alioupara katika uchaguzi wa tarehe 4 Mei, 2005 katika Ukumbi wa Chimwaga hali ambayo imewapa matumaini Watanzania wakitegemea kabisa kwamba yote aliyoafanya Mheshimiwa Benjamin Mkapa sasa yamepata mwanaume wa kuyaendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wananchi kwa ujumla tumuunge mkono Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ili utakapofika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aibuke na ushindi wa kimbunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa ushindi walioupara katika uchaguzi huo huo wa Chimwaga. Ni matumaini yangu kwamba ifikapo Oktoba baada ya Uchaguzi Mkuu tutakuwa tumpata viongozi hodari watakaoendeleza kuinua uchumi wa nchi kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndugu yangu Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda, bila kumsahau Katibu Mkuu ndugu yangu Mmari kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa Bajeti hii yenye mtazamo mzuri kabisa wa kimaendeleo. Ni matumaini yangu Bajeti hii itapata wasimamizi wazuri na yote yaliyoandaliwa yatatekelezwa ipasavyo. Mungu awabariki sana.

Vile vile nitakuwa mchoyo kama sitawashukuru kipekee watu wote hawa watatu. Nimejaribu kuingia ofisini kwao mara kadhaa, nimeanza kwa Mheshimiwa Waziri, nimekwenda kwake na kila nilipofika ofisini kwake alinipokea vizuri na hoja zote

ambazo nilikuwa nazo alinisaidia. Vile vile Mheshimiwa Mizengo Pinda, hali kadhalika amekuwa ni Naibu Waziri hodari wa kujibu wa maswali na hodari wa kusikiliza Waheshimiwa Wabunge, katika masuala ya maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie basi fursa hii vile vile kuipongeza Serikali kwa kuipa hadhi Halmashauri ya Mji wa Singida, kuwa Manispaa kuanzia tarehe 1 Julai, 2005 nina hakika Serikali haijatoa kama sadaka Halmashauri ya Mji wa Singida kuwa Manispaa, wamechunguza kwa kina kabisa na kuona vigezo vinavyostahili vimetekelezwa katika Mji wa Singida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Singida, itakuwa Manispaa naomba sasa Halmashauri hiyo ifanane na hadhi ya Manispaa. Mji wa Singida una barabara za lami, zenyen urefu wa nusu kilometa kama tatu tu. Mji mzima hauna barabara za lami. Nina matumaini Mheshimiwa Waziri utakuwa pamoja na mimi kuona umuhimu kuweka nguvu kwenye Bajeti ya Mkoa wa Singida ili Mji huo uweze kufanana na hadhi tutakayoanza nayo Julai Mosi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nitumie Bunge au jukwaa hili kuwaomba Watanzania waje kuwekeza Singida, ardhi ni tele Mkoa wa Singida, vivutio Singida viko vya kutosha kabisa, tuna maziwa ya kutosha yanayovutia watazamaji, tuna mawe yaliyobebana yenye mithili ya sanamu na mambo mengi. Hivyo basi njooni muwekeze Singida ili muweze kutuunga mkono katika kupanua Mji wa Singida, wenye kutaka kujenga hoteli, wenye kuweka miradi mbalimbali, karibuni sana kustawisha Mji wa Singida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuitia Bajeti hii naiomba Serikali ili hadhi ya Mji wa Singida iendelee kukua siku hadi siku nina mashaka na mkandarasi wa barabara ya Manyoni - Singida. Kuitia Bajeti hii naomba Serikali iende itazame upya mkandarasi huyu kwani utengenezaji wake ni wa kusuasua. Tunapenda wakandarasi wenye kasi na *speed* kwenda sambamba na jinsi walivyoweka mkataba. Napata wasiwasi mpaka mwaka 2006 mkandarasi huyu atakuwa hajamaliza.

Mimi nilikuwa nashawishi Serikali kumwondo huyu mkandarasi na kuweka mkandarasi mwininge atakayetengeneza barabara kwa kasi inayostahili ili hadhi ya Mji wa Singida iendelee na wawekezaji watakaopenda kuja Singida waweze kufika Singida kwa sababu barabara ni kigezo kikubwa kabisa watu kupenda kwenda mahali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie hadhara hii kuupongeza uongozi mzima wa Halmashauri ya Mji wa Singida, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweka Mji wa Singida safi. Usafi huo umepelekea Halmashauri ya Mji wa Singida kuwa mshindi wa pili kwa usafi wa mazingira kwa miji yote ya Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huu umeiletea sifa Mji wa Singida na Mkoa mzima. Naomba basi ari ya watendaji wa Halmashauri ya Singida isiihie hapo, iendelee siku hadi siku na itakapokuwa Manispaa ushindi huu tuweze kuuchukua pia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia fursa hii kipongeza Serikali kuendelea kupeleka hela kwenye mfuko wa vijana na akinamama na vile vile niipongeze Halmashauri zote nchini hasa za Mkoa wa Singida jinsi ambavyo zinajitahidi kutenga fedha hizi kwa ajili ya mfuko wa akinamama na vijana. Vile vile nawapongeza akinamama wote wa Mkoa wa Singida, natumaini hata nchi nzima na jinsi wanavyojitahidi katika kusimamia miradi ya uzalishaji mali kwa lengo la kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi akinamama hawa na vijana wanafika mahali wanakuwa kikwazo kwenye Halmashauri zetu kwa sababu wanashindwa kurudisha mikopo wanayopewa. Naamini kushindwa kwao hawajashindwa kwa makusudi, wanashindwa kwa sababu hawajapata elimu ya uzalishaji mali. Naiomba Serikali iwawezeshe maafisa maendeleo ya jamii usafiri ili waweze kutoka maofisini, naamini wanakaa maofisini kwa sababu hawana usafiri. Wapewe usafiri ili wawafuate akinamama mahali walipo, wawafuata vijana walipo watoe elimu ya kuweka fedha na namna ya kurejesha mikopo yao. Bila kupewa elimu ni hakika akinamama hawa wataendelea kuwa vikwazo katika Halmashauri zetu na Wakurugenzi hawa wataendelea kupata matatizo ya kugombana na Kamati za Bunge kwa kushindwa kurejesha mikopo ya akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuiomba Serikali kuwa Halmashauri zetu zimeshuka mapato baada ya kodi za maendeleo na kodi zingine kufutwa. Lakini kufutwa kwa kodi hizo siyo kigezo cha mapato ya Halmashauri zetu kushuka. Ni kwamba ubunifu wa vyanzo vya mapato ni mdogo.

Naomba elimu itolewe kwa Maafisa Mipango na Maafisa Uchumi ili waweze kujua namna ya kubuni vyanzo vya mapato. Wakipta uwezo wa kubuni vyanzo vya mapato nina hakika kila Halmashauri ina namna nyingi za kukusanya mapato. Lakini wenzetu hawa naamini taaluma zao zimeanza kupitwa na wakati ndiyo maana wanafika mahali wanashindwa kubuni vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nitumie nafasi hii kupongeza Halmashauri ambazo zimepata hati safi katika ukaguzi wa mwaka huu. Halmashauri hizi zimethibitisha wazi kwamba zimesimamia Halmashauri zao katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa sababu Kamati ya *LAAC* tumefanya ziara kutembelea Halmashauri hizo, tumeangalia sisi wenyewe na kuona *value for money*, tumehakikisha kwamba miradi iliyotekeliza inafanana na kiasi cha fedha kilichotengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii nizipongeze Halmashauri za Mkoa wa Singida pamoja na kwamba hazijapata hati safi lakini zimepata hati ya masharti hati ambayo angalau inatusaidia kupewa fedha za maendeleo kwa sababu fedha za maendeleo ambao hawapati kabisa ni wale walipata hati chafu. Waswahili wanasema haba na haba hujaza kibaba. Nina hakika mwanzo huo ni mzuri mpaka mwaka kesho Singida itapata hati safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vile vile nizipongeze Manispaa za Dar es Salaam. Manispaa za Dar es Salaam zimekuwa mfano katika Manispaa zote Tanzania. Kazi zao zimeonekana wazi, ni nzuri labda nitumie tu nafasi hii kukumbusha Jiji la Dar es Salaam. Tulipofanya ziara yetu walitudokezea kwamba wana mkakati wa kujenga barabara za angani, wanataka kuondokana na adha ya bomoa bomoa. Sasa mradi huo wa kujenga barabara za angani utaanza lini? Ni vizuri basi tukaanza kuona dalili yake, kwani barabara hizi za kupanua kila wakati ugomvi na wananchi waliojenga karibu na barabara hautaisha kwa sababu magari Dar es Salaam, yanaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bila kutafuta mbinu za kujenga barabara zingine hali ya barabara za Dar es Salaam itakuwa ni taabu kwa sababu mwendo wa Dar es Salaam hata umbali wa kilometra moja unaweza ukachukua nusu saa. Alituambia Mkurugenzi wa Jiji kuwa barabara za anga zitajengwa ninamwomba alitekeleze wazo zuri sana, halina matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuipongeza Serikali jinsi inavyowakumbuka na kuwajali akinamama kuwapa madaraka katika nafasi mbalimbali Serikalini. Nina hakika kabisa akinamama hawa wameonyesha ni jinsi gani wanaweza na wameweza kwa sababu Serikali imewajali na inawalea.

Sasa basi ni matumaini yangu kuwa Serikali ijayo, itatekeleza hoja hii vizuri zaidi ikiwa ni mwendelezo wa wazo la Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa la kuongeza akinamama madarakani na sana basi kama huku chini tumeshakuwa wengi tusogezeni na juu tupate ma-*DC* wengine, tupate ma-*RAS* wengine, tupate Wakuu wa Mikoa wengine, akinamama wapo na wana uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika mtakapoona umuhimu wa kuwakumbuka akinamama madarakani mtakuwa mmesaidia nchi hii, akinamama kwenda sambamba na akinababa katika suala zima la kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Ningependa kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa leo, pamoja na vitabu viliivoandaliwa vizuri ambavyo tumegawiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo Pinda, ndugu yangu, kaka yangu kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya na wananchi wa Kongwa wanakushukuru sana kwa kuwa ulipata muda kuwatemeblea bado wanakuomba utembelee tena kufungua ile nyumba ya mwalimu pamoja na kuona maendeleo ya hospitali yetu ya Wilaya ya ujenzi unaoendelea. Nawapongeza sana kwa kulimaliza suala

la malipo ya malimbikizo ya mishahara ya Watendaji wetu wa Vijiji lilikuwa ni tatizo moja kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kufufua uchumi, kurejesha imani ya wahisani wetu na kutufikisha mahali ambapo madeni yetu mengi sana yamesamehewa na wahisani wetu wengi. Pia nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na CCM kushika bendera katika uchaguzi unaokuja, Mheshimiwa Amani Abeid Karume pamoja Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. (*Makofi*)

Nilipokuwa nafanya ziara vijijini majuzi kule Kongwa walichoniambia ni kwamba hivi kwa nini uchaguzi uko mwezi wa kumi kwa nini usiwe kesho kutwa tu hapa, wao walete tu maboksi sisi tupige kura. Kwa sababu hamna haja ya kampeni, ushindi wa safari hii kwa kweli kinachosubiriwa ni *figures* tu kujua iko asilimia ngapi. Lakini kazi imeisha kwa kweli kimsingi. Ningependa ndugu zetu wafahamu shughuli imeshaisha kabla haijaanza. (*Makofi*)

Natoa rambirambi kwa kifo kilichotokea cha Mheshimiwa marehemu Abu Towegale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu ya kusimama hapa ni kushuhudia tu yale ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema asubuhi hii kwa kule ninakotoka mimi, maana alichokisoma hapa ni kile ambacho kimetekelizwa kule tunakotoka sisi wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumefanyika kazi nzuri sana katika kipindi cha uhai wa Bunge hili wa miaka hii minne na nusu mpaka sasa kazi iliyofanywa ni nzuri sana. Kupitia Wizara hii sisi tulikuwa na shule 65 mwaka 2000. Lakini leo tuna shule 97. Ni ongezeko kubwa katika muda mfupi sana. Shule hizi zinafanana fanana na shule za Wilaya ya Temeke au Halmashauri ya Temeke, *almost* sawa, Wilaya ya Temeke wana shule 100. Ni ongezeko kubwa la haraka sana. Tulikuwa na shule tatu za Sekondari, mwaka jana peke yake tumeongeza shule tatu na sasa hivi ziko shule 10 ambazo ziko katika *stage* tofauti tofauti zitaanzishwa kati ya mwaka 2006 na 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yasingewezekana bila kupitia juhudhi kubwa na mipango mizuri sana ambayo tumekuwa tukifanikiwa nayo kupitia TAMISEMI na kama walivyosema wenzangu pesa zimepelekwa kule kule kwenye Kamati za Shule, wanajenge wenyewe, wamewezeshwa wenyewe, utaratibu huu ningombaa uendelee, ni utaratibu nzuri wa kuwezesha wananchi kuweza kufanya mambo yanayohusu wao wenyewe kwa kuwashirikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za vitabu, fedha za nyumba za walimu, fedha za madarasa na Kamati za shule zimetolewa, zote hizi. Kwenye Afya sisi tulikuwa na Zahanati 14 mwaka 2000. Kwa miaka hii minne na nusu tumeweza kujenga Zahanati 21 mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatua kubwa sana. Lakini tusingeweza kufanya yote haya bila usaidizi mkubwa kama nilivyosema wa Wizara hii. Kwa hiyo, ninachokisema Mheshimiwa Waziri kwa kweli kwa kiwango kikubwa ni kweli kabisa kwamba hatua kubwa imefanyika. Hospitali ya Wilaya, Hospitali ya Wilaya ilikuwa ni kituo cha Afya kabla sisi ni moja ya Wilaya changa, lakini sasa hivi tumepatiwa majengo, *Surgical Ward*, *Maternity Ward*, Wadi ya Watoto, *OPD* inajengwa pale, *Pharmacy* imekwishajengwa tayari. Ukifika unapenda unaona kabisa kwamba mambo haya yanaenda hivi sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kipengele kimoja tu cha kuanzishwa Bodi ya Afya ya Wilaya ambayo najua kuwa TAMISEMI mlismaliza kazi hiyo ila bado iko kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maana ya kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili Bodi hiyo iweze kuanza.

Naomba muendelee kusaidia ili tuweze kupata Bodi hiyo ili tuweze kwenda mbele zaidi katika kuendesha Zahanati hizi nyingi sana zinazohitaji chombo kitakachowezesha kusaidia Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali wenyewe ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Utawala mmetusaidia sana, kama tulivyosema sisi ni Halmashauri mpya tayari tunalo jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa la zaidi ya milioni 100. Tumeweza kupata Mahakama mpya ya Wilaya, hatuna haja ya kwenda Mpwapwa tena kwa Mheshimiwa George Lubeleje na Mahakama yetu itakuwa ni kituo kidogo cha Mahakama Kuu kwa baadhi ya kesi za Mahakama Kuu, Majaji watakuja pale siku 10 hadi siku 20 wakamaliza mambo yote ya *size* ya Mahakama Kuu pale pale Kongwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimesimama hapa kusema aliyo sema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake na hatua ambayo tumeipiga ni kubwa. Tunaposema kwamba tunampongeza Mheshimiwa Waziri, tunaposema tunampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, tuna nia hiyo kabisa, toka ndani ya miyo yetu kwamba Awamu hii imefanya kazi nzuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwapongeza Mawaziri wote kabisa kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanyika. Sisi shida yetu namba moja, tumewahi kufanya zoezi linaitwa *PRA*, kutazama shida za wananchi, ipi inatangulia nyingine. Shida ya kwanza ilikuwa kutoka kwa wananchi wenyewe ni maji. Kama mnavyojuwa sisi tuko kwenye ukanda amba ni mkame kidogo. Kwenye eneo la maji peke yake tunao huu mradi wa Benki wa Dunia amba ni awamu mbili, awamu ya kwanza na ya pili.

Kwa awamu ya kwanza peke yake fedha zitaanza kufanya kazi mwezi ujao wa saba kuchimba visima kwenye vijiji 10 na mji mdogo wa Kongwa wenyewe ni shilingi bilioni 2 na milioni mia tatu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema, kule Kongwa wamesema jamani leteni maboksi, sisi tupige kura basi. Hakuna hoja ya msingi. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie eneo moja dogo tu la Kibaigwa. Amesema Mheshimiwa Jackson Makwetta ana vijiji vyake 20 vinafanana na Kibaigwa. Nitofautiane kidogo tu mjomba wangu kwamba vile bado vidogo vidogo. Kibaigwa ni mahali pa kipekee kidogo. Nitaeleza kwa nini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kibaigwa katika kipindi hiki hiki cha miaka minne na nusu pamejengwa soko la kisasa na la kipekee na la aina yake linaloitwa Soko la Kimataifa la Mahindi. Hiyo *aspect* ndiyo inayofanya tofauti sana na yale maeneo mengine aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Jackson Makwetta na tunatarajia kwamba kuna masoko mengine kufuatia Kibaigwa, moja tunatarajia tumeambiwa na Wizara ya Ushirika na Masoko litajengwa Segera na lingine Makambako. Sasa likishajengwa Makambako ndiyo mtafanana na Kibaigwa sasa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali, maana ni awamu hii, milioni kadhaa kwa ajili ya kujenga soko lile, tunashukuru sana. Tatizo letu ni moja dogo tu la usalama wa eneo la Kibaigwa. Wizara ya Mambo ya Ndani wanafahamu jambo hili. Nimewahi kulizungumza katika miaka miwili mfululizo na walitoa ahadi ya kulishughulikia suala hili kabla ya sasa na nimekuwa nikiwasiliana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kukumbusha kwamba mwaka 1998 wananchi wa Kibaigwa waliji-*organise* wenyewe wakajenga Kituo cha Polisi. Lakini wataalam wa Mambo ya Ndani wakasema Kituo hiki ni kidogo kilijengwa kama hivi vituo vya mijini vya *Police Post*. Wakasema hiki ni kidogo sana. Kwa hiyo, jitahidini mjenje kingine kikubwa chenye hadhi. Wananchi wale wakajiandaa na mimi nikawahamasisha na uongozi ukawahamasisha, wakajenga kituo kingine kikubwa kizuri, wao wenyewe tangu mwaka 2004 mwanzoni kiko pale, kimeisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo ya Ndani wakasema hatuwezi kufungua kituo cha Polisi bila choo. Kwa hiyo, waambieni wananchi wachimbe choo. Tukakimbia kimbia choo kiko tayari. Wakasema bila nyumba za Polisi hatuwezi kufungua. Sasa hapo ndiyo penye tatizo. Toka mwaka 1998 wananchi hawa wanafanya hatua moja au nyingine, lakini polisi hawahamii pale ndiyo kilio cha wananchi, wanasema Mbunge sisi mbona hatuna tatizo. Nyumba sisi tutajenga. Lakini waambie nao walete Polisi hata kama watatu, wanne tu. Kituo kifunguliwe angalau paanje kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu eneo lile ni la biashara kubwa. Tumesema kuna Soko la Kimataifa. Itakuwa ni soko pekee la Kimataifa la eneo la Kibaigwa ambalo usalama wake ni wa wasiwasi. Ni lazima polisi, hivi sasa ninavyoongea Polisi wanatoka Kongwa, wanaenda Kibaigwa kulinda usiku huu, watatu, wanne. Hawana usafiri. Tuliomba gari la polisi, bado hatujapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanadandia dandia magari, wakifika kule ni watu wako ugenini tu kesho asubuhi warudi tena. Kesho jioni wapelekwe wengine. Ni tatizo kubwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Kibaigwa. Kibaigwa kuna sifa zote za kuwa na kituo cha Polisi, wananchi wanaomba sana Serikali yao iwasikie katika hili, Kongwa ni wasikivu, wananchi wa Kibaigwa ni wasikivu. Wanapoambiwa kuchangia

jambo wanachangia. Mimi naamini kabisa suala la kujenga nyumba ya Polisi si tatizo. Lakini tushirikiane na Wizara tuone jinsi ambavyo tunaweza tukatatua jambo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama unavyojuua Kibaigwa inafanana tu na Mererani, inafanana na maeneo yenyeye miji inayokuwa haraka sana. Maeneo yale yana watu mchanganyiko, ni vichaka kwa namna moja au nyingine vyâ baadhi ya watu ambao si wema sana katika jamii na Kibaigwa pale pana sifa hizo. Kwa hiyo, panastahili kabisa kuwa na ulinzi wa kutosha wa jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niliseme hili kabla ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa vile ye ye ni Katibu Mwenezi wangu Taifa, sitapenda kusimama kwenye Bajeti yake na kwa kweli jambo hili tunaenda nalo vizuri na kaka yangu Naibu Waziri, ningewaombeni sana kwa niaba ya watu wa Kibaigwa na watu wa Kongwa tufanye kila linalowezekana kwa kushirikiana sote pamoja ili Kituo cha Polisi Kibaigwa kiweze kuanza ikiwezekana mwezi huu wa Julai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Alhaj Mussa Nkhangaa, Mkuu wangu wa Wilaya, viongozi wote kabisa wa Chama na Serikali Kongwa kwa ushirikiano mkubwa sana ambao umewevesha Jimbo letu kuingia katika ramani ya maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika muda wa wiki chache zizazo utanisikia nachukua fomu kurudi tena kujaribu kwa mara nyingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu. Naomba nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha hotuba yake vizuri leo asubuhi na vile vile nipongeze uzito wa hoja yenewe kwamba amewasilisha kazi nzuri, taarifa ya kazi nzuri inayofanywa na Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano. (*Makofî*)

Lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Mkoo wa Nchi ambaye ndiyo Mkoo wa Ofisi ile, Rais Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake wa kipindi cha miaka kumi na hasa akiisimamia vizuri Ofisi yake hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. (*Makofî*)

Naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa jinsi anavyomsaidia kazi vizuri. Yeye karibu kila siku iendayo kwa Mungu tunapokuwa katika Bunge huwa anajibu maswali yasiyopungua mawili na anajibu vizuri. Kwa msingi huo kazi imefanyika vizuri na ya uhakika. Napenda vile vile nimpongeze Katibu Mkoo, Ndugu Mmari, naye amekuwa ni msaidizi wao mzuri katika suala zima la utendaji. (*Makofî*)

Wizara hii mojawapo ya majukumu yake makuu iliundwa ili kupeleka madaraka kwa wananchi karibu ili kuweza kuwawezesha wananchi kushirikiana pamoja kuweza kutambua matatizo yao, kutafuta mbinu ya kuyatatua na pale ambako basi wanaona ugumu ndipo inapoingia Serikali na wahisani wengine na wote wenye nia njema kuweza kushirikiana nao kusaidiana kuweza kutatua na kuondokana na kero mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ya leo katika hotuba iliyowasilishwa ndani ya jumba hili Tukufu, ilitokea Taarifa kwamba Serikali imeunda na imeweza kuanzisha Kata mpya 17, pamoja na kuanzisha Vijiji vingine vipyta zaidi ya 9,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napongeza hatua hiyo sana. Kwa sababu inalenga kutaka kupeleka madaraka karibu na wananchi, isipokuwa tu kwa masikitiko napenda kuuliza, sikuweza kuelewa ni kwa nini basi maombi yaliyotokea Wilaya ya Muleba, katika jimbo la Muleba Kaskazini, yaliyopitia ndani ya Kikao chake kilichokuwa halali kabisa hayakuweza kupata sifa ya kuweza kugawika kwa Kata ambazo walau tuliona tungeweza tukapata Kata nyingine mpya tano, ikiwemo Kata ya Izigo ni kubwa sana inachukua zaidi ya robo ya Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Kata ya Ngenge, ni kubwa sana umbali wa kutoka Makao Makuu ya Kata kwenda mpaka kijiji cha mwisho ni zaidi ya kilometra 30. Imo Kata ya Rushwa ya Kihaya. Hicho ni Kihaya siyo Kiswahili. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hiyo pia na yenye ni kubwa. Eneo lake kwa kweli tulikuwa tunatarajia kwamba ingeweza ikagawanyika. Kata ya Goziba, ni kubwa sana. Kata iliyo ndani ya Ziwa Victoria, umbali wa kutoka Makao Makuu ya Tarafa kufika mpaka Makao Makuu ya Kata mpaka kufika kijiji cha mwisho ni siku nzima, tena unasafiri ndani ya maji.

Vile vile Kata ya Kagoma ni kubwa inachukua eneo kubwa na ina vijiji vingi na watu ni wengi. Kwa hiyo, mimi nilisikia kwa namna fulani kwamba hivi kulikuwa na sababu gani. Nikajaribu kuangalia vigezo vilivyotolewa ndani ya kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri. Sikuamini kama kuna kigezo ambacho hatukufanya kwa sababu kama sensa ilifanyika. Muhtasari wa Vijiji husika kuonyesha kwamba wanaomba kugawanywa ulifanyika, muhtasari ya *Ward DC* ilikwenda. Muhtasari ya Baraza la Madiwani ilikuwepo. Fomu zilijazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivyo vina Kaya zinazozidi 250. Kwa hiyo, sifa za kupata vijiji vipyta na kupata Kata mpya kwa kweli tulikuwa nazo na vile vile maelezo ya mipaka inayofahamika tulikuwa nayo. Basi Mheshimiwa Waziri akazielekeza Halmashauri zinazohusika kwamba zinapohitaji kugawa vijiji ziambatanishe na kumbukumbu hizi. Mimi naamini kwamba kumbukumbu zetu zinaweza kuwa zilishamfikia Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, naomba basi asiendelee kukawia kutupatia Kata hizo ambazo tumeambiwa zitagawanywa baada ya uchaguzi. Sasa sijui kama baada ya uchaguzi huu

tutafanya uchaguzi mwingine tena ama itakuwa vipi. Kwa sasa juhudini yetu yote ilikuwa ni kutaka kuona Kata na Vijiji vinatengwa kabla ya uchaguzi uliopita na huu unaokuja ili kuweza kabisa kufanya uchaguzi wa viongozi wa Vijiji na Vitongoji katika mipaka mipyä pamoja na Madiwani kwa upande wa Kata.

Lingine ambalo napenda niliseme mimi vile vile ni la kutoa shukrani. Nimesoma katika kitabu hiki juhudini kubwa sana ambazo zinafanya na Wizara hii katika kuboresha suala zima la usafiri na uchukuzi vijijini na hasa wakizingatia ujenzi wa madaraja ili kuwezesha barabara kupidika muda wote na mimi natoa shukrani za kipekee kwamba katika jitihada hizi Wizara ya TAMISEMI imeweza kukubali kutujengea daraja katika Jimbo la Muleba Kaskazini ambalo lilikuwa limeshindikana miaka yote tangu kuumbwa kwa dunia na kuwepo kwa Wabunge wenzangu wote waliotangulia ndani ya Chama cha Mapinduzi na hata ndani ya upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakakubali kutoa pesa nyingi tu zinazokaribia milioini 60 au kuzidi ili kuweza kutengeneza daraja hilo. Daraja hilo ni maarufu kwa jina Kishara. Lakini kinachonisikitisha sana ambacho sijakielewa sawa sawa ni ile kasi ya ujenzi wa daraja ambayo ilitakiwa kukabidhiwa tarehe 30 Juni, 2005. Lakini hatua ambayo nilipoondoka Jimboni niliiacha haitoi matumaini hata kama yule mwenye kuweza kujenga daraja hilo atakuwa anajenga *by speed* ya *super sonic* bado hawezu kumaliza daraja hilo ndani ya muda mchache ambao nilikuwa nimeondoka.

Sasa mimi nasikitika sana kuona kwamba tulikuwa na ugumu wa kupata pesa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Lakini baada ya kupata pesa, daraja linaweza likakaa tena kipindi kingine kirefu bila ya kujengwa. Kwa kweli yule mkandarasi afe yeze au nife mimi, asipojenga lile daraja lazima arudishe hizo pesa zetu. (*Kicheko*)

Kwa sababu amekwisha kulipwa zaidi ya nusu ya pesa. Lakini daraja halioneckani. Anataka kutuambia kitu gani. Ndiyo afe yeze, nakubali kwamba afe yeze. Sasa kabla ya kufa, mimi kwa sababu simtakii kifo cha mauti, basi ahakikisha kwamba tunapokuwa kumaliza Bunge hili tarehe 29 Julai, 2005 awe amekwisha kuonyesha *structure* inayolingana na pesa aliyochukua ili kuhakikisha kwamba pesa aliyochukua, amechukua kihalali na kazi aliyoifanya, ameifanya kihalali.

Vile vile nashauri Halmashauri yangu ya Wilaya ya Muleba kumsimamia kwa karibu kwa sababu siafiki kama mjenzi anaweza akaachwa yeze peke yake asijenge daraja na pesa akachukua kazi inayoonekana uki-access hata wao wenyewe wa Ujenzi walipofika pale hawakuridhika nayo. Kisha mtu huyo anaendelea kuomba pesa na anapewa pesa na anaendelea kuchukua pesa wakati kazi haifanyiki. Kwa hiyo, ni lazima wawe naye karibu kuhakikisha kwamba daraja hili linajengwa na linakamilika ili kuhakikisha kwamba ahadi ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi uliopita inakamilishwa ndani ya kipindi cha miaka mitano kama tulivyokuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloliletu na lenyewe ni ombi. Naipongeza Serikali kwamba imeendelea kutambua umuhimu wa kuwepo vikundi vya akinamama na vijana kupata mikopo inayotokana na mapato ya Halmashauri ya Wilaya. Lakini kama ambavyo mara nyingi nimekuwa nikisema hili kwamba tunaposema kwamba vile vikundi

vya akinamama na vijana vigate mikopo kutokana na mapato ya Halmashauri ya Wilaya, ni vizuri pia tukazingatia uwezo wa mapato wa hizi Halmashauri, tukazingatia idadi ya wanawake na vijana katika zile Halmashauri. Tukazingatia pia mazingira ya zile Halmashauri kwa sababu huwezi ukalinganisha Wilaya ya Muleba labda na mji tuseme wa Mwanza au Dar es Salaam ambapo kipato chao ni kikubwa.

Kwa hiyo, kile kipato kinawezesha pia na akinamama wa maeneo yale kupata asilimia kubwa na kuweza kujikomboa katika lindi zima la umaskini. Lakini wanawake katika maeneo ambako kipato ni kidogo na vijana kwa kweli wanaofikiriwa na wanaoweza kufikia kupata kiasi cha mikopo ni wachache mno. Nilikuwa najaribu kuangalia hapa haifiki milioni 40 ambayo walipewa vijana na akinamama wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kipindi cha miaka mitano.

Kwa hiyo, ni kiasi kidogo mno ambacho kwa kweli kama hakijaweza kufanyika hatua nyingine ya ziada ya kuwasaidia haitawezekana kabisa kuwakomboa akinamama hawa, kuwakomboa vijana hawa na tatizo la umaskini. Lakini vile vile kama ambavyo hotuba imesema kwamba tuelekee katika kutoa elimu zaidi. Ni vizuri mikopo inapoandaliwa ili kuweza kutolewa kwa kusaidia walengwa elimu itangulie kwanza kusudi huyu anayekwenda kupokea pesa ajue anazipokea kuzifanyia nini na yeze awe ndiye mwenye kuibua hoja kwamba anapenda zile pesa azifanyie kitu gani.

Lakini kwa mazingira kwa mfano ya kwetu kule ambako masoko ya kuuzia biashara si makubwa sana, basi mwelekeo wa kwetu uelekee katika kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa mfano sisi tunayo matunda mengi. Tuna nanasi nyingi, ndizi za kisukari nyingi na matunda mengine mengi tu ambayo tunaweza tukawa na viwanda vya kutusaidia sisi kuweza kusindika yale matunda na ikawa ni sehemu ya kusaidia vikundi hivyo vya akinamama na vijana kulima na kupata mahali pa kupeleka mazao yao.

Ama kuwa na hisa ndani ya hivyo viwanda vidogo vidogo nao wakawenza kupata kipato kikubwa zaidi badala ya kutegemea kwamba wao wapokee pesa na wakati mwengine hawajui watazifanyia nini. Lakini vile vile suala zima la ufugaji katika maeneo ya vijiji linapata nafasi kwa sababu kwanza malisho bado yapo ya kutosha na vile vile lishe inatakiwa sana kwa sababu ya idadi ya watu iliyoko kule si ndogo ya kushindikana kutosheleza soko hili.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali hili iliangularie na kwa kweli iangularie hata wakati ule inapotolewa mikopo kwa wanawake na vijana kuna usumbufu mwingu mno ambao unatisha na unakatisha tamaa. Kuna kikundi kimoja cha Jitihada ambacho nakumbuka kilipata mkopo huu baada ya kuwa kimesota mwaka mzima. Sasa mwaka mzima ukitoka mahali walipokuwa wanakwenda watu wanne ambao ndio kikundi kilichotakiwa kuwa kinafutilia, kila siku ni nauli ya kwenda na kurudi isiyopungua shilingi 3,000. Hivi kwa kipindi cha mwaka mzima walitumia shilingi ngapi. Mkopo waliopewa ni shilingi laki tano, walishakula shilingi ngapi katika mwaka mmoja na baadaye unapowapa mkopo unakuwa umewaachia shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya ni mambo ya kuangaliwa kabisa kama kikundi kimekwishapata sifa kisaidiwe haraka na kipewe pesa hizo haraka ili kiweze

kuwa kimezitumia katika muda muafaka wakamaliza lile tatizo lao lakini vile vile wakabaki na faida kuweza kuendeleza maisha yao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalopenda kulisemea wamelizungumza wenzangu. Tunayo kazi kubwa sana inayohusu matatizo ya Madiwani. Madiwani hawana imani kama sisi tunapokuwa Bungeni tunawasemea. Bungeni tunawasemea sana na hakika tunaona maisha waliyokuwa nayo tukiwatambua kama wasaidizi wetu wa karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, posho wanayoipata na yenyewe inatokana na uwezo wa Halmashauri, ni kiasi ambacho ni kidogo mno. Nashauri kwa sababu tumefikia mahali sasa mapato yetu ya Serikali yamepanda basi iwepo walau *token figure* ya namna fulani ya kuwapatia hawa Madiwani na wenyewe waongezewe na kile kipato kinachotokana na Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, simaanishi kwamba baada ya pale Halmashauri siziwape chochote, hapana. Lakini kiwape nguvu sasa walau ya kuweza kupata kitu chochote cha kuwasaidia.

Vile vile wasaidiwe vyombo vya usafiri, wana kazi kubwa sana ya kuzunguka ndani ya Kata kufutilia maamuzi na utekelezaji wa masuala yote yanayotoka Bungeni yanashuka kwenda kwa Madiwani. Hivyo wanayatekeleza vipi wakati hawawezi kupata usafiri. Ukizingatia pia na wenyewe wana matatizo kama ya baadhi ya Majimbo kwamba bado hatujaweza kuwa na Ofisi. Diwani hana Ofisi, hana usafiri, hana Msaidizi, hivi kwa namna hiyo anawezaje akafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nashawishika kuishawishi tena Serikali kwamba pamoja na kwamba hoja hii katika kipindi cha miaka mitano hajikubaliwa, lakini narudia kuiambia Serikali kwamba hoja hii bado ina uzito wake na sababu nilizozitoa mwaka wa kwanza mpaka leo wa tano bado zipo. Bado nashawishika kurudia kusema kwamba naomba Serikali iliangularie suala zima la kulipa posho fulani kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani ili kuweza kuona kwamba wanapata nguvu ya kufanya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaamini hoja nyingine wenzangu watachangia, basi nimpongeze sana Mkuu wangu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Kiwelu, kwa jinsi ambavyo anatusaidia kazi. Nimpongeze Mkuu wangu wa Wilaya ya Muleba, Ndugu Tappa, kwa jinsi anavyotusaidia kazi, nimpongeze na viongozi wote wanaosaidiana nao hakika wametuwezesha kufika hapa. (*Makofi*)

Lakini nisiwe mwizi wa fadhila niwapongeze na kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Muleba Kaskazini walivyoshirikiana nami katika kipindi cha miaka mitano katika kufanya kazi hii. Nami nina imani kabisa kwamba hawatatetereka, tutaendelea kuwa pamoja katika kipindi kingine kuikamilisha ngwe kubwa ambayo tumekwisha kuianza pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba na mimi nitoe salaam za rambirambi kwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero, Marehemu Abu Towegale Kiwanga. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali kule Chimwaga akiwepo ndugu yetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyechaguliwa kuwa mgombea Urais wa CCM wa Tanzania. Ninampongeza sana. (*Makofi*)

Nampongeza pia ndugu yetu, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa mgombea mwenza wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea Urais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Ninawatakia wote mafanikio mema na mimi nina imani CCM itapeta, itashinda na wale wanaofikiri kwamba watachukua madaraka, wataendelea kuyataja midomoni, wala madaraka hawatapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, kwa kazi nzuri, kwa hotuba nzuri ambayo ameonyesha hapa leo.

Lakini pia nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, pongezi alizozipata ni pongezi za kweli kweli, wala si zingine, maana huyu ni kiongozi mahiri na amekuwa anaonyesha umahiri wake hapa mbele yetu wote. (*Makofi*)

Nampongeza pia Katibu Mkuu wao, ambaye naye pia ni mchapa kazi na amekuwa akishirikiana na Waheshimiwa.

Lakini naomba pia nichukue nafasi kumpongeza Rais wetu, Rais Benjamin Mkapa kwa kazi kubwa ambayo amekuwa ameifanya kwa miaka kumi iliyopita. Kazi aliyoifanya ni kubwa, mwanzoni alipoanza na *privatization*, ubinafsishaji watu wengi walikuwa *sceptical* walifikiri kwamba mambo mengi hayatakwenda. Lakini leo sisi wote ni mashahidi, Mheshimiwa Benjamin Mkapa alikuwa na *vision*, alikuwa anajua anakokwenda na huko alikokuwa anakwenda ndiko kumetufikisha hapa, nampongeza sana. (*Makofi*)

Suala la madeni amelipigia kelele sana na hivi sasa lina *gain momentum*, kazi ambayo imefanyika ni kubwa, huko nje sasa hata wale wa nje wanaanza kufikiria suala la kusamehe madeni nchi maskini na hili ni jambo la kumpongeza sana maana alipoteuliwa kuwa kwenye vyombo vile vikubwa viwili kile cha *ILO* na sasa kwenye *Blair Commission* kazi anayofanya kule ni kubwa ya ku-sensitize watu ambao wamekuwa hawaelewi *special circumstances* za nchi zetu kuhusiana na madeni na jinsi yanavyo

affect maendeleo yetu. Kwa hiyo, tumpongeze sana maana mambo aliyoyafanya kwa Taifa hili kwa miaka kumi aliyotawala ni mambo ya msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika lakini pia itakuwa si vizuri kumpongeza Rais tu, tusimsahau Waziri Mkuu wetu, Waziri Mkuu amefanya kazi naye miaka kumi, si haba kama Waziri Mkuu, *a historical performance* ya huyu Waziri Mkuu lazima tumpongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa sana amefanya kila nyanja ameshiriki na mkiona hotuba aliyotoa ikifuatana na nyingine na bado nitawapongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, kuna vipaumbele kumi na mbili ambavyo vimetolewa katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, hongera sana Waziri wa Fedha. Vipaumbele vile vinaonyesha jinsi Serikali yetu ilivyokuwa ikifanya kazi na sasa inavyoendeleza mipango hiyo katika miaka inayokuja na vipaumbele vile vyote ni safi, ni sahihi ya kumkomboa Mtanzania kuondokana na umaskini, tuwapongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hata Waziri wa TAMISEMI alipokuwa akisoma hotuba yake leo amezungumza mambo ambayo yana *qualify* mambo waliyoyataja kule nyuma ya kwenda kwa *grass root* kwenda chini kwa Watanzania na mimi nawapongeza sana kwa sababu ni Watanzania hao walioko kule wilayani na kule mikoani ambao ndio watakao nufaika na mipango hii yote tunayoizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo ameionyesha na mimi nina imani tunakokwenda ni kuzuri na tunakokwenda ni sahihi, tutaongeza mapato ya wananchi wetu ili kuondoa umaskini wa kipato ambao unawakabili sana Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie mambo muhimu yanayogusa mkoa wangu. Kwanza kabisa nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kwa kazi kubwa ambayo amekuwa anaifanya katika mkoa ule toka amefika pale. Amejitätahidi sana kuhimiza elimu katika mkoa ule, ninyi mnajua Mkoa wa Kigoma ulikuwa nyuma sana katika elimu. Lakini kazi aliyoifanya sasa tunakimbilia kwenye sekondari school hamsini na zaidi. (*Makofi*)

Lakini sekondari tulizokuwa katika mkoa ule zilikuwa chini ya kumi na tano, lakini tunakwenda na mwaka kesho tutakuwa tumefunga karibu *secondary school* 69, hii ni pongezi kubwa kwa Mkuu wetu wa Mkoa amekuwa anakwenda kila Wilaya anahimiza elimu. Kila Wilaya anatembelea kila shule, kila *Secondary School*, wote anawahimiza pale panapostahili amekuwa anatoa mchango, kwa kweli nampongeza sana amefanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Sasa kwa upande wa elimu katika Mkoa wa Kigoma tumefika hatua kubwa tumeorodhesha, tumeandikisha wanafunzi wengi katika mkoa wa Kigoma. Tatizo la walimu ni kubwa naomba TAMISEMI wawasiliane na Wizara ya Elimu waendelee kushirikiana walimalize tatizo la walimu linalokabili shule zetu tupate walimu. Yako mashule mbalimbali ambayo yanawalimu wachache sana, lakini ukifika pale unaambiwa wana walimu watatu, wanafunzi wangapi mia saba, mia nane, hawa ni wachache sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba uwasiliane sana na Waziri wa Elimu, mtengeneze utaratibu mzima kama huo ni wa *training* basi mlenge zile sehemu ambazo zilikuwa nyuma nyuma zipatiwe walimu wakuendeleza kazi kubwa ambayo imefanyika. Maana ni elimu tu itakayotukomboa kutokana na umaskini, hakuna nchi iliyojikomboa na umaskini kama haikusitisiza na kuendeleza mpango wake mzuri wa elimu na mpango tulio nao sisi wa elimu ni mzuri tu na unahitaji kupongezwa wala asiwepo mtu wa kusema kwamba huu mpango si mzuri. Huu ni mpango mzuri na utatupeleka kuzuri sisi ni walimu tumefundisha, tunajua elimu maana yake tunakokwenda ni kuzuri sana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kasulu nampongeza sana yule *DC* wangu na yule Mkurugenzi, wamefanya kazi nzuri. Katika Wilaya ya Kasulu hususani Jimbo la Kasulu Magharibi, tumejenga *dispensary* kila kijiji, hakuna kijiji ambacho hakina *dispensary* katika Kasulu Magharibi, kila kijiji kina *dispensary*. Sasa shida iliyoko kwenye upande wa afya ni kwamba hospitali nyingi hazina *kit* za dawa, hospitali nyingi hazina watumishi, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sana wananchi wamejitolea sana wakajenga hospitali hizi. Sasa tupewe watumishi, tupewe *kit* za dawa, wananchi waweze kufaidi matunda yake maana si busara kufanya kazi kisha unaangalia kazi uliyofanya unaiona haikusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutaja ziko hospitali nyingi iko *dispensary* ya Muhunga, *dispensary* ya Kajana, *dispensary* ya Katundu, *dispensary* ya Songa, *dispensary* ya Rusaba zote hizi hazina dawa, hazina waganga pamoja na *dispensary* ya Nyakolongo zote hizi zinahitaji dawa na tukisaidiwa dawa wananchi watafurahi sana. Zingine zimekaa karibu miaka mitatu, miaka minne, zimemalizika watu wanasema hivi tulijenga jengo hili ili tulitazame tu au litusaidie? Hizi nilizozitaja zimejengwa muda mrefu sana na watu wetu tungependa wapate huduma zinazostahili pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukaendelea kuwasaidia, mipango ya nchi yetu ni lazima ianze huko vijijini *i-focus* vizuri katika Wilaya hizi kisha ndipo ipande juu. Ikipanda juu ndipo itaonyesha mikoa kama Kigoma inajihitaji nini, inahitaji barabara, maji, miundo mbinu, wafanyakazi wazuri wakuchanganua kazi zinazoendeshwa kule, bila haya hatuwezi kuzungumzia habari ya maendeleo kwa Taifa zima. Fungua barabara kwa Mkoa wa Kigoma tutalima sana maana sisi ni wakulima wakubwa, jenga *port* ya Kigoma tutauza sana mpaka Kongo, Burundi mpaka na Zambia tutapeleka mazao yetu. Barabara zikipatikana tutawauzia Kagera, Shinyanga, Tabora, tutapeleka mali nyingine zitapitia katika Mikoa ya Rukwa kwenda Zambia. Huo uwezo tunao na mkoa wetu ndio wenye *potential* kubwa ya kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya nayasema ndio ya msingi yanayoweza kutoondolea umaskini katika Taifa letu na mimi nina imani ya kwamba tukiyafanya tutakwenda vizuri. *NGOs* zimekuwa zinafanya kazi nzuri sana na mimi naomba nipongeze mashirika yote yasiyo ya kiserikali katika Mkoa wa Kigoma ambayo yamekuwa yanafanya kazi nzuri sana, wametujengea maji takribani katika Jimbo langu katika kila kijiji kasoro vile vijiji ambavyo juu ya mwinuko. Sasa hivi tunahitaji visima Serikali itufanyie mpango tupate visima ili watu wa Heru Juu wapate maji, watu wa

Rusaba wapate maji, watu wa Nyaruboza wapate maji na watu wa Mnanila wapate maji, hivyo vijiji vikipata maji Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imekamilisha kazi yake na tutaendelea kuipongeza tu wala tutakuwa hatuna maneno ya kusema tunapokuja kutoa hotuba hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa ujumla wake naomba niipongeze Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi iliyofanya kwa miaka kumi. Kazi iliyofanya kwa miaka kumi ni kazi nzuri sana inayohitaji kupongezwa na sisi wanachama wa Chama cha Mapinduzi tutaendelea kutesa na kutawala katika nchi hii na asitokee mtu wa kuanza kubeba mafanikio ambayo Chama cha Mapinduzi kiliyopata katika Taifa hili. Tunakwenda kwene uchaguzi na mwaka ujao tutachukua utawala na tutaendelea kutawala CCM itashika hatamu na Zanzibar itatawala na CCM itaendelea kushika hatamu, wale wanaosema tutakapotawala lakini hapo tutakapo tawala bado tunawapa miaka 50 mingine ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na mimi nitamke rasmi kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi. Nianze kwa kutoa pongezi za dhati sana kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa mambo yote ambayo Serikali yake ya Awamu ya Tatu ya Chama cha Mapinduzi imefanya mpaka sasa katika nyaja mbalimbali kukusanya mapato kudhibiti matumizi na kusogea huduma kwa wananchi, haya ni mafanikio ya kupongezwa sana. (*Makofi*)

Vile vile nichukue fursa hii kupongeza wagombea waliochaguliwa na Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uajo. Nikianzia na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye amechaguliwa kwa kugombea Urais kuititia Chama cha Mapinduzi na mgombea mweza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na vile vile Mheshimiwa Amani Abeid Karume, pongezi sana.

Mimi huwa napata ujumbe katika simu yangu ama kutoka kwa watu wa Jimbo langu au mahali pengine popote, sielewi lakini wanasema hivi na mimi naomba niuseme huo ujumbe hapa katika Bunge lako Tukufu, wanasema kwamba Mheshimiwa Jakaya Kikwete, anakubalika sio tu kwa wana CCM lakini hata kwa Wapizani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe ule unaendelea kwamba hakuna haja ya kufanya uchaguzi, atangazwe kuwa Rais moja kwa moja. Mambo kama haya safi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kutoa rambirambi kwa Marehemu Wabunge ambao wametutangulia mbele ya haki, naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Baada ya kusema hayo naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, katika maeneo mawili, matatu na yote yanalenga katika kuwezesha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana hatua ambazo Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI ya kutangaza maeneo mapya ya Halmashauri, Jiji, Manispaa, Miji na kadhalika. Hii ni hatua mojawapo ya kusogeza huduma kwa wananchi kwa hiyo, ni hatua ya kupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika aya ya 10 na aya ya 30 wakati Mheshimiwa Waziri anatangaza, tulistuka kidogo sisi Wabunge wa Kahama kuona kwamba Kahama haikutajwa jambo ambalo linashangaza sana kwa sababu tulikuwa tumefanya mawasiliano ya awali na ya karibu sana na Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda na tukakubaliana mtiririko mzima tunakwenda wapi, sasa lakini aliposema hapa Mheshimiwa Waziri kwamba Halmashauri ya Mji ni ya Mpanda tu, basi sisi tulistuka sana na pale pale tukapeleka ujumbe wa haraka haraka kwa Mheshimiwa Waziri. Nafurahi kusikia, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Mizengo Pinda ameniletea ujumbe akisema kwamba ye ye alikuwa amesahau tu na kwamba atafafanua, naomba kabisa kwamba basi tunasubiri kwa hamu Mheshimiwa Waziri afafanue hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwamba kilio chetu cha muda mrefu sasa kwamba kinatimia, Kahama inapata Halmashauri ya Mji. Lakini pamoja na hayo ya kushukuru niseme tu kwamba maamuzi kama hayo yanachukua muda mrefu sana, Kahama ni Mji ambaa umepanuka haraka sana katika miaka hii ya karibuni na tangu mwaka 1990, Halmashauri ya Mji wa Kahama ilikuwa iwe Halmashauri mapema zaidi tangu mwaka 1990 lakini mpaka sasa bado na mpaka sasa mwezi Julai labda ndio itakuwa Halmashauri ya Mji. Ni ngazi moja mbele kuliko ile Halmashauri ya Mji Mdogo tunashukuru sana, lakini tutashukuru zaidi kama katika miaka ya michache ijayo Serikali ifikirie kuifanya Kahama iwe Manispaa kwa sababu maendeleo yaliyopo naomba niseme wazi, matarajio yetu ya maendeleo ni kwamba, pamoja na kukua kwa misingi ya uchumi uliopo lakini kuna mgodi mkubwa mwingine unao kuja hivi karibuni, mgodi ambaa utakuwa mkubwa kama ule wa Bulyankulu, nao utakuwa hapo hapo karibu na Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake nini, maana yake ni kwamba wananchi wa pale watahitaji barabara, sio barabara hizi za changarawe hapa, watahitaji barabara za lami, tunashukuru Mungu kwamba mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria unaletwa, hilo tunashukuru sana watu wa Kahama kwamba utasaidia sana, lakini kuleta maji ya Ziwa Victoria katika Mji wa Kahama itamaanisha pia kwamba ile kasi ya kupanuka Mji itakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itarajie kwamba mahitaji ya ule Mji yatakuwa makubwa, maana yake nyingine ni kwamba miradi kama ya *sold west management* ya kimanispaa au ya kijiji pia ielekezwe katika Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia linahusu mgawanyo uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala. Hili na lenyewe ni suala zito, lakini inashangaza kabisa kwamba katika aya hii inayozungumzia uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala ni *paragraph* tena ndogo tu ya mistari mitano, sita, basi. Tulitarajia kwamba Mheshimiwa Waziri angetumia muda mrefu zaidi kuelezea kwa kina juu ya nini matarajio na mwelekeo wa Serikali kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 kufanyika na takwimu muhimu ya maendeleo kuanza kupatikana, matarajio yetu yalikuwa ni kwamba basi hizo takwimu zianze kutumika katika kuboresha maendeleo ya Watanzania. Lakini mpaka sasa hatujaona kwamba kuna mkakati mahsus (*Consistent Coherent Strategy*) ya kuzitumia hizi takwimu zinazotokana na sensa ya mwaka 2002 katika kuboresha maisha ya Watanzania, kuandaa mipango ambayo inalinga na hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni muhimu sana kwa sababu tunapozungumzia kusogeza huduma kwa wananchi, tunapozungumzia kuongeza maeneo ya utawala, hatuzungumzii pabaya mambo mengine isipokuwa kuboresha maisha ya Watanzania. Yapo maeneo makubwa sana kimaeneo ni makubwa kwa idadi ya watu, lakini pia yana mvuto mkubwa sana ya kiuchumi na kijamii. Lakini hayo maeneo yanafananishwa fananishwa na maeneo mengine ambayo labda hayana hivyo vigezo.

Sasa hali kama hiyo inaleta matatizo tunawaadhibu wananchi katika maeneo haya mathalan tuchukulie ya kiutawala, unakuwa na Wilaya kubwa kutoka pale *centre* mpaka incha ya mwisho kilometra 200 huku na huku ni vigumu kuyafikia sio tu kwa Mkuu wa Wilaya hata wale wahamasishaji wa maendeleo ni vigumu, haya maeneo lazima yaangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa nategemea sana kwamba wakati anafanya majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atalizungumzia hili kwa kina kuliko ambavyo amelizungumzia katika aya ya 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende suala moja lingine dogo la hatma ya Madiwani nchini, namshukuru sana Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa kulizungumzia hili na mimi kila mara huwa nafikiria kwamba hawa viongozi katika Kata wakisiasa, je, wenyewe maslahi yao yawe vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa katika upande mmoja na wafanyakazi ambao wanaajira rasmi Serikali, Mtendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji hawa wanaajira rasmi lakini cha kushangaza ni kwamba huyu Mwenyekiti wao wa *Ward DC* basi rai yake ni ya wasiwasi, hili linaleta wasiwasi. Ninaomba sana Serikali iliangalie kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie suala la mafunzo kwa Wahasibu, Serikali yetu ya Awamu ya Tatu kwa msukumo huo wa kupeleka rasilimali nyingi kwa wananchi ili kuwawezesha katika maendeleo yao umefanya kwamba fedha nyingi sana zina kwenda vijijini mahali ambapo katika wilaya viongozi wale wasimamizi wakuu wa fedha mahali pengine hawana utaalamu wa kutosha. Naomba sana Wizara hii ya

Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, ileezee mikakati ya kutoa mafunzo ya uhakika kwa hawa wataalam, vinginevyo kwa kweli haitaendelea kuwa ajabu kwamba baadhi ya Halmashauri hizo hati ambazo sio safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na wenzangu kuchukua nafasi kutoa nafasi za rambirambi kwa mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero na kutoa salaam hizi kwa wananchi wa Kilombero na Mkoa mzima wa Morogoro kwa kupotewa na kiongozi shupavu ambaye kwa kweli tulimpenda na tulishirikiana naye sana, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika nachukua nafasi hii fupi kumpongeza sana Rais wetu Benjamina William Mkapa, kwa kazi ambayo ameifanya miaka kumi. Ningesema tu kwa sentensi moja, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, ameinua heshima ya nchi hii na atakumbukwa katika historia kwamba aliweka misingi ambayo inaifanya Tanzania iende mbele ya Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii ya mwisho kuwapongeza kwa dhati kabisa wenzetu katika Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa ndani ya Chama cha Mapinduzi na kuchukua Bendera ya Chama chetu tayari kwa uchaguzi unaokuja, nachukua nafasi hii kwa niaba ya watu wa Singida kuwapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi ndogo kuzungumzia maslahi ya Mkoa wa Singida na mwenzangu Mheshimiwa Diana Chilolo, aligusia kidogo na mimi nataka niendeleze kidogo alipoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni kama vile Mikoa mingine ambayo kitu tunachokiita *natural harbour*, sisi Singida ni mkoaa uliokaa mahali makutano na *inter state commerce* inashamiri sana Singida hata bila msaada wa Serikali, *Transpotation Economics, Transit Economic* ya *movement* mbalimbali kutoka Dar es Salaam mpaka Burundi mpaka sehemu zote wote wanapitia Singida. Kwa hiyo, umuhimu wa Singida ilivyokaa kijiografia hata mtu ambaye haifahamu uko wazi kabisa na Mkoa wa Singida vile vile ukianzia Singida Mjini kwenda Babati, kwenda Arusha na Nairobi na ukianzia Singida kwenda Tabora na Shinyanga, Mwanza na Kagera, watu hawa wote lazima wapite Singida na kwa sababu uchumi wa nchi unaelekea kuwa kwenye *service economic* ndio dunia nzima Mataifa yaliyoendelea uchumi unaanzia kwenye *production*, malighafi kimsingi tukiendelea mbele uchumi utakuwa tu wa *service* kutoa huduma mbalimbali ndio zinafanya ule uchumi ukue na sisi Singida tuko mahali ambako hatuna hata sababu ya mtu aweye yejote kutuita sisi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii nafikiri tumeingiliwa na ukiri wa umaskini, Bunge hili kila tukijibowi maswali tutaambiwa kutokana na umaskini wa nchi yetu, kutokana na jinsi tulivyo mafukara na watoto wetu wadogo kule vijijini wanasikia mtoto yuko darasa la kwanza anasikia nchi yako ni maskini, baba yako mzazi maskini, mama yako maskini, shangazi yako maskini umezaliwa katika Afrika Bara maskini na neno umaskini linawachukua watu wengi nchini na mimi nafikiri imefika wakati sisi kama Taifa tuangalie *potential* zilizopo na tuzijengee hoja, wakati mwengine unaweza ukafikiri wewe maskini kumbe umekalia dhahabu ambayo itagundulika miaka 1000 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kujiaminisha kwamba *potential* ya Mkoa wa Singida na watu wa Singida haifanani kabisa na kuitwa umaskini na mimi ningeita upungufu wa vitu tulivyo navyo ni changamoto au *challenge* na tukiyatazama matatizo yetu kwa mtazamo huu nchi hii itaanza kuendelea mbele zaidi na zaidi. Benki ya dunia wanatuita sisi nchi maskini sana, lakini miaka ya 1960 nchi ya Korea Kusini ilikuwa maskini kama Tanzania, lakini wale wenzetu kufikia miaka miwili iliyopita wametolewa katika orodha ya nchi zinazosaidiwa duniani na nilitaka niseme kwa sababu Singida itashamiri kwenye *Inter State Commerce* tuna nafasi kubwa kama Mkoa kufaidi na wapita njia wote watakao kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niseme la kwanza kwamba Wizara iweke kipaumbele kwa mara ya kwanza kuhakikisha kwamba Manispaa ya Mji wa Singida inakuwa *harbour* ambayo itakuwa na nafasi ya kuwavutia *independent investors* waje wawekeze Singida kama alivyosema Mheshimiwa Diana Chilolo. Tuna nafasi kwenye *hotels*, sasa hivi mtu yejote akitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza hufiki wala hulali Dodoma lazima ukalale Singida, huna namna ya kulala hapa, lazima upite ukalale Singida.

Kwa hiyo, tuna namna nyingi sana ambazo naona kama nafasi pekee ya kufuta hili jina la umaskini na kuanza kufikiria *wealth creation*. Singida tuna ardhi nzuri na moja ya tatizo sisi tunaitwa maskini ni kwa sababu ile ardhi haina mtu, *it is almost like a no mans land* kwa sababu unaweza kwenda tu ukajichukulia. Sasa changamoto ambayo naitoa kwa Wizara hii na kwa nchi yetu lazima tupime vijiji vyote, hata yale mapori mwananchi wa kawaide awe na *title deed*, hata kama una heka tano kama zimepimwa na una-*title deed* wewe na ufukara haupo. Maana yake wewe unaitwa *land lord* saa ngapi unaweza ukamwita *land lord* ukamwita kabwela maskini? Miaka ya nyuma walichofanya wenzetu wakati wamewachukua hawa walalahoi wa Ulaya waliokuwa wafungwa, waliokuwa kitu gani wakachukuliwa Uingereza wakasafirishwa kule Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipofika Amerika ilikuwa ni mapori na mapori na kuna sehemu nyingi sana zilikuwa na magonjwa mengi sana ambayo yalikuwa hayana tiba. Kwa hiyo, watu waliogopa kukaa. Walichokifanya ile Serikali yao wakagawa hekta mia mbili, mia mbili, kwa mtu yejote ambaye alikuwa tayari kwenda kukaa katika hiso hekta 200 akazi-*develop* kwa miaka mitano Serikali ilimpa ile ardhi bure na ikampa na *title* ya kuzimiliki. Sasa hivi hekta 200 ni tajiri mkubwa sana kwa sababu ardhi ina thamani, kinachotokea Tanzania wageni wanakuja na kwa sababu ardhi yote ya Tanzania ukipita hapa mpaka Kondo, mapori unayopita hayana mtu na wale walioko pale

hawamiliki, itafika mahali wageni watakuja na kuchukua utajiri wetu. Kwa hiyo, ni marufuku kwa kiongozi kuita wananchi maskini wakati hatujachukua jukumu la kuwapimia ardhi kila mtu awe mmiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Mtanzania ye yote ambaye atastahili kuitwa maskini kwa viwango vya dunia kama ardhi yote tuliyonayo nchi hii itapimwa na wakamilikishwa wananchi. Hakuna Mtanzania anaye-*qualify* kuitwa maskini na mimi nafikiri kila wakati tunazungumzia sera ya kuboresha ardhi, nafikiri tumetoka mahali pa chini zaidi tumefika mahali.

Lakini ningesema wananchi wa kawaida wamilikishwe ardhi wapewe hati, ardhi iweze kupelekwa Benki na mtu akakopa pesa akafanya kazi. Ethiopia moja ya vitu ambavyo wana-*export*, wale watu wana-*export* wanariadha na nafikiri Kenya pia wamewafuata kwa karibu, moja ya *export staff* ya wao ni wanariadha kwa sababu wale watu wanakimbia kweli kweli. Nitoe mfano wa Tanzania kwa kuelekeza nguvu zangu pale Singida, sisi Singida tuna *manpower* ya kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unahitaji vitu viwili kubadilisha hii nchi. Jambo la kwanza unahitaji kumwambia wananchi wa kawaida wewe siyo maskini na unahitaji kumwezesha afike mahali, anaweza akamudu maisha yake yeye mwenyewe. Kwa sababu vijana wanakaa kijiweni kuanzia asubuhi mpaka jioni *wastage of time and sources*, *manpower* kwa sababu kila mtu anajua sisi ni maskini na wote wanasubiri Serikali. Ni lazima tuwaambie wananchi wetu Serikali haina uwezo wa kuwafanya wananchi waondokane na ule umaskini kwa sababu uwezo wa Wananchi kujitoa kwenye umaskini upo. Sisi wenyewe tunachohitaji ni kuwakabidhi vile vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina amini kwamba kama kila kijiji cha Singida kuanzia kijiji cha Modeda, Ntinko nenda mpaka Pohama, Busisi naweza nikaendelea kutaja mpaka vijiji 200. Kama kila kijiji kwanza kitapimwa na kila mwananchi wa Singida akapewa hati ya kumiliki ardhi na ile hati ya kumiliki ardhi ikamwezesha yeye kwenda Benki na kukopa fedha aendeleze kilimo au kitu anachoona kinafaa, maisha ya watu wa Singida yatabadilika. Hii biashara ya kuwaita maskini haitakaa iwepo tena na mimi ningependa na napenda kupendekeza badala ya kusema jitihada zetu ni za kupunguza umaskini.

Mimi ningependa kupendekeza ziwe jitihada za kujenga uwezo wa kila mwananchi kuwa tajiri kwa kadri anavyoweza *wealth creation*. Kwa sababu *wealth creation* inapendeza kusema, inapendeza kuzungumzia kwamba mtu ana uwezo wa kuzalisha akapata shilingi 500,000 kwa mwaka, lakini akifikisha milioni moja, milioni mbili, milioni tatu, huyo mtu anaendelea kuwa tajiri kuliko ilivyokuwa jana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirudie lile ambalo nililisema. Utawala wa nchi unakwenda sambamba na wananchi ambao wanaamini hali walijonayo, wananchi wa Tanzani wanaamini sana juu ya Serikali tulijonayo. Wananchi wa Tanzania wanaamini juu ya uwezo wao wa kushindana kiuchumi, naomba tuchukue hatua moja zaidi ya kumwezesha kila mwananchi wa nchi hii na kumnyima kila mgeni ardhi ambayo ndio urithi wetu tulipewa na Mwenyezi Mungu. Kwa kadri inavyowezekana tuifanye

iwe ngumu sana kwa mgeni wa aina ye yote kumiliki hata *ki-piece* kimoja cha ardhi ya nchi hii, kama yule mgeni hajashikamana na mwananchi ambaye ardhi imemilikishwa kwa jina la mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu ye yote anayeweza kuwekeza Japan kama Mjapan hayupo pembedi. Mbona waliweka hii Sheria siku nyingi hakuna kuwekeza Japan, hata kama ungetaka kufungua Kiwanda cha Lawalawa kama hujashikana mkono na Mjapani na useme yeye ndio yuko mbele yako wewe uko nyuma yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nguvu pekee *comparative advantage* ambayo anayo mwananchi wa kawaida, ni sisi kama Serikali tummilikishe huyu mwananchi ardhi. Vijana wote wanaofanya kazi hapa Dodoma, Dar es Salaam wazee wote walioko Dar es Salaam warudi nyumbani wamilikishwe ardhi. Hata kama anafanya kazi magorofani pale Buguruni lazima awe na *title* mikononi mwake yeye na mke wake wana ardhi yao. Popote walipotoka Tanzania itakuwa ni aibu sana nchi hii ifike mahali wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sasa hivi mtu akija na dola milioni moja akataka kununua pori lote la Kibaigwa si atalinunua? Watu wote watamuuzia kwa sababu kwanza hawana hati na pili namna ya kumiliki inategemea na mtu ana ng'ombe wangapi au ni nani ameweza kuwa baunsa akakamata eneo kubwa. Hakuna utaratibu, *roles of engagement* katika hili zoezi zima la kuimiliki nchi yetu halipo, halijachorwa.

Nawapa *challenge* Wizara hii mtafakari ni jinsi gani mtatengeneza *roles of engagement* kwa sababu ardhi ni sehemu muhimu sana ya utawala wa hii nchi. Huu utawala tunaouzungumzia ni nani anamiliki, nini katika nchi yako na nchi inafaidi nini kwa vinavyomilikiwa na nani, na watu gani vinaleta mstakabadhi wa Taifa.

Naomba nimalizie kwa kurudia lile nililolisema mwanzo kwamba nchi yetu imefika mahali inaheshimiwa na siyo tu inaheshimiwa, inaogopwa. Zamani ilikuwa ukiingia Tanzania unakutana the *bump road* ya kwanza utakayokutana nayo kama ulikuwa una-*drive* kutoka Kenya, unaendesa gari lako shimo la kwanza ukiingia kubwa lazima umefika Tanzania wanakwambia ebo! Tumeingia Tanzania. Lakini sasa ukiingia mahali pazuri umeingia Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nakushukuru sana. (*Makofî*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nasimama mara ya kwanza, naomba niungane na wenzangu kwa kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na wapiga kura wa Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya miaka yote kumi, ametutoa mahali pagumu sana na ametuacha mahali pazuri sana. (*Makofî*)

Pia naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na CCM kuwa mgombea wa Urais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa mgombe mwenza wake na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kugombea Urais Zanzibar. Mfano ambao CCM imeonyesha ni dhahiri na wakati huu tutashika pia hatamu za uongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri aliyetoa hotuba asubuhi kwa hotuba nzuri sana na naomba nipongeze wasaidizi wake wote na hapo naomba nianze kwa kusema naunga mkono hii hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Sasa katika maboresho yako, naomba mambo manne niyazungumzie. Katika ukurasa wa 10 wa kitabu cha hotuba Mheshimiwa Waziri anaeleza juu ya sekta ya ujenzi. Ni kweli katika maeneo yetu mengi barabara zimejengwa na miundombinu imeboreshwa. Lakini naomba niseme kuna sehemu ambazo zimesahauliwa, kwa mtu ye yeyote anayefika Dar es Salaam atajua kwamba siku hizi ili uweze kuwahi kazini asubuhi kutoka maeneo ya Kunduchi au Tegeta ni lazima uamke saa 11 alfajiri, saa 11.15 uwe barabarani. Kuna barabara moja tu inayoingia Mjini kutokea upande wa Bagamoyo, ile barabara ikikorofisha kwa njia yoyote pametokea ajali, kumetokea daraja limeharibika, basi siku hiyo hatuendi kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na barabara nyingine ya Bagamoyo, *Old Bagamoyo Road*. Siku nyingi sana tumeambiwa barabara hii inatengenezwa iweze kuwa barabara mbadala kwa sehemu zile ambazo kutoka Tegeta, Tangi Bovu nenda mapaka Bunju na Boko. Hatuoni maendeleo yanayofanyika. Tunaomba Serikali ifikirie kutupa barabara mbadala. Nashukuru sana Wizara ya Ulinzi pale Mlalakuwa wametuwekea daraja ambalo sasa lina umri wa zaidi ya miaka 10, daraja la kijeshi. Magari tunanyang'anyiwa pale kwenye daraja kwa sababu lazima tusubiriane kupita kwenye lile daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ile barabara ya Bagamoyo ya zamani ifufuliwe. Wakazi wote wa Dar es Salaam wenyе majengo wanalipa kodi ya majengo. Lakini ni jambo la kushangaza ukivuka Lugalo Jeshini barabara ya lami iliyoko ni ya Bagamoyo na ya kwenda kwenye mahoteli ya kitalii. Mvua zikinyesha watu hawawezi kuingia kwenye nyumba zao kwa sababu ya madimbwi, eneo lote la Tangi Bovu, eneo lote la *Africana* na eneo lote la Tegeta hayana barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wale pia ni watu wanaolipa kodi za majengo na wanastahili huduma. Watengenezewе zile barabara ili nao waweze kwenda kazini na sehemu nyingine kwa starehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo linakera sana wananchi wa Dar es Salaam, ni kweli ili amuliwa mawakala wawe wanakusanya kodi na siyo jambo baya kama kazi ikifanyika vizuri. Lakini pamoja na ukusanyaji wa kodi, Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam zinatumia mawakala kutekeleza sheria ndogo ndogo za Halmashauri, sheria za *parking*, sheria za afya na kama hizo. Wanatumia kampuni za udalali ambazo zile kampuni za udalali siyo *service oriented* ni *profit oriented*, hizi

kampuni za udalali nadiriki kusema ndani ya Bunge lako Tukufu zina ajiri wahuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi ukipita Jiji la Dar es Salaam utaona magari yanakokotwa hasa siku ya Ijumaa mchana, eti yame-park vibaya, eti yanasaafishiwa mahali pabaya ambapo hakuna ruksa na kadhalika. Jana nilikuwa pale Magomeni, magari yanasaafishiwa mlangoni kwa DC, hayakamatwi yale magari. Lakini unakuta haya makampuni ya udalali yanakwenda kukamata magari *Wazo Hill*, Boko kule, shamba kabisa. Wakikamata afadhali hata wakupeleke Mahakamani wakushitaki, wanadiriki kuendesha magari ya watu wanapeleka mpaka nyumbani kwa hao watu wanawadai pesa wanasema usipolipa shilingi 120,000 sasa hivi tunachukua gari. Naomba niseme nimekuwa *victim* wa tatizo hilo. Nimekuwa *victim* wa tatizo hilo na gari langu liko *Majembe Auction Mart* sasa ni mwezi wa saba, eti lilikuwa linaoshewa *Wazo Hill*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mke wangu akadaiwa shilingi 180,000 azitolee nyumbani. Faini ya kuosha gari mahali pasipostahili *maximum* ni shilingi 50,000. Rushwa tunailea sisi kwa watu tunaowateua. Wananchi wanaonewa, magari yanakamatwa. Naomba Waziri atizame hili jambo, ikiwezekana *enforcement* ya sheria za manispaa na Sheria za Halmashauri zipewe watu ambaو wamesomeshwa kufanya hiyo kazi. Hakuna sababu ya kuwa na watu ambaو wanafanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo lingine pale Jijini Dar es Salaam, tatizo la masoko, ni kweli tunalo Shirika la Masoko Kariakoo na linafanya vizuri. Lakini wakati umefika sasa lile Shirika lijitanue. Kuna soko lipo pale Tegeta barabarani. Kama watu hawagongwi lakini magari yanazuia watu. Watutizame pia, watengeneze masoko tuweze kwenda karibu na nyumbani badala ya kufuata vitu vyetu mbali Kariakoo.

Katika ukarasa wa 23 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amaeleza Bunge lako Tukufu kwamba kuna jitihada za kufanya ule mfuko wa kusaidia wanawake, vijana na watoto, Halmashauri zichangie asilimia 10. Akaendelea kusema kwamba wamefikiria hata kutumia mawakala katika kusimamia huu mfuko, naomba hilo jambo lirekebishwe. Mawakala katika kusimamia huu mfuko ni kukaribisha rushwa zaidi na ni kukaribisha upendeleo. Afadhali kuwe na Idara maalum ambayo inashughulikia hili jambo katika hizi Halmashauri. Pamoja na hayo pale Dar es Salaam, kutoa shilingi 50,000 kwa mama lishe, shilingi 30,000 kwa mama lishe mwingine, nafikiri ni jambo ambalo halitaondoa umaskini. Kwa nini vikundi visiungane, tuseme vikundi vya wavuvi, vikundi vya mama lishe wakapewa mtaji wa kutosha? Kama wavuvi wakapewa boti moja, wakapewa na nyavu ni shilingi milioni mbili au tatu, tukaanza kidogo kidogo badala ya kusambaza pesa nyingi kwa watu wengi ambazo hazifanyi kazi na hazirudishwi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri viundwe hivi vikundi hasa katika Wilaya ya Kinondoni. Wananchi wa Ununio, Mbweni na Kunduchi waweze kufanya biashara ya uvuvi vizuri zaidi.

MBUNGE FULANI: Hasa Kawe.

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Nasema hasa Kawe.
(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kushughulika suala la elimu hasa elimu ya msingi vizuri sana. Sasa hivi watoto wengi wako kwenye shule, tunaona shule zinavyojengwa, lakini pamoja na hayo bado walimu wanaishi maisha duni sana. Tunaomba Serikali iwafikirie zaidi. Kuna *complaint* moja kubwa sana ya walimu, makato wanayokatwa kwenye Bima ya Afya lakini hayatoshelezi kuwatibusi. Mimi nafikiria pamoja na hiyo Bima ya Afya hizi Halmashauri za Miji na za Wilaya zifikirie namna ya kuongezea kidogo zile pesa ambazo walimu wanakatwa ili waweze kupata matibabu ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nikae na niseme naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti na ile ya majumuisho.

Mimi ninahakika kabisa yale ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu kila mmoja wetu ameyasikia na yule asiyeyasikia ana matatizo yake labda ya kusikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa hotuba yake nzuri na vile vile Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo siku zote amekuwa anatufanyia humu ndani ya Bunge. Mimi nitangulie kusema kabisa kuwa naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo machache na nianze kwenye usajili wa vijiji. Zoezi hili huanzia kwenye ngazi ya kitongoji au mitaa wanapoamua kuomba wasajiliwe kama kijiji. Vitongoji au mitaa huenda kwenye uongozi wa vijiji mama ili kupeleka maombi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uongozi vijiji mama umekuwa kikwazo kikubwa katika maeneo mengine katika mchakato huo. Mara nyingi vijiji mama hukwamisha maombi ya vitongoji au mitaa kuomba usajili na zipo sababu za msingi ambazo vitongoji hivi au mitaa hii huombea kwanza kabisa vijiji vingi uongozi wake ni mbaya. Sasa wale walioko kwenye vitongoji huona kama hiyo ni kero kubwa na kama ni kikwazo katika maendeleo yao. Lakini lingine vile vile vitongoji hivi viko mbali na vijiji mama kwa hiyo, kupata huduma inakuwa siyo rahisi na ndio maana pale kitongoji au mtaa unapokuwa na sifa ya kuwa kijiji ndipo hutamani kuwa kijiji. Sasa unapopeleka maombi yao kwenye ngazi au kwenye uongozi wa kijiji mama mara nyingi uongozi huo huwakwamisha, maana uongozi wa kijiji mama unadhani kuwa kwa kuruhusu vitongoji vyake au mitaa yake kuwa vijiji basi vijiji mama hivyo vinapoteza sifa ya kuwa vijiji.

Sasa wanapokwamisha juhudhi hizo mara nyingi hukaa kimya, hawawaambii kuwa jamani hili haliwezekani, matokeo yake vitongoji au mitaa husubiri kwa muda mrefu wakijua kuwa maombi yao labda yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalieleza hili kwa sababu limetokea kwenye Jimbo langu la Nanyumbu, vipo vitongoji kadhaa ambavyo vimeomba maombi hayo. Lakini cha ajabu ni kwamba ukienda ngazi za juu kuulizia wanasemwa hawajapata maombi hayo.

Kwa hiyo, naomba Serikali iweke utaratibu mwengine badala ya vitongoji kupitia kwenye uongozi wa vijiji mama, vitongoji vingepeleka maombi haya moja kwa moja kwenye ngazi ya Kata. Hapa naomba ngazi ya Kata wasiwawekee mizengwe viongozi hawa wa vitongoji kwa kuzuia maombi hayo bali wahakikishe wanayawakilisha kwenye ngazi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji au vitongoji vingi ambavyo vinaomba kuwa vijiji, vinavyo sifa zote zinazotakiwa kuvizua visipate hati za vijiji kwa kweli ni kuwarudisha nyuma kimaendeleo. Naomba viongozi wa Serikali wabadili utaratibu huo ili vitongoji vingi viweze kupata hati za vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu kuna maeneo ambayo mpaka sasa hivi hayajapata vijiji. Maeneo kama ya Mtawatawa kwenye Kata ya Nanyumbu, kuna Chang'wale na Mchenjeuka kwenye Kata ya Lumesule. Inasemekana kuwa maeneo hayo walikwishapeleka maombi zamani pengine hata mimi sijafika Bungeni lakini hadi leo maombi hayo hayaonekani sehemu yoyote. Nimekwenda Wizarani wakaniambia hayapo pamoja na kwamba kuna vijiji vinne ambavyo vimeonekana na vimepatiwa usajili lakini mpaka sasa hivi hata hivyo vijiji vinne hati au cheti mpaka leo havijapata. Kwa hiyo, naomba kwanza utaratibu ubadilishwe ili kuruhusu maeneo mengi zaidi yaye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeomba kuchangia ni kuhusu maombi ya Wilaya mpya ya Nanyumbu. Sisi wananchi wa Masasi tumeshapeleka maombi ya kupatiwa Wilaya mpya kwa maana ya kugawa Wilaya ya sasa ya Masasi ili ziwe Wilaya mbili. Sababu za msingi zipo zikiwemo kwanza za ukubwa wa Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Masasi hivi sasa inachukua eneo la 53% ya Mkoa wa Mtwara na Wilaya zingine za Mkoa za Mtwara nne ndio zinachukua eneo la 47% iliyobaki. Wilaya nyingine hizo ni Tandahimba, Newala, Mtwara Vijijini na Mtwara Mjini. Mgawanyo huu hauutendei haki kwa kweli Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na takwimu zinazopatikana kwenye kitabu cha orodha ya majedwali yanayoambatana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona haya yafuatayo:-

Kuna ruzuku ya Matumizi ya Kawaida, Wilaya ya Masasi imetengewa shilingi 4,153,885,900 ya mishahara, shilingi 1,153,547,800 kama matumizi mengineyo na shilingi 645,024,100 kama *General Fund purpose* lakini Wilaya nne za Mkoa wa Mtwara

zilizobaki zikiwekwa pamoja zimetengewa jumla ya shilingi 5,902,635,100 kama mishahara, shilingi 1,879,231,800 kama matumizi mengineyo na shilingi 767,025,500 kama *General Fund purpose*. Ukiangalia takwimu hizi utaona moja kwa moja kuwa Wilaya ya Masasi pamoja na ukubwa wake lakini inapata kidogo. Hali ni hiyo hiyo kwenye majedwali mengine kwa mfano jedwali namba 10, ukurasa wa 28 na majedwali mengine ambayo yanapatikana kwenye kitabu hicho.

Mimi naiomba Serikali iangalie upya uwezekano wa kukubali maombi yetu hayo ili angalau kuisaidia Wilaya ya Masasi ambayo sasa imeonekana kupunjika kimgao kwa ajili ya fedha za maendeleo iweze kupata haki yake nayo iweze kupata maendeleo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu daraja la Mto Lukwamba. Daraja hili lilizolewa na maji miaka mitatu iliyopita kulipokuwa na mafuriko kwenye Mto huo na toka kipindi hicho mpaka sasa kwenye Mto ule hakuna daraja. Tathmini ya Wilaya kwanza daraja lenyewe lina urefu wa mita 43 na gharama za ujenzi zimekadiriwa kuwa shilingi milioni 250. Sasa kwa kiasi hicho cha fedha ni dhahiri kuwa Wilaya isingeweza kupata fedha kutoka kwenye mgao wake kwa ajili ya kujenga daraja hilo. Kwa hiyo, Wilaya imepeleka maombi angalau ya kusaidiwa ujenzi wa daraja lingine. Sasa huu ni mwaka wa tatu nasikitika kusema kuwa hakuna maendeleo yoyote ambayo yamekwishaonekana mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *nature* ya kuzolewa daraja lenyewe kwanza ilikuwa ni maafa. Kwa hiyo, mimi nilitegemea kuwa suala la daraja la Mto Lukwamba lingeingizwa kwenye mpango wa maafa, mpango wa haraka haraka ili kufungua mawasiliano ya wananchi wale walioko upande wa pili na sehemu nyingine ya Masasi inayobaki. Hivi sasa wananchi wa vijiji vilivyoko upande huo, wakati wa masika Mto unapofurika wanashindwa kusafiri hivyo wanakuwa wametengwa na sehemu nyingine inayobaki ya Masasi lakini vile vile na sehemu nyingine ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa daraja hili licha ya kuwaunganisha wana vijiji walioko upande ule lakini vile vile upande ule ndiko kwenye makao makuu ya hifadhi ya Pori la Lukwika Lumesule. Kwa hiyo, wafanyakazi walioko upande ule na hata watalii wanaokwenda kuwinda kwenye maeneo yale, wakati wa masika hawawezi kwenda au hawawezi kwenda upande wa pili hivyo kupunguza mapato kwa Serikali maana watalii hawawezi kwenda kule. Sasa naiomba Serikali kuona umuhimu wa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa barabara safari hii nilipokwenda nimekuta wanaitengeneza vizuri tu lakini kama barabara itatengenezwa vizuri namna hiyo lakini daraja halipo, ina maana kuwa umuhimu wa hifadhi hiyo kwa kweli utakuwa umepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe tu Serikali kuwa wananchi wa maeneo yale wamesubiri kwa muda mrefu sana, miaka mitatu bila ya mawasiliano kwa hiyo, naomba wasaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini vile vile nitamke na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa shughuli za leo tumeishia hapo. Kama mnavyofahamu, hoja hii itaendelea kujadiliwa kesho na ndipo jioni mtoa hoja atafunga mjadala wa hoja hii.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
Tarehe 22 Juni, 2005 saa tatu asubuhi)*